ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni

19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Saba - Tarehe 26 Mei, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

UTARATIBU

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Naibu Spika, ili Baraza lako tukufu liweze kufanya shughuli zake linahitaji kupata *quorum* ya nusu ya Wajumbe na tukiangalia ninaona idadi hairuhusu.

Mhe. Naibu Spika: Katibu hesabu Wajumbe. Wajumbe 25.

Wajumbe waliopo nje waingie ndani tuanze shughuli zetu. Wajumbe muliopo nje muingie ndani tuanze shughuli zetu.

Waheshimiwa Wajumbe tunaahirisha kikao chetu kwa muda wa dakika 5 ili Wajumbe waweze kuingia na tupate *quorum*.

(Saa 3.04 Kikao kiliahirishwa)
(*Saa 3.10 Kikao kilirudia*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninaona nizungumze kidogo kwamba Bunge ni kitu muhimu na bado naona Waheshimiwa hatujaona umuhimu huo kuufanya katika kikao chetu hiki. Sasa naomba Kamati ya Uongozi tutatoa maamuzi ya kila mtu aliyechelewa achukuliwe adhabu gani sasa hivi. Kwa sababu wapo wanaowahi na wapo watu wanafanya kama leo nitake niende sasa hivi.

Hivyo Kamati ya Uongozi itakuja kutoa uamuzi kila anaechelewa achukuliwe adhabu gani. Kwa hivyo tunaendelea, Katibu.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 5

Utaratibu wa Ndege Kufanya Safari Bila Rubani Msaidizi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kukupongeza kabisa kwa uamuzi uliochukua hivi sasa kwa kutowajibika kwa baadhi ya Wajumbe wako kwa kuchelewa. Naomba swali la Mhe. Saleh Nassor Juma Nam. 5 kupitia ruhusa yako lijibiwe.

Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba mara nyingi imekuwa ikipata huduma ya usafiri wa anga kupitia makampuni binafsi kama vile *Zan Air, Coastal Air Services, Flight Link, Tropical Air* nakadhalika. Kwa kuwa kampuni hizi katika kutoa huduma zake mara nyingi hutumia rubani mmoja tu na kile kiti cha msaidizi rubani *(Co-Pilot)* huuzwa kwa abiria.

a) Je, mamlaka inayohusika na usafiri wa anga inaelewa jambo hilo.
b) Kama mamlaka inaelewa suala hilo je, ndege kufanya safari zake bila ya kuwa na rubani msaidizi si kwenda kinyume cha taratibui za usafiri na usafirishaji katika njia ya anga.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 lenye (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania ambayo ndio inayohusika na usafiri wa anga inalielewa jambo hilo.

Mhe. Naibu Spika, ndege iliyosajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa na idadi ya marubani inayopaswa kama ilivyoainishwa katika kitabu cha mwongozo cha aina ya ndege husika *(aircraft flight manual).* Idadi ya marubani kwa ndege iliyosajliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa shughuli za kibiashara, haitoakuwa na idadi pungufu ya marubani walioainishwa katika uundwaji wa ndege hiyo ambayo mara zote huwekwa katika kitabu cha mwongozo cha aina ya ndege husika *(aircraft flight manual).*

Mhe. Spika, mmiliki wa ndege, kwa kuzingatia mazingira ya uendeshaji anaweza kuweka katika kitabu cha uendeshaji *(operation manual)* idadi ya marubani watakaorusha ndege husika. Hata hivyo, idadi hii haitakiwi kuwa pungufu ya ile iliyoelekezwa na mtengenezaji wa ndege hiyo *(aircraft flight manual)* au cheti kinachoruhusu ndege kuruka *(certificate of airworthiness)* kinachotolewa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga.

Mhe. Naibu Spika, ndege iliyosajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa shughuli za kibiashara yenye uzito wa kilo 5,700 ulioruhusiwa kuifanya iruke *(maximum certificate take - off weight)* inatakiwa kuwa na marubani wasiopungua wawili (2).

Hii ina maana kuwa ndege yenye uzito chini ya kilo 5,700 inaruhusiwa kuendeshwa na rubani mmoja hata kama ina abiria 9 au zaidi ilimradi hairuki katika mazingira ya uendeshaji ndege kwa kutumia *instrument flight rules* au kuruka kwa wakati wa usiku.

Mhe. Naibu Spika, maelezo ya uundwaji wa ndege ambayo yamekuwa katika kitabu cha mwongozo cha aina ya ndege *(aircraft flight manual)* ya *CESSNA 208 (CARAVAN*) ambazo zina uzito usiozidi kilo 5,700 na zinatumika sana na waendesha biashara ya ndege kwa kubeba abiria yanabainishwa kuwa ndege hizo zimetengenezwa kwa mfumo wenye uwezo wa kubeba abiria 13 au chini ya yake ikiwa na rubani mmoja.

Aidha, maelekezo ya *ICAO* yanazuia ndege aina hii kuruka katika mazingira ya *intrument flight rules* au usiku ispokuwa kama imeruhusiwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga. Mamlaka pia katika kutoa ruhusa hiyo inatakiwa kuzingatia mambo kadhaa yaliorodheshwa ikiwemo la kwamba ndege hiyo isiwe na ruhusa ya kubeba abiria zaidi ya tisa (9) hata kama ruhusa yake kubeba abiria zaidi ya 13.

a) Mhe. Naibu Spika, majibu Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania ambayo ndiyo inayohusika na usafiri wa anga inalielewa suala hili.
b) Mhe. Naibu Spika, kama ndege iliyolazimika kuwa na rubani msaidizi kwa maana ya kuwa na marubani wawili, pindi ndege hiyo ikifanya safari zake bila ya kuwa na rubani huyo, kufanya hivyo ni kosa na kwenda kinyume na taratibu za kiusalama wa usafiri wa anga na hatua stahiki zitachukuliwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutojibu swali la msingi, anasemaje iwapo rubani mmoja atashikwa na matatizo, Mwenyezi Mungu ajaalie isije ikatokea mshipa au ngiri na wakati ndege ikiwa angani.

a) Je, wale wataalamu Wazungu waliotengeneza ndege ile hawakulizingatia hilo au kutokuwa na akili hao Wazungu.
b) Ndege nyingi Zanzibar zimekabiliwa na uchakavu, ni chombo gani kinachosimamia, tumeshuhudia ndege nyengine hata kufungwa waya hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

a) La kwanza nilikuwa ninamuomba tu Mhe. Mjumbe kwamba hili la kusema kuwa majibu hayakujibu swali lake la msingi si kweli. Maana wewe umeuliza la kwanza kama mamlaka nalielewa au halielewi. Jibu kwamba mamlaka inalielewa.

b) La pili ukauliza kama kufanya hivyo ni kinyume au si kinyume na sheria. Tumekujibu kwamba kufanya hivyo ni kinyume na sheria, sasa sijui majibu gani unayotaka.

Sasa suala la rubani mmoja tumeeleza kwamba kwa mujibu wa utaratibu wa ndege, ndege inapoundwa, mtengenezaji ndege anatoa *flight manual* ambayo inaongoza kwamba ndege hii itarushwa na rubani mmoja ama mawili. Kitabu kinavyoelekeza kama ndege itazimika kurushwa na marubani wawili huwezi ukapunguza ukaweka rubani mmoja. Pindipo kitabu cha kutengenezea ndege na kitabu cha *operation* mwenyewe amekubali ndege irushwe na rubani mmoja, hulazimiki mamlaka kumlazimisha mtu ndege kurushwa na marubani mawili.

Sasa kama kuna masuala ya ubinadamu, hayo ni masuala mengine lakini sheria hailazimishi. Utaratibu wa ndege upo vizuri kwamba rubani kabla ya kurusha kuna taratibu zake lazima awe amezipitia.

Jambo la pili, anazungumzia suala la uchakavu wa ndege. Mhe. Naibu Spika, ndege kama tutafuata *principles* zake sitegemei kama ndege itakuwa chakavu. Kwa sababu ndege inaruka kwa mujibu wa masaa na kila kifaa kinahitaji mabadiliko kwa mujibu wa maelekezo ya mtengenezaji na mtu ambaye anafanya *operation*.

Kwa hivyo kama masaa ya tairi yamekwisha unatakiwa kubadilisha tairi, kama masaa ya *engine* yamekwisha unatakiwa kubadilisha *engine*, kama masaa ya viti yamekwisha unatakiwa kubadilisha viti. Kwa msingi huo ndege hutegemei kuwa chakavu. Ndege siku zote itabakia kuwa usafiri mzuri na iliyo salama. Msingi ni kusimamia taratibu na maelekezo ya utengenezaji na utoaji wa huduma wa usafiri wa ndege.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza nitoe pongezi kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kuhusu suala hili. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi nina maswali mawili;

a) Kwa sababu ndege hizi siku zote zinakuwa na rubani mmoja lakini ukitizama kimaumbile sehemu ile ya rubani inaekwa kwa marubani wawili; rubani na msaidizi. Je, hawa waliotengeneza ndege na kuwa inaruhusika kusafiri kwa mtu mmoja, kwa nini wakaweka sehemu ya rubani wa pili. Hilo ni la kwanza.

b) Tunapoangalia tunaposafiri tunatumia ndege za aina mbali mbali kama zilivyotajwa hapa lakini kwa namna gani mwananchi anatakiwa alipe kwa ndege yoyote, mfano kutoka Unguja kwenda Pemba na sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilisi maswali yake (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, tumeeleza kwamba ndege kule mbele inakuwa na sukani mbili. Lakini katika suala la uendeshaji kuwa na marubani wawili inategemea maumbile ya ile ndege pamoja na yule mwenyewe anaye-*operate* ile ndege. Kwa maana kwamba ikiwa aliyetengeneza ndege amelazimisha ndege hii irushwe na marubani wawili, huwezi ukarusha kwa rubani mmoja. Kuwepo usukani wa pili, *it means* ni *option*. Kama wewe unataka kurusha na marubani wawili huzuuiliki lakini sheria hazikulazimishi ndege ambayo ina uzito usiozidi kilo 5,700 hairushwi usiku, haitumii *instrument*, haikulazimishi kwamba wewe ndege hiyo ni lazima irushwe na marubani wawili. Kwa hivyo kuwepo kwa kiti au sukani wa rubani, *it means option*, ukihitaji unaweka rubani wa pili, huhitaji, sheria inakuruhu kuwa na rubani mmoja.

b) Chombo kilichopo kina-*regulate maximum fee*, kwa maana kwamba bei isizidi hapa. Kupunguza hata ukiweka shilingi kumi sisi haituathiri. Msingi usizidi kile kiwango ambacho kimeekwa.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ingawa umenidhibiti kwa kuniambia dogo kabisa, kwa hivyo na mimi nitajitahidi liwe dogo kabisa.

Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na nimpongeze sana kwa upeo wake na ujuzi katika fani hii ya anga jinsi alivyokuwa akifafanua.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri ipo siku na mimi nilibahatika kuwepo katika safari ya kwenda Dodoma kwa ndege na ilikuwa ni ndege ndogo yenye *pilot* mmoja na mimi nilibahatika kukaa kile kiti cha pili chenye usukani, yaani cha *Co-pilot*.

Sasa kwa bahati mbaya katika safari yetu ile yule *pilot* ama rubani alibanwa na tumbo la kuendesha na lilimsokota vibaya sana, kwa sababu nilimuona tangu tunaanza kuondoka hali ilikuwa si nzuri. Kwa bahati nzuri wale wenyewe wana mbinu zao mule ndani, wana kidoo chao kule nyuma ya ndege kabisa. Kwa hivyo alitoka pale akaweka *auto pilot* na ile ndege niliachiwa mimi, lakini sikuigusa.

Sasa baada ya kurudi mimi nilimuuliza yule rubani mbona ikikuta hali kama hii inakuwaje. Akaniambia kwamba katika safari iliyokuwa haizidi saa mmoja basi anaruhusiwa *pilot* mmoja lakini ikiwa ile safari inazidi muda wa saa moja inakuwa hairuhusi.

a) Sasa ningemuomba Mhe. Naibu Waziri anitolee ufafanuzi juu ya suala hilo kwamba je, na muda pia unachukuliwa au ni sheria zile nyengine tu.

b) Sheria za kimataifa za *ICAO* wao wanapanga sheria zao kwa ndege ndogo. Sasa nilikuwa ninataka nijue pia sheria zile sisi tunafuata za kimataifa au kidogo hapa Tanzania tunafuata sheria zetu za *Civil Aviation Athority*. Mhe. Naibu Spika, ahsante.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, suala la msingi liliulizia suala la kwamba kama mamlaka inafahamu au haifahamu. Na suala la pili lilikuwa linahusiana na suala la kisheria.

Sasa sijui kama muda nao unazingatiwa ama vipi. Inawezekana ikawa muda unazingatiwa lakini katika msingi wa kisheria ni kupima uzito, urukaji wa ndege kwa kutumia vyombo. Maana wanachosema hata hii *instrument* kwa maana kwamba kuweza kurusha ndege usiku pia nayo inaathiri kwa rubani mmoja, kurusha ndege kwa kutizama kwa macho au kwa vifaa, nayo pia inaathiri kuwa na rubani mmoja.

Jambo la msingi kwamba yawezekana ikawa na muda nao pia unachangia, maana msingi wa swali lilivyoulizwa na safari inazozifanya zipo chini ya muda saa moja.

Jibu la pili, Mhe. Naibu Spika, *Civil Aviation* ya Tanzania inatunga sheria zake lakini msingi mkubwa tunafuata maelekezo ya *ICAO*, na *ICAO* maana yake ni *regulator* wa *operation* za ndege duniani nzima. Kwa hivyo ukitunga sheria zako unatunga sheria za ku-*administer* ile taasisi lakini *regulations* za ku-*oporate* ndege lazima ziandane na *ICAO*.

Kwa hivyo *standards* tulizokuwa nazo sisi, tunapofuata *standards* za *ICAO it means global wide*, sote tunatumia vigezo na viwango vilivyo sawa. Kuna sheria ambazo tunatumia sisi lakini *administration* zinaweza zikatofautiana na nchi nyengine, lakini utaratibu wa *regulation* lazima tuendane na *ICAO* kama zilivyo nchi nyengine zote.

Kwa sababu ndege inatoka nchini kwako inakwenda nchi nyengine, sio kitu ambacho unaki-*manage* katika *boundary* moja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Waziri majibu ya nyongeza.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Kwanza ninapenda nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu aliyotoa. Nilikuwa na nyongeza ndogo tu ya hii *part b* kuhusu suala la ndege hizi na namna tunavyofuata sheria za *ICAO*.

Kwa bahati nzuri sisi tulipata ziara wiki mbili zilizopita ya Katibu Mkuu wa *ICAO* hapa Zanzibar, alikuja. Mimi binafsi nilimuuliza suala hilo kuhusu taratibu na sheria za ndege ndogo. Akasema kwamba *regional laws* ndizo zinazotumika kwa kufuata vigezo kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, kwamba ile taasisi ambayo ipo hapa, ndio inayotunga taratibu za ndege ndogo na *operation* zake, wale wanashughulika na zile ndege za kimataifa. Kwa upande wa miongozo ni ile ile wanayotoa *ICAO*. Kwa hivyo kwa ufupi hizi ndege ndogo tunazo-*operate* hapa ni *TCCA* ndio wanaozipangia utaratibu wake.

Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri tunaendelea.

Nam. 64

Mapato Yanayopatikana na Usafiri wa Anga

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Anga ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano na ndege zinazoruka kwa kutumia anga ya Tanzania zinaingiza mapato mengi sana.

a) Wizara inaweza kuwambia wananchi kiasi gani cha mapato yaliyopatikana kutoka kwa ndugu zetu wa Tanzania Bara.
b) Na kama hazidaiwi ni lini kamati itaundwa kufuatilia fedha hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 64 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba anga ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndege zinazoruka kwa kutumia anga ya Tanzania zinaingiza mapato. Kwa mujibu wa sheria za Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*ICAO*) mapato yatokanayo na shughuli za uongozaji wa ndege ni vyema vikatumika kuweka katika maslahi ya watumishi kwa ajili ya mafunzo na ununuzi wa mitambo ya kuongozea ndege pamoja na matengenezo yake. Pia kulipia ada mbali mbali za mashirika ya kimataifa.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba mapato ya anga ni utaratibu unaotokana na utaratibu wa huduma za kianga zinazotolewa kwa wale wanaotumia anga hiyo pamoja na huduma za kiusalama, yaani kwa kupata mwelekeo, maelekezo ya anga katika anga husika.

Hii ina maana kwamba ndege inapopita juu kwenye anga husika, lazima ardhini kuwe na vifaa vya kuongozea kwa ajili ya usalama na huduma nyengine. Aidha, kwa kipindi cha 2009/2010 hadi 2012/2013 jumla ya shilingi milioni mia tano na tisini, mia tano na thalathini na nne na mia mbili zilikusanywa kwa huduma hizo.

Jumla ya bilioni nne, milioni mia tano hamsini na saba, laki tano na tisini na saba na nne zilitumika kwa kuimarisha huduma ikiwa katika kiwango chote hicho kinachotolewa na *TCCA*.

b) Hatuoni sababu ya kuunda kamati kwa kutambua ukweli kwamba mapato yetu ni kidogo sana ukilinganisha na matumizi tuliyoyafanya kwa msingi wa kutoa huduma bora na za salama za uongozaji wa ndege katika anga ya Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri hivi sasa, naomba kumuuliza swali dogo moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, watumishi wa Mamlaka ya Anga wa Tanzania wapo wangapi na mapato yanayokusanywa Zanzibar inapata gawio lake kwa asilimia mingapi kwa muda wa miaka mitatu.

Pili, kwa nini shughuli zinazofanywa na Mamlaka ya Anga ya Tanzania zisitiwe na viwanja vya ndege Zanzibar wakasimamia wao *ZAA*.

Mhe. Naibu Spika: Anasema Mhe. Naibu Waziri hakusikia, rudia tena kidogo, rejea tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, naomba Mhe. Naibu Waziri anisikilize kwa makini.

Pamoja na majibu aliyotoa Mhe. Naibu Waziri mazuri watumishi wa Mamlaka ya Anga Tanzania wapo wangapi na mapato yanayokusanywa Zanzibar, inapata gawio lake kwa mwaka kiasi gani. Kwa bahati mbaya Waziri umenipa gharama za uendeshaji tu za malipo ya mishahara, ninataka kujua Hazina Zanzibar inapata kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, swali lake la msingi lilikuwa kwamba anataka kujua mapato.

Tumemuelezea mapato yaliyogaiwa na Zanzibar ambayo tumesema ni milioni 590 na tumekuambia mapato kwa maana kwamba matumizi sasa ambayo yamefika bilioni 4.

Suala lako la idadi halisi ya watumishi naomba uniruhusu nikuletee kwa maandishi. Lakini mapato ni kwamba tumeweza kukusanya shilingi milioni 590,534,200. Kwa upande mwengine tumeweza kutumia shilingi bilioni 4,597,596,704. Haya ni kwa maana ya mapato, matumizi ambayo yametokana na fedha zilizotoka *TCA* kwa kuwalipia wafanyakazi wao, kununua vifaa, kufanya matengenezo ya mitambo pamoja na huduma nyengine, ukitoa yale mapato ambayo sisi tumeweza kukusanya milioni 500, matumizi yamekuwa bilioni 4. Kwa hivyo, karibu bilioni 4 na zaidi zote zimetokana na mapato yaliyotokana na *TCA* katika kuimarisha huduma za utoaji wa huduma katika masuala haya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali langu nambari 2 Mhe. Naibu Waziri nafikiri hakulisikia. Nilimwambia nataka kujua Hazina Zanzibar kwa muda wa miaka mitatu imepata kiasi gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, suala la Hazina mimi halinihusu. Mimi nilichokisemea taasisi yangu imekusanya kiasi gani na imetumia kiasi gani. Kama kuna mapato ya Mfuko Mkuu wa Hazina, hayo hayatuhusu sisi. Sisi tunazungumzia taasisi ambayo tunaisimamia, kipi ambacho kilipaswa kuja kwetu, kipi ambacho kimetumika na kwetu sisi tunasema ni faraja.

Tumekusanya milioni 500, tumetumia bilioni 4. Kwa maana kwamba kuna ziada inayotokana na *TCA* na matumizi yenyewe yanatokana na kulipa mishahara wafanyakazi waliopo, kununua mitambo na kufanya matengenezo, ndio matumizi yenyewe yalivyotumika. Sasa kama Hazina zimeingia fedha, hizo sisi hazituhusu na wala hatuzielewi moja kwa moja. Ni lazima wao wenyewe Hazina ndio watakaoweza kutoa ufafanuzi huo. Maana swali lako la msingi halikuulizia Hazina, liliulizia Mamlaka ya Uwanja wa Ndege pamoja na kile chombo kilichopo pale.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ningekushauri ungemuandikia Mhe. Waziri wa Fedha suala la msingi. Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo swali jengine la nyongeza.

Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa umahiri wake na upeo wake wa kufafanua majibu haya.

Mhe. Naibu Spika, hizi mamlaka nyingi zinazohusu Muungano, nakumbuka sheria yake ina wajumbe wa bodi kutoka Zanzibar. Nitatoa mifano michache, mmoja ni *TCRA* ilikuwa na wajumbe 2 wa bodi, Marehemu Dkt. Suleiman na Dkt. Lila, sasa hivi ninavyofahamu bodi ile imevunjwa haina mjumbe kutoka Zanzibar. Hata *TCAA* ilibahatika kuwa na mjumbe wa bodi ambaye yumo humu humu ndani ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi, ambaye sasa ni Naibu Waziri wetu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na mambo mengine yote mazuri kwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwa sheria hii hivi sasa, tuna wajumbe wangapi sisi Zanzibar katika mamlaka ya bodi hii na kifungu (b) katika kipato chote hiki kinachopatikana Zanzibar, ndege kutua

ndege kuruka na ndege kuegesha. Je, zile pesa zinabakia hapa hapa au zinapelekwa katika mfuko Mkuu wa Muungano. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna bodi ambazo zinahusiana na masuala ya Muungano, ambazo Wazanzibari ndio wanalazimika kuwa wajumbe. Ni kweli kwamba *TCRA* bodi yao imekwisha na Dkt. Lila alikuwa ni Makamu Mwenyekiti wa bodi ile ya *TCRA*. Kwa bahati nzuri kama wiki tatu Mhe. Waziri wa Sayansi na Ufundi Prof. Mnyaa aliweza kuwasiliana na wizara yetu na kutuambia kwamba wako mbioni kutaka kuirejesha bodi mpya ya *TCRA*. Alituthibitishia kwamba wajumbe wa Zanzibar watakuwepo. Tunaamini kwamba hata mwenyekiti anaweza kutoka Zanzibar katika bodi hii ya *TCRA*.

a) Katika *TCA* tumeweza kufanya mazungumzo mazuri na wenzetu wa Wizara ya Uchukuzi na katika msimamo huo huo Dkt. Harrison George Mwakyembe aliwathibitishia kwamba *TCA* ni mbombo cha Muungano na katika bodi yake lazima iwe na sura ya Muungano. Akasema kwamba wenyeviti wa *TCA* wamekaa muda mrefu upande wa Tanzania Bara, mara hii lazima mwenyekiti awe anatoka upande wa Zanzibar. Ni kweli, lililofanyika Mwenyekiti wa *TCA* anatoka upande wa Zanzibar na miongoni mwa wajumbe hao ni mfanyakazi wetu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

b) Mhe. Naibu Spika, ameulizia masuala ya mapato yanayotokana na ndege kutua, kuruka pamoja na maegesho. Mapato hayo yanagawika kwa mujibu wa taratibu husika.

Unapozungumzia suala la mapato yanayotokana na Anga, bila shaka mapato haya yatakwenda katika Hazina Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mgawanyo,kwamba hawa watachukua kiasi hiki na hawa watachukua kiasi hiki na mkusanyaji ambaye ni IATA, hazikusanywi na Jamhuri moja kwa moja. Ndege zinapita tunachukua takwimu za ndege zilizopita zinazotumia Anga mnapeleka IATA, ndio wanaokwenda kudai, wanakuleteeni fedha zenu mnafanya mgao kwa mujibu wa *ration* ambazo mmekubaliana. Kuna mapato mengine ambayo yanatokana na kuegeshwa kwa ndege ambayo ni mamlaka husika.

Kwa mfano, ndege itaegeshwa katika uwanja wetu wa ndege hapa Zanzibar, maana yake mapato yale ya kuegesha yataingia kwetu. Kwa hivyo, mgawanyo utakuwa ni wa kwetu kati yetu sisi na Hazina yetu, hayaendi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nam. 29

Kero ya Foleni Kwenye Vituo vya Kununulia Umeme

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Pamoja na Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) kupandisha bei ya umeme kwa wananchi wanyonge, bado kumekuwa na usumbufu mkubwa wa wananchi hao wanaokwenda kununuwa huduma hiyo katika vituo mbali mbali vya Shirika. Kumekuwa na kero ya foleni katika vituo hivyo vya kuuzia umeme hasa katika maeneo ya mjini.

a) Wizara inajua kuwa kero hii imelalamikiwa muda mrefu na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kuiondowa.

b) Ni sababu gani zinapelekea kituo cha kununulia umeme kilichopo Malindi, mara kwa mara kufungwa kabla ya wakati.

c) Ni lini vituo vya kununulia umeme vitaongezwa ili kuondosha kero na usumbufu kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 29 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli wizara yangu inajua kuwa wakati wa Magharibi foleni inakuwa kubwa na kuliondosha tatizo hilo wizara yangu kwa kupitia Shirika la Umeme imeingia mkataba na Zantel, ili kuweza kutoa huduma ya kununua umeme kupitia simu za mkononi.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu haina taarifa inayoelezea kituo cha kuuzia umeme Malindi kufungwa mara kwa mara kabla ya wakati. Hata hivyo, wizara yangu imetoa agizo kwa Shirika la Umeme kuhakikisha kwamba vituo vyote vinafungwa kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wizara yangu imo katika harakati za kuanzisha huduma ya kununua umeme kupitia simu za mkononi, imelazimika kusitisha kuongeza vituo katika maeneo ya mjini. Hata hivyo, hivi karibuni tumefungua kituo cha kuuzia umeme huko Makunduchi. Pia tumo katika mipango ya kufungua kituo huko Konde na Mtambile Pemba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo sana ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa nishati ya umeme ni nyenzo muhimu sana katika kupunguza umaskini na kujenga uchumi. Sababu gani zinazopelekea kupanda kwa gharama za umeme Zanzibar na serikali imechukua hatua gani kuwa katika chanzo chake cha umeme.

(b) Alisema Mhe. Naibu Waziri atasaini mkataba wa Zantel. Hebu atuambie tarehe ngapi mkataba huu utasainiwa, ili wananchi wapate kujua baada ya kilio chao cha kuteseka pamoja na pesa zao wanazokatwa pale kituo cha Michenzani na Malindi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kupanda kwa bei ya kuuzia umeme Zanzibar inatokana na bei tunayopandishiwa kutoka TANESCO na serikali tayari imejiandaa katika kutafuta wawekezaji ambao watawekeza sekta hii ya kuanzisha umeme hapa Zanzibar.

Suala la pili la kuhusiana na kufunga mkataba kwa Zantel. Tayari kama nilivyoeleza kwamba wizara yangu kwa kupitia Shirika la Umeme imefunga mkataba na Zantel kwa ajili ya kuanza shughuli rasmi za kuuzia umeme wananchi kupitia njia za simu. Kwa hivyo, muda bado tutautangaza pale tu ambapo tutakapomaliza. Aidha, makubaliano yetu tutatangaza na tutawafahamisha wananchi.

Mhe. Naibu Spika: Kazungumza tarehe gani mkataba mumetia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante Mhe. Naibu Spika, suala la tarehe nitamjibu Mhe. Mjumbe kwa kupitia njia ya maandhishi, kwa sababu sitaki nimpe majibu ya kubahatisha.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote kwanza nichukuwe nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika leo hapa kwa ajili mambo yetu mbali mbali ya kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa anajibu jibu mama alisema kwamba wizara yake haina taarifa kwamba kituo cha Malindi kinafungwa kabla ya wakati.

Sasa je, analithibitishia Baraza lako hili tukufu tokea siku alipolipata suala hili kwamba ameshindwa kwenda kuangalia kwamba kweli kituo hicho kinafungwa kila wakati, ndio analithibitishia Baraza hili kwamba kazi zake hazifanyi vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, baada ya kupata taarifa hii tumetoa agizo kwa Shirika la Umeme ihakikishe kwamba vituo vyote vinafunguliwa kwa wakati na kufungwa kwa wakati. Kwa hivyo, hiyo ni hatua moja ambayo tumeichukua.

Mhe. Asha Bakari Makame: Swali langu hajanijibu. Naomba alijibu swali kwa mujibu nilivyomuuliza. Sio aniambie linafunguliwa kwa wakati na linafungwa kwa wakati. Nilimuuliza analithibitishia Baraza lako tukufu kwamba tokea siku alipolipata swali hili hajajua kwamba kituo hicho kweli kinafunguliwa kwa wakati na kufungwa kwa wakati. Sasa asiniambie kwamba katoa agizo, yeye ndiye muhusika Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri labda nikufahamishe alivyokusudia Mhe. Mjumbe. Je, baada ya kupata hiyo taarifa ya tatizo hilo ulikwenda kukagua, ndio kakusudia hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nirejeshe majibu yangu kwa Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo.

Kwanza ninachotakiwa ni kuchukua hatua baada ya kupata taarifa. Kwa hivyo, hatua ya kwanza baada tu ya kupewa taarifa hii ni kupeleka agizo kupitia Shirika la Umeme. Vile vile kuhusu ufuatiliaji bado sijafuatilia, lakini nitafuatilia sio muda mrefu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwanza niwapongeze kwa hatua waliyosema wanataka kufungua kituo cha kuuzia umeme Mtambile. Lakini kwa sababu watu wa maeneo ya Mtambile na vitongoji vyake inawabidi kufuatilia ulipaji wa umeme Mkoani ambako ni mbali kidogo. Je, azma hii ya kufungua kituo Mtambile ni lini itatekelezwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Kama nilivyoeleza hapo awali kwamba tumo katika harakati ya kufungua kituo cha Mtambile. Kwa hivyo tumo kwenye maandalizi ya mwisho sasa hivi na kitakapokamilika tu basi tutatoa taarifa kumueleza Mhe. Mwakilishi, kwa sababu vile vile na yeye tunapenda tushirikiane katika ufunguzi huo. Kwa hivyo, tumo katika maandalizi ya mwisho yatakapokamilika tu, basi tutatoa tarehe rasmi ya kwenda kufungua kituo hicho.

Mhe. Naibu Spika, Ahsante Mhe. Naibu Waziri kwa majibu. Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwatambulishe tumepata ugeni leo katika Baraza letu. Kuna wanafunzi 40 kutoka Skuli ya Mwanakwerekwe E, nawaomba wasimame pamoja na walimu wao 6 karibuni sana. Kaeni.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2014/15 ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijawaita walioomba kuchangia huku. Juzi tulimalizia wachangiaji watano na leo nina wachangiaji sita na tunategemea jioni Mhe. Waziri tumwite ili afanye majumuisho na tupitishe vifungu. Kwa hivyo, naomba wale wenye nia ya kuchangia walete ili wapate nafasi. watakaochelewa tena itabidi wachangie kwa maandishi.

Kwa hivyo, namtaja Mhe. Mjumbe wa kwanza atakayeanza kuchangia hivi leo ni Mhe. Mohammed Haji Khalid, akifuatiwa na Mhe. Marina Joel Thomas na pia ajiandae Mhe. Salim Abdalla Hamad. Dakika 20.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, asubuhi hii kupata nafasi ya mwanzo kutoa mchango wangu mdogo kuhusu Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kabla ya mchango wangu ningeomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa wasaa asubuhi hii kusimama mbele ya ukumbi huu kutaka kutoa mawazo yangu.

Pia nikushukuru wewe kwa jinsi unavyotuongoza katika Baraza hili. Kadhalika nitowe pongezi maalum kwa waziri na watendaji wake wote katika ofisi yake, kwa jitihada wanazochukua kufanyakazi katika ofisi hii licha ya mazingira magumu sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianzie na Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Kwanza. Hapa nitaangalia namna ya maingizo ya fedha. Sitaki nitaje ni kiasi gani kilichoingizwa, lakini hadi kufikia mwezi wa Machi mwaka huu pesa walizoingiziwa ni kama asilimia 26 tu, kama huu ungekuwa ni mtihani basi wangepata F, wamefeli kwa ofisi hii.

Nyengine ni Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Hii nayo ingizo lake ni kama asilimia 27 tu ni F vile vile wamefeli, kwa sababu fedha walizoingiziwa hawawezi kufanya shughuli walizokusudia.

Idara ya Utumishi na Uendeshaji hawa ingizo lao kidogo wamepata asilimia 54 kama ungekuwa ni mtihani wangekuwa wamepata C, wamefauli kidogo.

Idara nyengine ni Idara ya Mazingira, nayo hii wamepata asilimia 44 ambayo kwa wakati huo nasimama mimi ilikuwa ni D, sijui leo ikoje. Lakini D ni *just simple pass* ni kupasi kidogo sana.

Mhe. Naibu Spika, idara nyengine ni ya watu wenye ulemavu. Hii pamoja na huduma zake za watu wenye ulemavu kuwa ni huduma maalum, bado ingizo lao lilikuwa ni asilimia 12 tu, ni F.

Taasisi yao nyengine ni Ofisi Kuu Pemba, ingizo lao ni asilimia 43 tu nayo hii kadhalika ni D. Mhe. Naibu Spika, nyengine ni Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya. Hii ingizo lao ni asilimia 25 ni F.

Mhe. Naibu Spika, nyengine ni Tume ya Ukimwi, ingizo lao ni asilimia 34 tena ni F, kwa ujumla Mhe. Naibu Spika, ukichukua wizara hii au ofisi hii na idara zake zote ujumla wake ilikuwa imefanya vibaya katika maingizo ya fedha, lakini watendaji wamejitahidi kufanya kazi zao kwa ufanisi ndio maana nikasema mwanzo kuwa wamefanya kazi ngumu katika mazingira magumu.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ofisi hii ipo idara ya mazingira; idara ambayo kwa mawazo yangu mimi ni miongoni mwa idara muhimu sana kwa sababu inashughulika na uatunzaji na uhifadhi wa mazingira, uharibifu na uchafuzi wa mazingira. Sasa kama idara hii na umuhimu wa aina hiyo ingizo lake ni dogo mno je, ni kweli Serikali imekusudia kiudhati kutunza mazingira, kuyahifadhi mazingira. Kwa hivyo nichukue msemo wa Mheshishimiwa Mshimba hapa bado Serikali haijakuwa serious kuhusu suala hili.

Mhe. Naibu Spika, nije katika makaazi kwenye nyumba ya Makamu wa kwanza wa Rais ningeomba Waziri anieleze kodi ya nyumba hizi ikoje, kwa sababu ni nyumba ya kukodi na hatujui Serikali inalipa kiasi gani na ikiwezekana na ile ya Mhe. Makamu wa pili ingawa haipo kwake lakini ni nyumba ya Serikali pia tuone zile gharama za anayekaa kwenye nyumba ya Serikali zikoje, na yule anayeishi katika nyumba nyengine gharama zake zikoje, ili tuone namna gani tunaweza kusaidia viongozi hawa wawili kuishi katika nyumba za bei nafuu kidogo.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi katika kipindi hiki cha miaka mine tuliyokuwa nayo tumeingia katika mfumo mpya wa uongozi, mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo imeshirikisha vyama vyote vyenye wawakilishi katika baraza navyo ni viwili tu; chama tawala CCM na CUF. Tunakwenda vizuri kwa mtazamo wangu mimi kama itakuwa ni sahihi au sio sahihi, tumekwenda kwa mashirikiano lakini pia kufanya tathmini ya miaka hii minne iliyopita nadhani kila mwaka tathmini Mhe. Naibu Spika, inafanyika kwa sababu kila mwaka huwa tunaadhimisha sherehe zetu za Mapinduzi. Nafikiri Serikali huwa inafanya tathmini pamoja na mambo mengine ya mambo yaliyofanyika kwa mwaka mzima uliopita.

Sasa kwa mchango wangu tathmini hiyo Serikali inayofanya na mara nyingi huwa Serikali inasema tuko katika hali nzuri tunatunza amani na utulivu wa nchi uliopo, sasa hoja tunayotaka kujenga sisi wajumbe hii si tathmini ya kuuliza watu ama mfumo huu wanautaka au laa, hii si tathmini ni jambo jengine mbali, lakini kwa kuwa tuna haki hiyo na ni haki ya kikatiba ni vyema wenye wazo hilo wakafanya hivyo. Lakini Mhe. Naibu Spika, kana kwamba haya matokeo mabaya yote yaliyotokea katika kipindi hiki kwenye Serikali hii ni kwa ajili ya huu Umoja wa Kitaifa uliopo, kutiwa watu tindikali, kuchomwa makanisa na mara nyengine maskani na matawi ya CCM yote yanaonekana ni matukio ya Umoja huu wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, nijiulize kabla ya hapo matokeo ya aina hii nchi hii yalikuya hayapo, kabla ya Serikali ya kitaifa, suala nitajibu mwenyewe yalikuwa yanatokea tena sana. Pemba kuna watu kadhaa bila ya hatia mwaka juzi waliuwawa, ilikuwa hakuna umoja wa kitaifa, Piki katika uchaguzi mmoja ulikuwa mwezi wa ramadhani watu walipigwa wakaporwa mali zao na wakanyanyaswa na kufedhehewa na wakaingiliwa mchana mwezi wa ramadhani, ilikuwa hakuna umoja wa kitaifa na haya yalitokeya.

Mtoni nyumba kadhaa zilivunjwa ilikuwa hakuna umoja wa kimataifa, kwa hivyo haya ni matukio ya kawaida Zanzibar, si kwa sababu ya Umoja wa Kitaifa ni matukio yanayoendelea kutokea kwa sababu mbali mbali, sio sababu ya Serikali ya Kitaifa, yaliyotokea nyuma ni mengi zaidi na magumu zaidi kuliko haya yanayoonekana sasa, Mhe. Naibu Spika, hii si hoja ya kweli.

Mhe. Naibu Spika, lakini kwa kuwa kila mtu ana mawazo yake kulingana na mwenyewe anavyoona yeye ni sawa lakini zamani watu walikuwa wenye mashamba walikuwa wanamuweka mtu kuja kuangalia lile shamba lake, na huyu alikuwa anaitwa nokoa na kawaida Mhe. Naibu Spika, Nokoa katika shamba huwa mkali zaidi kuliko yule

tajiri aliyemkabidhi shamba, kwa hivyo watu wenye mawazo ya aina hii ya kuona huu Umoja wetu ndio sababu ya mengi kutokea, hawa wana mawazo ya nokoa, kuona mwenye shamba hana nguvu kuliko yeye.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa wajumbe twendeni kwenye bajeti, kuna vifungu, kuna miradi mna kila kitu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Naibu Spika, ukichukua Tume ya Ukimwi kama nilivyoeleza kuwa ina asilimia 34 bajeti yake ni ndogo, sasa serikali pamoja na mipango yetu yote ya kukemea, ya kuelimisha, ya kuelekeza, kuondoka katika janga hili, lakini bado ile sehemu ya Serikali ya kuhudumia taasisi hii ni ndogo sana je, ni kweli Serikali ina nia ya kupiga vita jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, ofisi kuu Pemba ambayo inaongoza masuala yote ya Pemba fedha wanazoingiziwa ni ndogo ukilinganisha na hizi tume tu hii Wizara, lakini Ofisi kuu Pemba ambayo inafanya kazi zote wameingiziwa kama milioni 160 na kidogo tu hivi tena hawakupewa zote, hivi ni kweli serikali imekusudia kwa Ofisi hii kule Pemba ifanye kazi gani kwa vijisenti vichache wanavyowatilia? Je, haina lengo la kuwakwamisha hawa watendaji washindwe kufanya kazi zao?

Mhe. Naibu Spika ningeomba Wizara ya Fedha, Wizara na idara zote wazione kuwa ni za Serikali wala nyengine wasifanye kama mtoto wa kambo au mtoto wa kuleya, tena kapata mlezi ambaye hampendi. Ningeomba kwa kuwa pesa zinazoombwa sio nyingi zaidi kwa ofisi hii, vijipesa wanavyoomba ni kidogo sana sana na bado wanaingiziwa kidogo sana sana wangeiona kwamba Ofisi hii nayo ni Ofisi ya Serikali inahitaji kufanya kazi zake kwa ufanisi kama zinavyofanya Ofisi nyengine.

Mhe. Naibu Spika, nirudi pale nilipoanza habari ya mazingira; wizara imesimamia kupiga vita mifuko ya plastiki, na niseme kwa asilimia zaidi ya 90 kwa zoezi hili wamefanikiwa. Lakini kuna masuala mengine Mhe. Naibu Spika, ambayo ni muhimu nayo kushughulikiwa kama uchimbaji wa mchanga ovyo. Uchimbaji kule kwetu wa matofali, sasa masuala haya kwa upande mmoja yanaharibu mazingira, kwa upande mwengine ni vyanzo vya ujenzi na mpaka sasa hatujakuwa na vyanzo mbadala vya ujenzi, maana ama tutumie miti au tutumie matofali. Matofali yapo ya aina mbili; yanayotokana na saruji na yanayotokana na kifusi kule Pemba. Lakini kwa Pemba yale ya kifusi kidogo ni rahisi na ndio maana tukawa tunatumia kwa wingi ingawaje tunaharibu mazingira.

Je, Wizara au Serikali ina mpango gani mbadala ambao itatuwezesha kuweza kutafuta makaazi yaani kujenga nyumba bila ya kuchangia na kuharibu mazingira. Huu ni uharibifu wa kibinaadamu, lakini upo wa kimaumbile kama maji chumvi, maeneo kadhaa tu yamekumbwa na maji chumvi, mara nyengine yanatokea majanga ya moto. Mimi katika jimbo langu imetokea hata Mhe. Makamu wa Pili ilibidi aje kukagua na aliagiza kuwa pajengwe tuta la kuzuiya yale maji chumvi kiasi cha miaka miwili iliyopita nyuma. Lakini bado hatua hiyo haijachukuliwa wala sijapata habari yoyote kwamba angalau kuna hatua itakayochukuliwa kuhusu lile agizo la Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, Wapemba ni watu na ni waungwana sana tofauti na vile vinavyoonekana kwamba si watu wala sio waungwana, ni watu na ni waungwana miongoni mwa waungwana wa dunia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Naibu Spika, kwanza nilikuwa naomba nizungumze suala la matukio mbali mbali ambayo yametokea na Mheshimiwa Mohammed alisema suala hilo kabla ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa yametokea matukio mengi, lakini kwa muono wangu ningetegemea Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeundwa na nilitegemea matukio hayo yasingetokea tena. Hata hivyo yameendelea kutokeya kwa hivyo kubwa tumuombe Mwenyezi Mungu matukio hayo yasitokee tena na hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa isiwe ni mwendelezo wa matukio hayo. Sisi tulitegemea Serikali ya Umoja wa Kitaifa itazidisha amani, mshikamano lakini Mhe. Naibu Spika, kumbe kinyume na tulivyotegemea.

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda katika suala la Mheshimiwa Mohammed alisema suala la Upemba kwa kweli lugha kama hizo hazipendezi za kiubaguzi hazipendezi kabisa. Wazanzibari sote ni wamoja na hii naona inashamiri siku hadi siku. Wapemba na Unguja ni kitu kimoja, kwa hivyo kila matu akisimama hapa wapemba hivi, wapemba hivi inakuwa si vizuri kwa kweli naomba tusiendeleze lugha hizi ni za kibaguzi, haipendezi.

Nitakwenda katika hotuba na nitazungumzia suala zima la Idara ya watu walemavu Mhe. Naibu Spika, katika taarifa yake Mheshimiwa Waziri alieleza kama mambo matatu ambayo; la kwanza kutengeneza mfumo wa takwimu, *data base* za watu wenye ulemavu na cha pili mfumo huu wa kutengeneza *data base* Mhe. Naibu Spika, ni mfumo mzuri ambao utasaidia kujua hali halisi ya watu wenye ulemavu wanaoishi hapa Zanzibar. Pia mfumo huu utasaidia kujua mahitaji yao muhimu na utasaidia kupanga mipango ya maendeleo bora kwa watu wenye ulemavu.

Sasa nakwenda kwenye madawa ya kulevya, Mhe. Naibu Spika, madawa ya kulevya ni tatizo kubwa hapa Zanzibar na hata duniani pengine, hapa katika kitabu cha bajeti cha Mhe. Waziri *page* ya nane walisema kuna mpango wa kujenga kituo cha tiba cha marekebisho ya tabia kwa watumiaji wa madawa ya kulevya na hatua iliyofikia sasa hivi katueleza Mhe. Waziri. Katika eneo la Kidimni wameshazungusha uzio kwa ajili ya kuhifadhi eneo hilo, lakini Mhe. Naibu Spika, kujenga vituo kama hivi na hasa ukiangalia sasa hivi kuna *sober houses* nyingi tu katika shehiya mbali mbali, *solution* sio kujenga vituo vya kurekebisha tabia.

Mhe. Naibu Spika, kutatua tatizo ni kudhibiti huu uingiaji wa madawa ya kulevya, tukizuia uingiaji wa madawa ya kulevya Mhe. Naibu Spika, hata vituo hivyo hatutojenga namna hiyo na vituo hivi mimi nahisi baadae vitakuwa mzigo kwa Serikali. Kwa sababu vitajengwa vituo watawekwa watu, watu wanataka huduma; wanataka wapatiwe nyenzo ambazo pengine akitoka katika sehemu ile waweze kujitegemea. Baadae itakuwa mzigo kwa sababu madawa ya kulevya yatakuwa yanaingia na watu watakuwa wanatumia na mtu akishaona mtoto katika nyumba yake ameshamshinda pengine anamuibia atampeleka katika kituo hiki. Kwa hivyo Serikali baadae itakuwa na mzigo mkubwa ambao pengine kwa baadae utakuwa ni mzigo ambao watashindwa kuhudumia serikali.

Mhe. Naibu Spika kubwa hapa ninavyoshauri serikali ifanye kila njia idhibiti uingizaji huu wa madawa ya kulevya na hasa katika maeneo ya *Airport* na maeneo ya Bandarini. Bandarini ukipita sasa hivi mizigo yote inapekuliwa kwa mikono tu, mtu begi lake anafunguliwa, hivi kweli utajua kila kitu kilichomo ndani ya begi lile?

Tuimarishe japo mashine ya *scanner* ambayo pengine inaweza ikajua kama katika mzigo huu labda kuna kitu hiki na hiki na kwa kuimarisha pia ulinzi mimi naamini serikali ikiamua kama madawa ya kulevya yasiingie naona inaweza. Kwa sababu serikali ina taasisi nyingi ambazo zinaweza zikasimamia, ina vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo imara. Kwa hiyo ni kuweka mikakati madhubuti ili kuudhibiti huu uingiaji wa madawa ya kulevya, hiyo ndio nahisi itakuwa *solution*.

Mhe. Naibu Spika, tukiacha iendelee watu wanaendelea kuingiza madawa huku tunajenga vituo vya kurekebisha tabia baadae nahisi serikali itakuwa na mzigo mkubwa ambao utakuwa ni tatizo kwa siku za baadae. Pengine katika vijana hawa wakiwekwa katika vituo vya kurekebisha tabia pengine hudumu hawatopata, ina maana wanaweza wakageuka hata wakawa wanaingia mitaani wanafanya matukio ambayo si mazuri. Kwa hiyo, nahisi ingejikita hasa katika udhibiti wa uingiaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda katika masuala ya Tume ya UKIMWI. Katika kitabu chake Mhe. Waziri alitueleza hapa takwimu **ambapo skuli mbali mbali walizitembelea na kuzipatia elimu kuhusu** maambukizi ya UKIMWI kwenye madawa ya kulevya, labda nimuulize tu katika kutoa mafunzo hayo vipi waliwahamasisha wanafunzi hao kupima maambukizi ya Virusi vya UKIMWI? Wamewapima na kama wamewapima wamepata matokeo gani?

Nije katika suala zima la mabadiliko ya tabianchi, mazingira. Suala la mazingira sasa hivi kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira na kuna suala zima la mabadiliko ya tabianchi katika upande wa baharini hapa, kubwa nilikuwa na ushauri kwa Mhe. Waziri, wazidi kuweka mikakati iliyo bora ili uchafuzi huu usiendelee.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono asilimia mia moja.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii fupi ya kuchangia chochote katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, hotuba ya Bajeti ya mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa majukumu mazito aliyonayo katika wizara yake inayowalenga wananchi kwa jumla. Walemavu, waathirika wa virusi vya UKIMWI, mazingira, madawa ya kulevya ni mambo mazito na nashukuru kwa juhudi ya kazi anayofanya katika kutekeleza wajibu wake.

Pili, nashukuru kakisoma vizuri kitabu chake tumekifahamu na kwa sababu nimekifahamu vizuri mimi leo nitachangia kwa kutaka ufafanuzi zaidi tu, katika baadhi ya mambo ambayo nimeyaona kwa mimi binafsi yanahitaji maelezo zaidi. Kwa sababu hii nianze na kifungu nambari saba (7) kilichopo kwenye ukurasa wa pili na watatu wa kitabu hiki na kifungu hiki kinahusika na malengo makuu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Katika kifungu hiki Mheshimiwa ningeomba kupewa maelezo kuhusiana na kifungu cha 7(4), yaani hii wizara kwa maana ya wizara kutokana na kuwa tabianchi ni tatizo ambalo ni kubwa sana, na hili linatokana na harakati za binaadamu katika nchi mbali mbali na hata zilizoendelea. Kutokana na harakati hizo za kimaisha dunia yetu inaingiliwa na mambo ambayo hayahitajiki na yanasababisha uchafuzi wa mazingira, na pia yana sababu kuongezeka kwa joto, mabarafu kuyayuka na matokeo ni kima cha maji kuongezeka.

Haya ni mambo makubwa sana yanafanywa nje ya Zanzibar, yanafanywa nje ya Tanzania. Pamoja na kuwa Tanzania yapo, lakini si kwa kiwango kikubwa sana kiasi hicho. Kwa hivyo, ningeliomba kujua ni kwa namna gani hasa kutokana na hali hii ilivyo ambayo haimo katika mikono yetu, wizara inasimamia mabadiliko haya ya tabianchi, yaani wizara inasimamia vipi hasa kwa sababu mambo haya yanatokea mbali au yanatuathiri tu. Ningeliomba kujua namna gani wizara inasimamia mabadiliko haya.

Hii ni kwa sababu nasikia nchi za dunia ya kwanza katika kutekeleza mambo yake ya kimaisha na kusababisha huu uharibifu wa mazingira. Mambo haya yanaitwa tabianchi huwa zinatoa fidia kwa zile nchi zilizoathirika hasa nchi masikini. Kama hilo ni kweli ningeliomba kujua na Zanzibar nayo ikiwa ni moja kati ya nchi zinazoathirika, inapata au imeshapata msaada wa kiasi gani na msaada huo umetumika vipi kama ni kweli.

Halafu kifungu cha 7(2) ukurasa wa tatu (3) hapa imeeleza kuwa wizara hii moja katika kazi zake ni kuratibu na kuthibiti usafirishaji, uingizwaji, matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya. Inadhibiti usafirishaji na uingizaji matumizi na biashara haramu za dawa za kulevya. Sasa mimi kutokana na hili la madawa ya kulevya athari yake ilivyo kubwa na hata Zanzibar kuzungumzwa kuwa ni njia ya kupitisha madawa haya ya kulevya. Mimi nafikiri suala la uingizaji katika udhibiti lingelikuwa la mwanzo halafu tena kukawa na usafirishaji.

Kwa sababu hatuwezi kudhibiti usafirishaji kama kitu hakijaingia na kwa hivyo ili suala hili liondoke kwanza tungehakikisha kuwa tunaendelea na kuimarisha udhibiti huu wa uingizaji wa madawa ya kulevya, halafu ndio tena tuendelee na usafirishaji. Lakini tukianzia usafirishaji mwanzo ni kama hiki kitu tayari kipo na ni cha kawaida.

Mhe. Naibu Spika, tukiendelea kuna mradi huu wa ujenzi wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya, mradi ambao utajengwa Kidimni au ushaanza shughuli zake za ujenzi kwenye eneo la Kidimni. Taarifa hii iko katika kifungu cha 21 ukurasa wa 8 wa kitabu hiki. Mimi kwanza tofauti na wenzangu, kwa sababu hili suala ni janga pamoja na kuwa nashukuru hatua ya kuridhisha imefikiwa japo kuwa mambo ya madawa ya kulevya yangalipo, lakini si kama ilivyokuwa mwanzo. Hatua imeonekana, mimi nipongeze kwa kujengwa au kwa serikali kuwa na azma ya kujenga jengo hili. Lakini nina masuala naomba nipate majibu.

Kwanza, mradi huu kwa mujibu wa maelezo kuwa utatekelezwa kwa fedha ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tu, ni kwa nini haukuombewa msaada wa fedha kutoka nje kama ikiwezekana kutokana na kuwa hali yetu ya kiuchumi ni ndogo sana, huenda mradi huu ukachukuwa muda mrefu sana kwa kutegemea serikali peke yake?

Pili, mradi huu unatakiwa kutumia kiasi gani cha fedha mpaka kukamilika, kuanzia huu uzio unaojengwa mpaka kukamilika kwake? Pili kunatarajiwa kumalizika lini kutokana na umuhimu wake na huu ujenzi wa uzio ambao umeshaanza kujengwa ili kuzuia hili eneo lisivamiwe, umeshafikia hatua gani? Umeshatumia kiasi gani na kumalizika kwa uzio tu binafsi kutahitajika fedha kiasi gani?

Wizara imeeleza kuwa kabla ya kuanza kwa kazi hiyo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilifanya hatua zote za kuratibu za manunuzi kama sheria inavyoeleza. Ningeliomba kujua ni hatua zipi na ni manunuzi ya kitu gani?

Halafu (b) katika ujenzi wa hii nyumba naamini itagharimu fedha nyingi sana, ni utaratibu gani uliofanywa wa kihalali kama kwenye manunuzi, ili kusiwe na hoja huko usoni?

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye Idara ya Mazingira. Kwa mujibu wa maelezo ni kuwa idara hii ambayo inafanya kazi naomba nipewe maelezo, naomba kueleweshwa kutokana na uperesheni 115 zilizofanywa 75 kisiwani Unguja

na 40 Kisiwani Pemba za Mifuko ya Plastiki kwa ajili ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira, ambapo jumla ya watu 18 Unguja na 15 Pemba walikamatwa na kulipa faini ya jumla ya shilingi 3,290,000/=.

Sasa masuala yangu hapa ni hivi, kwanza hii Mifuko ya Plastiki binafsi kuangamizwa kwake inaweza ikaharibu mazingira, nilitaka kujua iliangamizwa katika hali gani ambayo haichafui mazingira?

Vile vile katika hii faini ya Shilingi 3,290,000/= zilizopatikana, Pemba ililipwa faini ya kiasi gani na Unguja ililipwa faini ya kiasi gani? Katika jumla ya kilo hizi za mifuko ambazo ziliteketezwa, ni kilo ngapi kutoka Pemba na kilo ngapi kutoka Kisiwa cha Unguja?

Mhe. Naibu Spika, tukifungua ukurasa wa 50 kuna kiambatanisho hapa nambari 4 ambacho kiambatanisho hiki kinahusiana na haya mambo ya uchafuzi wa mazingira. Katika kiambatanisho hiki kuna *column* kubwa juu iliyoeleza idadi ya operesheni halafu waliokamatwa na mchanga. Sasa waliokamatwa na mchanga imegawiwa sehemu 3; kuna gari, ng'ombe na kuna msumeno. Ningeliomba msumeno usiingie katika *column* kubwa ya watu waliokamatwa na mchanga. Kwa sababu naamini msumeno unahusiana na uharibifu wa mazingira kwa ukataji wa miti ovyo, huo ni ushauri wangu.

Halafu jambo jengine hapa pana gari 11 zinajulikana kuwa gari hizi zilikamatwa na mchanga, lakini ng'ombe je, alikuwa akipakiwa kama punda au zilikusudiwa kuwa ni gari za ng'ombe. Vile vile naomba maelezo ili kitabu hiki kikae vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, tukitoka hapo tunakwenda katika kifungu cha 38 ambacho kiko katika ukurasa wa 16 na katika kifungu hiki kimeelezwa kwamba, jumla ya miradi 20 imefanyiwa ufuatiliaji na kutolewa ushauri wa kimazingira na katika miradi hiyo 20, miradi 17 imetowa vyeti vya tathmini ya athari za mazingira na hivyo kutakiwa kuanza kazi ya utekezaji. Hapa kidogo naomba nipewe maelezo kwa kweli utekezaji au ilikusudiwa utekelezaji. Halafu huwo ushauri uliotolewa ni upi? na ikiwezekana hiyo miradi ishirini (20) ni ipi? naomba kupewa maelezo.

Jengine Mheshimiwa Naibu Spika tutaendelea na Tume ya kuratibu na kudhibiti dawa za kulevya, maelezo ni kuwa kutokana na juhudi zinazohusiana na mapambano zidi ya dawa za kulevya pamoja na mashirikiano kutoka kwa Raia wema ambazo zinaendelea jumla ya watu ishirini na tatu (23), ishirini na mbili wanaume (22) na mmoja (1) mwanamke wamekamatwa kwa makosa ya dawa za kulevya, na hivi sasa kesi zilizoko mahakamani kati ya watu ishirini na tatu ni kesi 21, ningeliomba kuelewa waliokamatwa na makosa kama taarifa ilivyoeleza ni 23, hawa tayari walikwishakamatwa na makosa ya dawa ya kulevya. Hizi kesi mbili (2) ni kwa sababu zimeshahukumiwa zikabakia 21 au hawa wawili (2) walisameheka baadae.

Halafu (b), hivi sasa kuna upelelezi unaendelea; upelelezi huu ni kwa hizi kesi zilizoko mahakamani au ni upelelezi wa mambo mengine kwa sababu hawa tayari kwa mujibu wa maelezo wameshakamatwa na madawa ya kulevya, halafu hapa kaandika kuwa juhudi za taasisi zinazohusika, sasa taasisi hizi zinazohusika ni ngapi? Na kama ikiwezekana kwa kuweza kuelewa ni zipi ili tuzipongeze, yaani taasisi zinazohusikana na dawa za kulevya.

Halafu kutokana na dawa za kulevya zilivyo naamini Wizara inakumbwa na changamoto nyingi sana. Haya madawa yanaingizwa na watu wanajuwa kazi yao, ni lazima kuna mtandao kama tulivyoona katika semina kadhaa. Naamini wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, ningeliomba kujua Mheshimiwa Waziri anatushauri nini kuhusu kuangamiza kabisa tabia hii ya kuingiza na kusafirisha na kutumia madawa ya kulevya katika visiwa hivi vya Zanzibar.

Jengine Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuelewa hizi kesi za watu hawa 21 waliokamatwa na madawa ya kulevya zishachukuwa muda gani mpaka hii leo. Kwa sababu katika uzoefu wangu huoni kuwa kesi hizi huchukua muda mrefu sana halafu nyengine hupotea ovyo.

Jengine Mheshimiwa Naibu Spika nizungumze habari ya UKIMWI. Hii iko katika kifungu cha 76 ukurasa wa 28 na maelezo kwa ufupi ni kuwa upatikanaji wa huduma za ukimwi kwa makundi maalum umeongezeka. Vile vile huduma za elimu ya ukimwi na ushauri nasaha na upimaji wa virusi vya ukimwi na usambazaji wa kondom na rufaa umeongezeka.

Sasa Mheshimiwa mimi ningeliomba kujua hii taarifa imeletwa wakati UKIMWI upo katika nchi lakini kuongezeka kwa mambo haya ni kwa sababu UKIMWI umeongezeka na ukiwa umeongezeka kwa kiasi gani? Mpaka ikiwa mafunzo, ushauri nasaha, upimaji nakadhalika ukaengezeka. Nasema hivyo kwa sababu hili ni suala la kutisha sana, halafu kwa mujibu wa taarifa jumla ya kondom 5192 zimesambazwa katika sehemu mbali mbali na katika hizi 5192 ikiwa ni asilimia 99.1 ni za kiume na 42 tu ikiwa ni asilimia 0.81 ni za kike. Kwa sababu takwimu za kule nyuma tulizokuwa tukiziona ni kwamba wanawake walikuwa wanaathirika kwa wingi zaidi kuliko wanaume. Sasa kwa nini kukatolewa kondom zote hizi 5192 kwa wanaume na 42 tu kwa wanawake, ni kwa vigezo gani wizara iliona katika kuongezeka kwa ugonjwa huo wa UKIMWI.

Halafu makundi hayo maalum yaliyopewa mafunzo na kadhalika ni makundi ya aina gani? Naomba vile vile nielezwe.

Pia Mhe. Naibu Spika, ni kwamba unajua suala la ukimwi ni suala gumu sana, na Serikali inatumia fedha nyingi kwa kutafuta dawa za kurefusha maisha. Mimi ninaloomba kueleza ni kuwa katika nchi hii hali halisi ilivyo tunaishuhudia ina kila sababu, kwa sababu ya watu kuingia wanavyotaka na kimazingira kuvaa wanavyotaka, na kutembea wanavyotaka na kufanya wanavyotaka. Hivyo kuna sababu ya kuongezeka kwa matatizo haya na akipata mmoja anamuambukiza mwenzake. Ningeliomba kwa sababu ni suala baya sana na ni zito, na ni maradhi ambayo hayana tiba, Serikali hasa kwa kupitia wizara husika ina msimamo gani wa kimazingira kutokana na huu uhuru uliotolewa ili tuone kuwa hali inabadilika ya kudhibiti ukimwi na maradhi haya yaweze kutuepuka. Ni maradhi mabaya sana kweli kweli.

Kingine Mhe. Naibu Spika, nizungumzie kuhusu Idara ya Walemavu, Idara ya Walemavu kwa taarifa kwa bahati mbaya haikupewa maelezo marefu, na walemavu tunao wengi sana, walemavu ni wananchi wenzetu Mwenyezi Mungu kawajaalia alivyowajaalia. Kuna walemavu wa aina kadhaa na walemavu wanahitaji mahitaji maalum. Nashukuru kwa mpango wa Serikali lakini kwenye kitabu haikuelezwa hasa ni hatua gani zinachukuliwa kuwashughulikia walemavu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba katika kutoa majumuisho anieleze kwa urefu na kifungu cha 92 kiko ukurasa wa 36.

Halafu (b) kuna malalamiko kwa walemavu walioko Pemba; kwanza wako katika mazingira magumu, hawana ofisi yao maalum, nafikiri haijawa tayari wanakodi tu, wanatafuta misaada ya kujenga ofisi yao. Lakini kuna kasma ambayo inatolewa kwa Idara ya Walemavu, masikitiko yaliyoko ni kwamba walemavu walioko Pemba kama wanapewa fedha wanazopewa ni ndogo sana. Na suala hili naamini Mhe. Waziri limeshamfika tokea mwanzo, na kabla ya kupitisha bajeti hii alikuwa analielewa. Kwa hiyo, mimi kutokana na umuhimu wao wa kimaumbile na mahitaji ya walemavu ningeliomba Mhe. Waziri amejipanga vipi kuona kuwa na walemavu walioko Pemba wanaangaliwa na kupatiwa msaada ili waone kuwa Serikali yao inawatambua na kuwathamini.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, nimsifu Mhe. Waziri kwa ufuatiliaji wa shughuli za mazingira na ninaelewa katika nchi hii Serikali kwa kupitia wizara yake imechukua juhudi kubwa sana. Serikali inajua kuwa visiwa vyetu vinaathirika, maji yanaongezeka, sehemu za kilimo zinaathirika kwa maji ya chumvi. Serikali imetumia fedha nyingi kwa kujenga matuta katika sehemu kadhaa ili wananchi waweze kujiendeshea maisha yao. Lakini pamoja na juhudi yote anayoifanya kwa makusudi Mhe. Waziri alikuja katika jimbo langu na kutembelea kisiwa cha Mtambwe Mkuu; ni kisiwa chenye historia ndiyo kikaitwa Mtambwe Mkuu na ni kisiwa ambacho Mwenyezi Mungu amekijaalia ni kisiwa ambacho ardhi yake ni ya mchanga, na alikitembea chote kwa miguu na akaona ni namna gani hali ya maji yanavyoongezeka na kisiwa kile kinavyoathirika kwa miporomoko.

Ile hali Mheshimiwa aliiona na alitoa nasaha nzuri sana ya kupanda miti na kadhalika ili hali isiendelee, lakini ndiyo inaendelea mti unaupanda mpaka ukiota lakini hali inaendelea. Na aliiona ile hali kiserikali tu haiwezi ikatekelezeka mpaka kuwe na misaada maalum, na kile ni kisiwa cha historia. Hivyo, ningeliomba Mhe. Waziri anipe maelezo tokea siku ile aliyokuja na mimi nashukuru kwa kufanya ziara maalum kuja kuona baada ya kuitwa na wananchi na kuiona hali ilivyo, mpaka hii leo amechukua hatua gani ya kuona kuwa alau tunakihami kile kisiwa kutokana na mmong'onyoko wa kasi kubwa unaondelea kwa sababu ya kuongezeka kwa kima cha maji.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa dhati asubuhi ya leo kunipa fursa kuweza kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika mwaka wa fedha 2014.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nianze kwa masikitiko sana namna ya utekelezaji wa kazi katika ofisi hii, kwa sababu mengi ya mambo ya Idara hii Mhe. Naibu Spika kila ukiangalia ukweli na udhati wake hakuna ambalo limeweza kufikia asilimia nzuri katika utekelezaji wake wa kazi. Na niseme kwamba nakuwa napata tabu sana kutaka kujua nini tatizo, kwa sababu nikimuangalia Waziri mwenyewe dada yangu Fatma Abdulhabib Fereji unamuona kwamba ni mtu ambaye anapenda kusimamia kazi zake. Ni mtu mkweli na muadilifu, mpole sana, alhajat, mwanamke ambaye amepewa tunzo ya ujasiri, sasa sifa zote hizo ambazo alizokuwa nazo lakini napata tabu kuona sifa nzuri anazo, lakini utekelezaji katika taasisi yake hauko vizuri.

Leo nilikuwa nataka nimuombe Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kutokana na sifa nzuri alizokuwa nazo, na nina imani ambayo ninaitegemea sana na ninaamini kwamba kauli yangu atakubaliana nayo, hebu atumie ujasiri aliotunukiwa kujiuzulu nafasi hii kwa kutokutenda mazuri katika kipindi cha mwaka uliopita. Nina imani kwamba hatolikataa hilo kwa sababu ya ukweli wake na ushupavu wake na ujasiri aliokuwa nao. Kwa nini niseme hivyo Mhe. Naibu Spika?

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka nizungumzie suala la walemavu hili atanisaidia kidogo, nataka kujua yeye na Wizara ya Afya wanashirikiana vipi katika kuona kwamba haki au fursa za walemavu wa viungo kuweza kupata viungo bandia angalau kuweza kujisaidia katika shughuli zao za kijamii. Hili ni tatizo kwa kweli zamani sisi tulikuwa tunatishika sana tukiona mtu hana mguu wala mkono, lakini sasa hivi imekuwa ni kawaida mtu kumuona ule ulemavu wake. Sasa nataka kujua hilo wizara yake inashirikiana vipi na hiyo Wizara ya Afya.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia wenzangu wengi sana wamelizungumzia ni suala zima la madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, nilisema kwamba wizara hii sioni ambalo wanalifanya kwa sababu baada ya kuona hii hali sisi tukatarajia kwamba haya matatizo yaondoke, lakini siku hadi siku unaona matatizo yanaongezeka na inafikia mahala mpaka tunapata aibu ambazo hatuzitegemei. Uwanja wa Ndege kama wetu, uwanja wa ndege una vifaa vya *security;* kwamba kilo 50, ambalo ni polo zima lina madawa ya kulevya liweze kupita mpaka lifikie katika hatua ya mwisho ya kutaka kusafiri. Sasa huwa najiuliza haya mashirikiano hizi taaluma zimetoka wapi?

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kijitabu chao hiki cha wizara kubwa ambalo naliona ni suala zima la masomo, tumetoa taaluma skuli, tumetoa *brochure,* tumefanya hivi kwenye magazeti. Mimi nafikiri kama hii wizara imeshindwa kazi basi hebu haya mambo tuhamishie Wizara ya Elimu waende wakasomeshe ili vijana wetu wanapokuwa *matured,* basi waone kwamba hizi athari za haya mambo tayari wameshasoma tangu maskulini na tuondoshe katika hii Wizara ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, suala la madawa ya kulevya limekuwa ni tishio sana, na mimi napata tabu kwamba haya mashirikiano yako wapi Mhe. Naibu Spika? Mhe. Naibu Spika, kama sikosei kitengo cha madawa ya kulevya kina gari moja tu la Nissan lile; ukiliona hilo gari lenyewe hata kufukuza gari la punda haliwezi. Sasa utawezaje kupambana na vitu kama hivyo wakati wewe mwenyewe nyezo huna, hilo la kwanza.

Lakini kitengo chenyewe Mhe. Naibu Spika, cha kupambana na madawa ya kulevya kuna tatizo ambalo linanipa tabu. Mheshimiwa kitengo hiki askari wake wanakaa kwa muda mrefu wanazoeleka, akipita mitaani tu anajulikana huyo anakuja kukamata madawa ya kulevya. Sasa kunakuwa kuna tatizo katika suala zima la kupambana na vitu vya wahalifu ambao wanakuwa wana fedha nyingi, halafu watu wenyewe unawaweka kwa muda mrefu na watu wenyewe vipato vyao duni, sitegemei kama tutafanikiwa hata siku moja. Askari wameshazoeleka hivyo watakula hela na kazi zitakuwa kila siku tunapiga kelele madawa ya kulevya hayaondoki, Mhe. Naibu Spika watu watapitisha vipolo mpaka magunia uwanja wa ndege, na majumbani watauza mpaka wachoke, kwa sababu bado hatujajipanga kupambana na suala la madawa ya kulevya.

Mhe. Waziri atakapokuja labda atakuja kunieleza mikakati na njia, lakini sioni zaidi ya kwamba tunatoa taaluma, na nimesema taaluma kama imefika pahala bora tupeleke maskulini waanze vijana tangu wadogo waanze kuelewa athari za madawa ya kulevya, na tuondoshe kutoa taaluma katika wizara hii Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, maeneo ambayo pia nasema kwamba bado yana mapungufu na ambayo yamenifanya leo niendelee kumng'ang'ania dada yangu atumie ujasiri wa kujiuzulu katika suala zima la uharibifu wa mazingira.

Mhe. Naibu Spika, mpaka jana nashuhudia gari la mchanga saa 2:00 za usiku linapita kituoni wakati suala la kusafirisha maliasili mwisho ni saa 12:00 kisheria. Sasa najiuliza hizi kazi zinafanywa vipi?

Mhe. Naibu Spika, mimi bado napata tabu na nasema kwamba hatufikii pahala tukapata ufumbuzi, uchimbaji wa mchanga umekuwa mwingi, umekuwa wa holela, maguzo ya umeme yananing'inia maeneo ya Mwanakwerekwe na maeneo mengine, magari ya punda yamekuwa tatizo, ukija ukisema au ukija kuambiwa unaambiwa aah wenye magari ya punda wanatembea na mapanga watu wanashindwa kuwazuia. Ah! Sisi Serikali, Serikali inashindwa kujipanga vipi kuwazuia wafuga punda katika suala zima la uchimbaji wa michanga katika maeneo mbali mbali.
Mhe. Naibu Spika, nasema mikakati nataka kuja kuisikia ili kuweza kuipitisha bajeti hii kuiongezea fedha ili iweze kufanya kazi zake, vyenginevyo Mhe. Naibu Spika mimi leo nitakuwa mkaidi sana katika wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala zima la mifuko ya plastiki. Dada yangu kama atakubali mimi tutoke leo saa 7 baada ya kumaliza Baraza twende sokoni Mwanakwerekwe akaone namna ya mifuko ya plastiki inavyotumika kwa wafanyabiashara kwa kuwatilia biashara wateja wao. Sasa mara nyingi tunakuwa tuna vigezo kwamba tumejitahidi na tumefikia pazuri, mifuko imepungua, hatutaki kupungua tunataka itoweke kabisa, suala la kupungua Mhe. Naibu Spika ni suala ambalo kwa kweli mimi huwa sikubaliani nalo, lazima hiki kitu kitoweke. Na kama atakubaliana na mimi tuondoke mchana twende tukaone wafanyabiashara namna wanavyotumia mifuko ya plastiki, kweupee!

Sasa hubaki najiuliza Mhe. Naibu Spika hii kazi inafanywa saa ngapi, tunafanya kazi gani Mhe. Naibu Spika? Ndiyo maana nasema bado Mhe. Naibu Spika mimi kila nikiangalia taasisi za idara hii hakuna pahala nimehisi kwamba tumepata mafanikio na matatizo yameondoka, najua jibu lake kubwa ataweza kuniambia ah tumejitahidi, majibu ambayo tumeyazoea na tutajitahidi ili kuondosha.

Mhe. Naibu Spika, sitozungumza sana lakini nitazungumza katika maeneo mafupi sana ambayo nategemea Mhe. Waziri atakuja kuniridhisha niridhike.

Nataka niende katika ukurasa wa 4 Ofisi ya Faragha kwenye kifungu namba 11 msaada wa kifedha kwa vikundi 25, madrasa na misikiti 13, wananchi 62. Mheshimiwa nimejaribu kuangalia katika kitabu chake hiki sijapata kuona kiambatanisho ambacho kimefafanua kama shehia ambazo zimeweza kusaidiwa au maeneo ya misikiti iliyosaidiwa. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa anambie hao wananchi 62 wametiwa katika shehia gani na shehia gani, hizi madrasa na misikiti imetiwa katika shehia gani?

Mhe. Naibu Spika, baada ya kukiangalia kitabu na kutoa michango yangu hilo la mwisho ambalo nataka nilizungumzie ili niweze kuingia katika kitabu cha bajeti ni suala ambalo nilikuwa nalipigia kelele kwa muda mrefu, nimeanza kwenye Bunge la Katiba nimekuja hapa nikamwambia Makamu wa Pili wa Rais na leo ninaiambia Wizara hii. Nielezwe sababu za msingi za kumuhamisha Makamu wa Kwanza wa Rais katika nyumba ya Bosnia; nyumba ambayo ni ya Serikali na kwenda kumuweka katika nyumba ya uraiani.

Mhe. Naibu Spika, nasema bado Waziri hatutendei haki, waziri wetu kwenda kumuweka kichochoroni mahala ambapo hapana usalama wa kutosha, aniambie dunia gani mawaziri au viongozi wakuu wa nchi wanakaa chochoroni. Mheshimiwa nchi zote duniani Marais wanakaa katika maeneo maalum yaliyotengwa na yenye hadhi, lakini leo Makamu wa Kwanza kaenda kuwekwa kichochoroni kabisa. Hivyo waniambie sababu za msingi za kuhama nyumba ile, nielezwe ni gharama za kiasi gani anazozitumia katika kukodi nyumba ile.

Mhe. Naibu Spika, kama sikupata maelezo ya kutosha mimi leo hapa Mhe. Naibu Spika, kazi itakuwa kubwa sana, kwani nchi hii ina matatizo mengi, tuna matatizo ya mahospitali, madawa, bajeti hazikamiliki, ukiuliza unaambiwa tatizo fedha hakuna, lakini fedha tunazitumia katika njia ambazo hazistahiki na njia ambazo kwa kweli hazituoneshi mwanga.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoka hapo nataka nije katika kitabu sasa ukurasa wa 43 kifungu cha 21 (1208) nieleze pana milioni 5,400,000/= pesa za ulinzi *(security service fees);* ulinzi huu ni wa aina gani na nani wanaolipwa, na ulinzi huu unafanyika wapi?

Jengine Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 45 kifungu cha 31 (1203) unununzi wa honda, vespa na ciao zimetengwa shilingi 351,000/= hapa sijaridhika na hizi fedha ni ndogo nataka kujua vespa gani au ciao gani inauzwa kwa shilingi 351,000/=.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 49 safari za ndani kifungu cha 22 (0301) na 22 (0302) zimetengwa milioni 40 kwa safari za ndani na milioni 30 kwa safari za nje. Mhe. Naibu Spika, hapa nataka nije nielezwe iwe Serikali au iwe wizara vigezo vinavyotumika kwa ajili ya safari napata tabu sana, kwa sababu nikiangalia safari za Makamu wa Pili halafu naangalia na safari za Makamu wa Kwanza kunakuwa kuna tofauti kubwa sana. Sasa labda nataka kujua Serikali wanatumia vigezo gani katika kuweka hizi bajeti za safari za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, halafu katika fungu 20601 Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ukurasa wa 51 mpaka 54 kama sikosei, hapa naona kidogo pana mashaka sioni kitu, yaani wenzetu hawa hawakuwekewa kitu chochote kile. Mhe. Waziri atapokuja anieleze kwa nini mafungu yote haya yana 00 tupu.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 55 kifungu 220408 Gharama za Umeme. Makisio ya mwaka jana yalikuwa ni shilingi 1,200,000; mwaka huu shilingi 5,400,000, mara tatu maradufu, tatizo liko wapi umeme umepanda mara tatu zaidi kutoka mwaka jana kuja mwaka huu. Mhe. Waziri atapokuja hapa atakuja kunieleza.

Mhe. Naibu Spika, fungu jengine nililokuwa nataka kulizungumzia ni ukurasa wa 58 kifungu 263129 Huduma za Walemavu. Mheshimiwa nina masikitiko sana, mwaka jana ilitengwa bajeti ya shilingi 258,020,000; mwaka huu zimepungua karibu zaidi ya nusu Mhe. Naibu Spika, mpaka shilingi 115,625,000. Sababu za msingi za kuwaondoshea fedha walemavu nije nielezwe, hatuwataki walemavu kuwasaidia au vipi. Mhe. Waziri akija atanieleza.

Lakini sehemu nyengine Mhe. Naibu Spika, ambayo nataka nizungumzie ni ukurasa wa 59 kifungu cha 211201 Kodi ya Nyumba (*House Rent),* mwaka jana walitengewa shilingi 98,150,000; mwaka huu shilingi 114,000,000 nataka nielezwe pesa hizi shilingi 114,000,000 ni kodi ya nyumba gani hiyo, Ikulu au kitu chengine. Mhe. Naibu Spika, Waziri atakapokuja atanieleza zaidi.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 61 kifungu 311204 Ununuzi wa *Furniture*. Mheshimiwa tumetengewa shilingi 43,000,000; kidogo napata mashaka pesa ni nyingi *furniture* hizo ni za aina gani na za maeneo gani.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi sitounga mkono bajeti hii na nataka nimuondoshee Mhe. Waziri shilingi, na nilikuwa na imani siku nyengine inawezekana lile ombi langu la kujiuzulu kwa kushindwa kazi atalisikiliza mpaka nitakapojibiwa majibu ya kuridhisha katika maeneo niliyoyazungumza.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa na afya njema asubuhi hii. Pia Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Pia Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri Fatma Fereji kwa hotuba yake hii nzuri na imeeleza mambo mengi katika bajeti yake hii ambayo yatakayofanyika katika 2014/2015. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, niwapongeze watendaji wake wote kwa umakini wao mkubwa kabisa waliouonesha. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mwenyekiti makini kabisa Mhe. Hamza kwa ripoti yake nzuri aliyoisoma hapa katika kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwenye ukurasa wa 17; Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Mhe. Naibu Spika, ninavyojua Idara hii ni muhimu sana na ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kufuatilia masuala mbali mbali yanayohusu watu wenye ulemavu. Kama tunavyojua Mheshimiwa sekta hii inagusa moja kwa moja jamii yetu iliyotuzunguka, hasa watu wenye ulemavu wanahitajia mahitaji maalum weweze kujiwezesha vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nanukuu kidogo sheria ya watu wenye ulemavu, haki na fursa namba 9 ya mwaka 2006 inasema:-

“Watu wenye ulemavu wanatakiwa kuwa na fursa iliyo sawa kwa manufaa ya taifa katika nyanja zote za kijamii na katika elimu, habari, mawasiliaono na kuwasaidia kuwawezesha, kuimarisha ujasiri amali ili waweze kupata kipato chao na maisha yao kuwa mazuri”.

Lakini niseme Mhe. Naibu Spika, kila mtu katika sisi jamii yetu ni mlemavu mtarajiwa naweza kusema hivyo Mhe. Naibu Spika, lakini na kama sio leo basi kesho unaweza kuwa mlemavu. Usijione leo mzima ukasema mimi nitakuwa mzima maisha yangu, aah, wakati wowote kama si leo kesho. Lakini wahenga walisema Mhe. Naibu Spika, ninukuu, "*hujafa hujaumbika*".

Mhe. Naibu Spika, lakini naomba nimuulize Mhe. Waziri vizuri sana yeye kajipangapanga vipi katika mwaka huu wa 2014/2015 kuwasaidia walemavu, kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, Wizara hii inataka nguvu za ziada ambayo iweze kuwasaidia na iweze kuwagusa wananchi wetu moja kwa moja sio kwa njia ya kuwaambia tu bila kuwatendea kivitendo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, niseme kidogo sekta hii kama nilivyosema ni muhimu na si ya mchezo na ya kutilia maanani sana, mimi nitoe sababu za msingi ambazo zinaweza kusababisha ulemavu. Zipo sababu nyingi mtu kupata ulemavu wa maradhi, vita, dawa za kulevya ambao tunapiga vita kila siku Mhe. Naibu Spika, hizi dawa unaweza kupata ulemavu kwa kutumia dawa hizi za kulevya, kisukari pia unaweza kupata ulemavu, homa kali, ajali, au kupigwa Mhe. Spika, unaweza kupata ulemavu.

Huduma kwa mama wajawazito wakati wa kujifungua. Mheshimiwa huduma hii kama tunavyojua, haiko makini na haiko vizuri. Kwa hivyo mwanadamu au mwanamke anapokwenda kujifungua anaweza kupata ulemavu katika kujifungua, sababu hizi ni za msingi na kuziangalia. Pia kupata mimba kwenye umri mdogo chini ya miaka 18 au miaka 35 pia unaweza kupata ulemavu Mhe. Naibu Spika.

Sasa sababu hizi nilizozieleza Mhe. Naibu Spika, zitiliwe maanani na serikali kwani wananchi wetu wakati wowote kwa matatizo niliyoyaeleza hapa wanaweza kuwa walemavu kama si leo kesho, Mungu atusaidie lakini watashindwa kufanya kazi zao za kawaida kwa matatizo haya niliyoyaelezea Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, naomba Waziri aangalie sana suala hili la kuwasaidia watu wenye ulemavu, hasa hawa wenzetu waliokuwa sio sawa katika maisha yao. Kwanza waangaliwe kwenye misaada ya kielimu Mhe. Naibu Spika. Kama tunavyojua sasa hivi wanapata tabu sana walemavu kufika skuli au kwenda katika shughuli zao za kikazi kwa sababu ya hali yao ya kimaumbile.

Pia ujasiriamali Mhe. Naibu Spika, wasaidiwe sana hawa wananchi wetu au hawa watu wenye ulemavu kuwawezesha kujikwamua katika hali ngumu ya kimaisha bila kutegemea msaada wa mtu au taasisi fulani. Hili ni tatizo kubwa Mheshimiwa katika jamii yetu, sasa watu wenye ulemavu wanategemea kusaidiwa, lakini naomba sana Mhe. Waziri kajipangapanga vipi kuwawezesha kujikwamua na kufanya kazi zao kwa umakini kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua hawa watoto walemavu wanapata tabu sana wakati wanapokwenda skuli hasa kwenye daladala, wanapopanda daladala kufika skulini kwao na kurudi. Mimi mfano mmoja naona wanafunzi wangu wa Jimbo la Bububu wanapata tabu sana kwenye gari ya wanafunzi lakini tunawapa kipaumbele sana wapate nafasi zao maalum wakifika wasaidiwe ili wakae zile sehemu bila ya usumbufu wowote. Wasikae foleni wala wasihangaishwe, na nafasi zao ziko tayari kwa kila siku ambazo wanakwenda skuli watoto hao.

Pia Mhe. Naibu Spika, sehemu zao za riziki watu hawa kufika wanazofanyia kazi ni ngumu na shida, usafiri wao unakuwa tabu, kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri aangalie vizuri hapa jinsi gani ya kuwasaidia watu hawa ili kufika katika sehemu husika za kujipatia riziki zao.

Mhe. Naibu Spika, pia tuangalie sana katika haya majengo yanayojengwa sasa hivi hayatiwi sehemu za kupandia watu wenye ulemavu wanapata shida. Kwa hivyo majengo yatojengwa haya Mheshimiwa naomba ipite sheria kamili zitiwe sehemu za kuwasaidia. Mimi nitoe mfano mdogo Mhe. Naibu Spika, jana Mjumbe mmoja alizungumza pale, kwa kweli ilinigusa kweli tukiangalia sisi Baraza letu la Wawakilishi lilivyojengwa hakuna sehemu iliyotengewa kwa mtu mwenye ulemavu kufika juu. Kwa hivyo Mheshimiwa mfano huu mzuri wetu sisi hapa, lakini naomba kama kutakuwa na uwezekano basi itiwe jampo *lift* hapa, kwa sababu alivyosema jana pale ni kweli, hali halisi anapata tabu kufika juu kwenye vikao vyetu vinavyoendelea huko juu.

Mhe. Naibu Spika, hawa watu kwa kweli wanakosa haki za msingi za maisha za kila siku, kwa kweli tuangalie sana, Mhe. Waziri aliangalie sana hilo ili tuweze kuwasaidia. Mhe. Naibu Spika, watu wenye ulemavu kila siku

hujiona hawana umuhimu katika maisha yetu au maisha yao ambayo wanayoishi na hilo ni kweli Mhe. Naibu Spika, wanajiona watu ambao wako nyuma sana, ni watu si wa kuwahurumia katika jamii yetu, kuna watu wanawadhalilisha, hawawapi kipaumbele. Kwa hivyo naomba sana suala hili Mhe. Naibu Spika, lisifanyike kwa watu hao, kwa hivyo watu hawa wanatia huruma sana na katika maisha yao duni kabisa Mhe. Naibu Spika.

Pia katika haki ya kuishi kama watu wengine wanabaguliwa sana Mhe. Naibu Spika na jamii yetu, wanatengwa, hawapewi zile fursa zinazotakiwa za kijamii kama mtu mwengine anazopata. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri aliangalie hili na aliwekee sehemu hasa ya sheria nzuri ya kuwasidia watu hawa wenye ulemavu. Pia niseme Mhe. Naibu Spika, wanakosa haki za msingi watu hawa tukianza na moja haki zao muhimu sana kama ajira. Utakuta kwa ulemavu wao wanakosa ajira serikalini hata kwenye sekta binafsi, tushaona mifano hiyo mingi na wanasikitika sana na wakati elimu wanayo pengine nzuri, lakini kwa hali yao wanaonekana kama watu hawafai. Kwa hivyo Mhe. Waziri pia hili aliangalie, anajipanga vipi kuhusu suala hili la kuwasaidia watu wenye ulemavu kwa ajili ya ajira.

Mhe. Naibu Spika, pia kwenye suala la tiba wanapata tabu hawa ndugu zetu, uwezo wa kununua dawa wanakuwa hawana, uwezo wa kujikimu kwa kweli inakuwa mgumu. Kwa hivyo naomba wawekewe kipaumbele hasa kwenye matibabu, isiwe kama mtu wa kawaida anaweza kupata *facilities* hizi au hizi, kama wao wapewe kwanza na inawezekana ikawa Mhe. Waziri aliangalie watengewe hata bajeti yao ya kupewa hata dawa bure kabisa isiwe usumbufu kwao.

Lakini Mhe. Naibu Spika, hawa watu wenye ulemavu wanapata tabu hata kununua visaidizi au zile *wheelchairs* zao wanashindwa. Na tumeangalia kitabu hiki kwenye bajeti hapa mwaka jana kuna fedha kidogo sana zimetiwa na serikali kununua visaidizi vyao. Lakini hata serikali inapotoa fedha Mhe. Naibu Spika, hizi fedha hazifiki kwa wananchi au walengwa zinaishia, mitaani huku chini, kwa sababu wananchi wetu kila siku wanakuja na shida hii hii, na ukiwaambia mmesaidiwa vipi na serikali au na Wizara husika wanasema hakuna kinachofanyika kule.

Kwa hivyo Mhe. Waziri ninakujua makini na una huruma, una imani kabisa, kwa hivyo naomba suala hili ulifuatilie vizuri hizi fedha japo kidogo lakini zifike kwa walengwa wetu, wananchi wetu hawa watu wenye ulemavu. Na kawaida sio wengi kwa hesabu tunaweza tukawajua. Mimi naweza kukwambia hata jimboni wako wangapi nitakwambia watu wenye ulemavu. Na mimi mwenyewe nishawasaidia *wheelchairs* lakini hazitoshi Mhe. Naibu Spika. Lakini naomba Wizara yako Mheshimiwa tusaidiane kuwajua watu na kuwasaidia hasa kwenye hivi visaidizi vyao.

Mhe. Naibu Spika, lakini jambo jengine la muhimu, la msingi kabisa wanakosa elimu ya juu hata ya msingi hawapati. Utakuta wana upeo mzuri, wana uelewa mzuri lakini unakuta hawapati zile fursa kwa sababu ya fedha hawana za kujisogeza mbele kupata elimu ya juu ya mahitaji yao. Mimi nitoe mfano mzuri kabisa Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa Bungeni katika kamati ya Kanuni kama unakumbuka alikuwa jamaa mmoja mtu mwenye ulemavu anaitwa Amon Mpanju; yule jamaa mimi ninampongeza sana na ninamsifu sana yule jama alikuwa kwenye Kamati ya Kanuni hodari sana yule jamaa, lakini ni mtu mwenye ulemavu haoni. Mimi naona ajabu anasoma vipo na mtu mwenye ufahamu mkubwa Mungu kampa yule mtu. Kwa hivyo hawa watu mimi ninaamini wana uwezo mkubwa lakini hawaonekani katika jamii yetu. Kwa hivyo ninaomba Mhe. Waziri uliangalie sana katika elimu watu hawa wanaweza kufanya vitu vizuri katika jamii yetu na katika taifa letu la hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine mishahara yao midogo hawa watu haiwakidhi mahitaji yao. Kwani ukisema mtu humu kufanya kazi afanye kazi moja, kazi moja mahitaji madogo kwa sababu hali yake ilivyo mtu aliyekuwa sawa anaweza kufanya kazi asubuhi, akamaliza kazi ya mchana akaenda kazi nyengine ya usiku, lakini huyu hawezi kufanya kazi hizo mbili. Kwa hivyo ninaomba mishahara yao kupitia Mhe. Waziri iongezwe hawa wapewe kipaumbele sio kama watu wengine wanapewa mishahara, iongezwe kwa sababu mahitaji yao, nguvu zao za kazi ni ndogo sio kama mtu wa kawaida. Nilikuwa ninaomba Mhe. Waziri hilo uliangalie sana katika haki za hawa watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, niseme jamii hii inahitaji msaada wa kila mara kusaidiwa watu, kila wakati wawe wanapata msaada na wanaangaliwa na kuulizwa mahitaji yao kwani wanapata tabu sana kwa kweli katika jamii yao na wanavyoishi.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, nije kwenye jambo moja katika jamii yetu ambalo jambo si busara katika maisha halisi ya wazanzibari, nchi yenye sifa za kipekee katika uso wa kidunia kwa wema, kwa heshima, kwa busara imani

kubwa tuliyokuwa nayo. Wananchi kwa imani kwa kila kitu tulivyojaaliwa katika visiwa vyetu vya Zanzibar hasa Unguja na Pemba.

Lakini vipo vitendo Mhe. Naibu Spika, vinasikitisha kwa mfano, yaani havifai hata kusema vya kinyama, vya kishenzi ninaweza kusema. Watu wenye ulemavu Mheshimiwa hasa ulemavu wa akili utashangaa wanapata ujauzito wanakuwa vipi? Watu wanawadanganya au kwa sababu vile akili zao wanawapa ujauzito watu hawa na watu hawa wasiojulikana, hawajulikani hata nani, unakuta yule mtu mwenye ulemavu wa akili anakuwa mjamzito. Kwa hivyo hilo Mhe. Naibu Spika, naomba tuliangalie sana watu hawa wachukuliwe hatua lakini sheria za nchi hazitekelezwi ila tujue majukumu yetu. Kwani suala hili linafanyika lakini hatusikii mtu kufungwa au kutiwa adabu kubwa kabisa za kuwakomesha na kuwapa onyo wale wengine watakaofanya mambo hayo.

Lakini tunakuta sheria zipo hatuzitekelezi. Mhe. Waziri naomba ulisimamie hili watu kama hawa wanaofanya vitendo kama hivi vibaya tuweze kuwasimamia na kuhakikisha sehemu ambayo husika kwa vitendo hivi viovu havina maana, vinatia sura mbaya katika nchi yetu, katika jamii yetu na inafanyika ndani ya jamii yetu ninaweza kusema hivyo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Idara hii ya watu wenye ulemavu kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ilikadiriwa kutumia mwaka jana karibu milioni 400 lakini imepata milioni 200 nafikiri. Lakini naiomba sana serikali Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo hii huduma ni muhimu kwa jamii yetu imetugusa moja kwa moja, kwa hivyo naiomba serikali kupitia Wizara yako Mhe. Waziri hili lipewe kipaumbele sana kwa hizi fedha zote za kitabu hiki ulizoziandika zipatikane hasa kwa Idara hii ya Watu wenye Ulemavu zipatikane vile vile ulivyoziomba. Naomba Mhe. Naibu Spika, serikali iangalie sana suala hili la watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie sana kuingia katika haya madawa ya kulevya katika ukurasa wa 21, kifungu namba 56 kitabu hiki cha Mhe. Waziri. Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Cha kusitisha na cha ajabu Tume hii ina jukumu la kuratibu mapambano vita dhidi ya biashara, matumizi, uingizwaji na usafirishaji wa dawa za kulevya. Mhe. Waziri kitabu chako ndio kinasema hivi ni kazi yako na ni kazi ambayo kitabu hiki kinasema kudhibiti uingizwaji na usafirishaji wa madawa ya kulevya.

Lakini Mheshimiwa cha kusikitisha zaidi pia mimi kwa kweli katika ukurasa wa 23 na kitabu hiki kimeeleza vizuri Mhe. Waziri mimi inaniuma sana sana kuona vijana wanapoingia kwenye janga hili la madawa ya kulevya, kwa kweli hili jambo la kuumiza sana na vijana wetu wanapoingia hapa wanashindwa kufanya chochote; kusoma, kufanya kazi au kuendesha taifa letu kwa makini kabisa, wanakuwa si watu wa maana au si watu wa kusaidia taifa hili.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi ilikuwa inanisikitisha na inaniuma sana, tukiona kwenye kitabu cha Mhe. Waziri hapa katuelezea ukurasa wa 23 *bulletin* ya 59, jumla ya watu 23 wamekamatwa kwa makosa ya dawa za kulevya na makosa ya aina mbali mbali, ama ya kuingiza, ya kuuza au kwa njia nyengine. Lakini unakuta kesi hizi ziko Mahakamani mpaka leo, na Waziri katwambia kwenye kitabu chake humu ushahidi haujapatikana mpaka leo. Sasa tunasubiri nini hawa watu tusiwafunge au tusiwatie adabu kuwapa funzo na wale wengine watakaoleta au watakaouza madawa hayo.

Kama nchi za wenzetu niliona juzi kwenye gazeti liliandikwa kama mwezi mmoja nyuma au miwili hivi, kuwa mtu kaenda kuomba *visa* ya China anaambiwa subiri kidogo kule gerezani wako Watanzania wengi mpaka wachukuliwe hatua ndio utapata *visa* wewe.

Kwa hiyo, inamaanisha wazi kwamba Watanzania ndio wanaopeleka madawa ya kulevya na wengine wanaleta hapa, hapa wanachukua wanapeleka kule lakini njia kuu ni hapa Tanzania kwa ujumla kuingiza madawa hayo. Kwa nini hawa watu hawapewi adhabu kama ya kunyongwa au kufungwa maisha, hata wale wengine wakajua kama mimi nikifanya biashara hii haramu basi naweza kumaliza maisha yangu kufungwa au kunyongwa.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri na hili nishalisema mwaka jana hapa, lakini nashangaa halijafanyiwa kazi hakuna kinachoendelea mpaka sasa hivi. Nilikuwa naomba serikali ichukue hatua ya kutoa sheria nyengine; atayekamatwa na madawa ya kulevya basi pale pale achukuliwe hatua kama ya kunyongwa au kufungwa maisha huyu mtu, bila ya ushahidi kukamilika hili suala lifanywe hivyo hivyo, kupewa mfano wale wengine wataogusa haya madawa ya kulevya.

Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri uliangalie sana hilo kwa ajili ya watoto wetu au vijana wetu hawa wanaoishi hapa Zanzibar wasiharibike kwenye madawa haya yanayoingizwa.

Lakini niseme suala moja pale Skuli ya Bububu kwenye jimbo langu. Skuli ile ni nzuri wanafunzi wanasoma wa msingi na sekondari, lakini cha ajabu panauzwa madawa pale nyuma, hakuna uzio wa skuli, watu wanakaa kama kijiwe chao cha kuuzia madawa ya kulevya. Mimi juzi nilipokwenda nimeambiwa, nikaambiwa hapa watu wanauza madawa, watoto wengine wanaharibika kupitia humu. Kwa hivyo, naomba serikali kwanza itie uzio skuli ile yote iwe huwezi kuingia ndani. Skuli ile ina eneo zuri, eneo la bahari lakini hakuna udhibiti wowote wa lile eneo limekaa tu ovyo. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri hilo pia aliangalie; ile skuli itiwe uzio haya madawa yaweze kuondoshwa isiwe pale ndio kama sehemu ya kufanya biashara ya madawa ya kulevya.

Lakini cha kusikitisha Mhe. Mjumbe aliyepita kasema juzi hapa, pamekamatwa watu *airport* na tumeambiwa sote na habari tunazo, karibu kilo 50 za madawa ya kulevya na tunaambiwa jana Mhe. Hamza Hassan Juma alisema hapa *camera* zimeharibika au nafikiri Mhe. Makame Mshimba Mbarouk yule, alisema *camera* ziliharibika muda ule, kwa hivyo hatujui yale mabegi ya nani. Na ilipotolewa ripoti ya *IGP* wamekimbia wale watu. Sasa madawa ya kilo 50 jamani watu wetu wangapi wataharibika kwenye madawa yale, na madawa yameingizwa hapa yanasafirishwa kupelekwa sehemu nyengine.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba huu udhibiti kama nilivyosema mwanzo adabu bado haijapatikana kwa vijana wetu, kama itakuwepo adabu nzuri hao wanaoingiza nafikiri madawa yatakuwa hayaingii tena, kwani nasikia huu mtandao ni mkubwa sana, na kama hatutakuwa makini na tukaamua sote haya madawa ndio itakuwa biashara kuu hapa Zanzibar. Kwa hivyo, naomba tuwe makini na tuwe wajasiri katika kuamua madawa haya kuweza kuyadhibiti, kwani sisi hapa tuna historia nzuri ya hekima na busara; watu wenye busara, watu wenye kusaidiana naamini mambo haya tunaweza kusaidiana na wapo raia wema watatusaidia suala hili la kuwafichua hawa wanaoingiza madawa.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwenye suala la *Sober house*. Suala hili ni zuri na mimi mwenyewe nishasema nishapeleka watu hawapungui watano *Sober house* na wengine nimewapeleka Pemba. Tuwasaidie vijana ili waache madawa ya kulevya, na baadhi ya vijana niliowapeleka ni wa Mji Mkongwe, wakanifuata wakataka nauli na pesa ya kuingilia kule. Mimi nikawapa fedha zile ili waache yale madawa.

Lakini cha kusikitisha nasema fedha zangu kwa baadhi ya wale vijana zimepotea, wamerudi tena wameingia kwenye janga hili la unga kama kawaida. Sasa tutakuwa tunawapa pesa *Sober house* za kuwaweka wale watu kwa maadili mema lakini baada ya muda wanarudi tena kwenye madawa haya. Kwa hivyo, itakuwa tunatibu kisha wanarudi, sasa hiyo itakuwa pesa zinapotea za wananchi wetu na serikali. Mhe. Waziri wizara yako itapoteza fedha nyingi. Kwa hiyo, naomba *Sober house* ziendelee, lakini serikali iangalie kwa makini uingizwaji huu wa madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi kwa heshima kubwa na taadhima naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia nafasi hii asubuhi ya leo nikaweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja nitaanza kuchangia kuhusu safari 18 zilizoandikwa kwenye kitabu hiki. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwenye majumuisho yake aje anieleze safari hizi zimeleta tija gani na zimegharimu kiasi gani cha fedha.

Nikitoka hapo niende kwenye hizi ruzuku ambazo wanapatiwa hawa vijana wa *Sober house*. Vijana hawa tulibahatika kuwatembelea, narudia tena nilipochangia hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais tulitembelea *Sober house* iliyoko Nyarugusu na vijana hawa walitwambia kwamba wana matatizo makubwa. Lakini bahati nzuri Mhe. Waziri kwenye kitabu chake ametwambia kama wana ruzuku ambayo wanawapatia vijana hao. Nataka akija aje anambie ni kiasi gani ambacho wanawapatia vijana hawa katika kutekeleza mahitaji yao ya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Idara ya Watu wenye Ulemavu. Idara hii ina jukumu kubwa sana kwa watu hawa wenye ulemavu. Watu wenye Ulemavu wanabakwa, matokeo yake kesi zile zinaingia mitini, ukiulizia unaambiwa hakuna ushahidi eti mpaka mtu yule ajifungue, akishakujifungua kichukuliwe kipimo kipelekwe Dar es Salaam, baada ya mwaka ndio inaletwa jawabu kama mtu huyu ushahidi haukupatikana kesi zile hazionekani zinakokwenda. Hili ni tatizo kubwa sana.

Kwenye kitabu chao wameelezea kama wameshapitia skuli na kutoa taaluma ya watu wenye ulemavu, lakini kuna skuli wako watu wenye ulemavu wapo pale wanasoma na vyoo vya skuli viko sawa sawa na wale watu ambao hawana ulemavu. Sasa hivi wanawasaidia vipi hawa watu wenye ulemavu hasa skuli za vijijini, bado skuli za vijijini hawajaweka miundombinu ya watu wenye ulemavu. Mhe. Waziri kwa kupitia Idara yako hii ya Watu wenye Ulemavu mwende tena katika skuli mfuatilie na muelezee kama watu wenye ulemavu na wao wanahitaji miundombinu yote na huduma zote wanahitaji sawa kama na waliokuwa si walemavu, kwa sababu wakati wowote unajiona wewe ni mzima lakini unaweza ukapata ulemavu, hata kama hukuzaliwa na ulemavu lakini unaweza ukapata ulemavu. Unapofanya dharau na umepewa wizara kama hii ikawa hutekelezi yale majukumu ambayo umepangiwa kuyatekeleza, ujue wakati wowote na wewe linaweza likakuzungukia.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye hizi kalenda 800 ambazo zimechapishwa katika kipindi cha mwaka 2014. Kalenda hizi pamoja na mambo mengine yote waliyoorodhesha kwenye sehemu hii ya 12 aje anambie Mhe. Waziri zimegharimu kiasi gani cha fedha, sitochoka kuhoji mambo haya ya pesa kwa sababu kila siku tunapitisha bajeti na ukienda kwenye mawizara unaambiwa hili halijakamilika, hili limekamilika, unaambiwa Wizara ya Fedha bado hawajatuingizia fedha. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aje anambie pesa hizi ambazo zimetumika kwenye gharama hii ni kiasi gani cha fedha, hata kama wamepewa na wafadhili na wao pesa zao za maendeleo zinazoletwa na wafadhili zinatakiwa ziingizwe.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya wameshindwa mpaka leo, kitabu hiki kinasema kuwa kuna watu 21 ambao walitumiwa au walikamatwa na madawa ya kulevya, lakini mpaka leo hatujasikia nani kawekwa ndani au hukumu gani imepatikana, bado tunaendelea kuwaathiri vijana wetu wa Zanzibar. Vijana wengi wa Zanzibar wamepoteza mwelekeo kwa madawa ya kulevya, ukitembea kwenye *Sober house* unawakuta vijana wasomi ndio waliokumbwa na kadhia hii ya madawa ya kulevya. Sasa Mhe. Waziri tatizo hili litaondoka lini ikiwa serikali haitoi hukumu kwa hawa wanaokamatwa na madawa haya, tumechoka, vijana ajira hakuna na matokeo yake vijana wanapoteza mwelekeo wa maisha.

Mhe. Naibu Spika, kwa haya machache niliyoyachangia naomba niunge mkono hotuba hii ya mama yangu Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej, lakini aje anipatie majibu yangu haya niliyomuuliza.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii nikushukuru sana na mimi kunipatia nafasi hii ya kuchangia kitabu hiki kwa Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwanza niseme kwamba, Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kweli ina mambo muhimu sana ambayo yamelenga katika kitabu hiki, yale mambo nyeti ya nchi; ukija kwenye mazingira nitaanza huko Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, katika ulimwengu tunaona mambo mbali mbali ya mazingira na ikiharibika dunia kwa mazingira basi tujue na sisi tunaingia katika dunia hiyo. Niseme kwamba tabia nchi ina mwelekeo wa kuharibu mazingira ambayo yale mengine si ya kutarajia. Tuseme ni hivi karibuni mvua zetu zilizonyesha hizi zimeharibu mazingira na zimeharibu maendeleo mbali mbali ambayo yanapitia kwa wananchi. Sasa nimuombe Mhe. Waziri kwamba ashirikiane na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ili somo la mazingira lipelekwe katika skuli. Kwa nini nikasema hivyo?

Mhe. Naibu Spika, ni hivi karibuni Kamati yangu ilitembelea sehemu mbali mbali na tukaona namna ya athari ya mazingira. Tulikwenda Kisiwa cha Chumbe tumeona namna gani mazingira ambayo yamekifanya kisiwa kile, lakini si hayo tu, niiombe Wizara ya Afya kwamba ni wizara ambayo kwa kweli imeharibu mazingira kwa Kisiwa cha Chumbe na sifikirii kama ni kisiwa kile tu kwa mujibu wa maelezo tuliyoyapata. Zinaokotwa sindano, kunaokotwa vile visu vya kufanyia operesheni, kunaokotwa mambo mbali mbali yenye kuharibu mazingira. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri pamoja na Waziri wa Afya washirikiane wajue ni namna gani mazingira ya Wizara ya Afya yaweze kufanyika ili vitu vile visitupwe ovyo. Kwa kweli kisiwa kile kimeharibiwa vibaya sana kwa vitu kama hivyo, sindano za aina mbali mbali zinaokotwa. Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Waziri wakae pamoja, kwa sababu haya ni mazingira ambayo yataleta athari katika visiwa vyetu. Hilo moja nilisema nilizungumze kwanza.

Jengine nimuulize Mhe. Waziri na nimtake aje anipe maelezo. Kipindi cha mwaka jana tulizungumzia namna gani visiwa vinavyoathirika kwa mmong'onyoko (*erosion*), hebu atwambie wizara yake ilifanya nini na nini kuhakikisha visiwa vile au kama wanasaidiwa na wafadhili wamefanya nini na nini?

Kwa sababu sasa hivi ukiangalia kwa upande wa Pemba kwa kweli visiwa vingi sana viko hatarini, na tuliambiwa hapa na tulipata semina tukaambiwa kwamba kuna visiwa ambavyo viko hatarini. Sasa nimuulize Mhe. Waziri je, kuna mwelekeo gani wa kuweza kusaidia mmong'onyoko? Tusiende mbali hapo Maruhubi katika Chuo chetu cha Utalii, mmong'onyoko mbaya sana ambao tukifanya mchezo basi chuo kile mapesa yale yaliyopotezwa pale hebu Mhe. Waziri atwambie ana mashirikiano gani na Wizara husika kuhakikisha kwamba haya mazingira yasije yakatuathiri kwa kiasi kikubwa. Nakuomba Mhe. Waziri.

Nikitoka hapo nije katika madawa ya kulevya. Wenzangu wamezungumzia sana suala hili lakini mimi najiuliza, hivyo kweli tunashindwa kukamata watu wanaoleta madawa ya kulevya na tukawapa hukumu ambazo zikawaridhisha wananchi? Kwa sababu miongoni mwetu sisi humu ni wazazi hasa sisi wanawake, tunaumia sana kuona vijana wetu wanafikwa na maafa ambayo ni maafa mabaya. Kwa sababu hawa ndio viongozi tunaowatarajia, sisi yetu yamekwisha, tuking'atua mguu wanaweka wao. Sasa kwa kweli tuhakikishe kwamba vijana wetu hawa tuwalinde lakini tutawalindaje?

Kuwalinda vijana hawa ni kwamba mimi nina hakika tunawajua kati yetu, lakini sisi wenyewe ndio wabaya, wewe unakuta mtu anakamatwa na madawa ya kulevya na wewe utaambiwa kwamba unga, haujulikani, unaitwa unga tu, lakini hatujui kama unga wa ngano, unga wa sembe au unga wa nini, lakini athari zake ni kubwa sana Mhe. Naibu Spika. Namuomba Mhe. Waziri wafanye jitihada zao kuhakikisha hao wanaokamatwa na madawa haya ya kulevya tusiwaonee huruma, wanatuangamizia vijana wetu, na vijana wamechoka kwa sababu hakuna hatua inayochukuliwa.

Mimi namuunga mkono Mhe. Viwe Khamis Abdalla, vijana wamechoka kwa sababu wanaona vijana wenzao jinsi gani walivyo, utamuonea huruma mtoto mdomo umeregea utafikiri kapata ulemavu kumbe ni unga tu, kusema neno moja halieleweki kwa kweli ni athari kubwa sana kwa vijana wetu. Mimi namuomba sana Mhe. Waziri ashirikiane na wizara husika hili jambo lisiachiwe ovyo, kwa kweli vyombo ambavyo vinahusika na wizara yako kuhusu madawa ya kulevya basi mshirikiane kwa pamoja.

Lakini nikiondoka hapo nije katika *Sober house*. Mimi namuomba Mhe. Waziri aje anieleze hivyo kweli kwenye *Sober house* kumetengewa kiasi gani hasa. Safari ile tulilizungumza tukasema kwamba *Sober house* zitafutiwe fedha za kuweza kuwakimu watoto hao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nikitembelea *Sober house* kwa kweli kuna vijana wetu ni wale *educated* huwezi kufikiria. Sasa kama hawa vijana ambao sasa hivi wako katika *Sober House* lakini wana uwezo wa masomo wana uwezo wa kila kitu tunawafanyaje hawa? Hilo moja lakini jengine kwa nini hatuwatafutii vitega uchumi hawa watoto wa *Sober House*. Kuna *Sober House* nyengine zina Vitega Uchumi tumeona wanalima baadhi ya mambo.

Sasa hebu tuzishughulikie hizi *Sober House* na *Sober House* haziridhishi Mhe. Naibu Spika, naiomba wizara hii kwa sababu ndio Wizara husika ya Makamu wa Kwanza wa Rais hebu tuache tuliyonayo wale ni watoto wetu " *Msohili ana lile*" mimi nasema wala tusiwacheke wala tusiwadharau kwa sababu ni Mwenyezi Mungu ambaye ameumba, kama hukuvuta bangi utavuta sigara, kama hukuvuta sigara utakunywa pombe, kama hukunywa pombe una mambo mengine unafanya Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, suala hili tusilifanyie mchezo naomba sana hawa vijana wetu kwa kweli lazima tuwalinde na tuwasaidie, tusiseme tu *Sober House*, ukienda wewe mwenyewe utaona vibaya, na utaona haya kwamba hizi ni nyumba za *Sober House* wakati zile tunatakiwa vijana wetu hawa tuwaenzi vizuri ili tuhakikishe wanachama na haya madawa ya kulevya. Lakini ni tofauti mazingira yao Mhe. Naibu Spika, lazima watafute tena unga kwa mazingira ya ndani ya nyumba tu na mazingira ya maisha yao.

Pia nitoe wito kwa wazee; Mhe. Naibu Spika, mtoto akinyea kiganja hakikatwi. Unachukua sabuni unamsafisha basi. Natoa wito kwa wazee tusiwanyanyapae watoto wetu kwa sababu tunamokwenda humo *Sober House* wanatwambia kwamba wazee na wao upande mwengine wanachangia. Kwa sababu wanapokwenda vijana

wameshajua kwamba sasa hivi mimi nimepungua, na wavutaji wa unga wanapokwenda kwa wazee, wazee wanawakaripia, na kumfukuza unamzidishia matatizo yule, unampa fikra nyengine za matatizo badala ya kumsaidia, kama hukumsaidia wewe mzee ulomtoa tumboni ataweza kusaidiwa na mwengine nani? Na wewe mama na baba muwape mawaidha mazuri watoto.

Kwa hivyo, natoa wito huu kwa wazee hasa wa kike; kwa sababu ndio wanaokaa na watoto kwa malezi. Naomba wazee wenzangu wa kike, watoto hawa tusiwanyanyapae; ni watoto wa kuwapa elimu zaidi hasa ukiwa wewe ni mzazi Mhe. Naibu Spika.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nimepata taarifa kwamba aneyeshughulikia haya madawa ya kulevya ni Fatma Sukwa amepelekewa barua kwamba watoto chini ya 18 waondoshwe kwenye *Sober House*. Sasa mimi nitamuomba Mhe. Waziri aje anieleze kulikoni hapa. Kama mtoto wa 18 unamuondoa wakati kule ndio wanapata mafunzo unamuacha tena akae huku huku kwenye madawa ya kulevya ili azidi kupotoka. Hilo naomba aje anieleze vizuri Mhe. Waziri.

Jengine wanawake ambao wana watoto wachanga pia tunaambiwa waondolewe. Sasa naiomba Wizara hii ishirikiane na Wizara husika ya walezi wa watoto hawa wapelekwe lakini mama zao waachwe kule kule ichukue jukumu; serikali ya watoto akina mama wenye watoto wachanga kwamba walelewe na serikali.

Namuomba Mhe. Waziri hapo ashirikiane na Waziri wa Wanawake ili tuhakikishe kwamba na wale watoto na wao wanapata malezi mazuri, na mama zao wanapata mawaidha mazuri katika *Sober House*.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, nije katika watu wenye ulemavu. Jamani naomba sana sisi hatumalizi kuumbwa mpaka siku ya kufa, na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye Rehma unaweza kuwa unasema, unakwenda kwa mikogo, unaringa njiani Mwenyezi Mungu akataka kukuonesha kwamba yeye ndiye muweza wa yote. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, kupitia kwa Mhe. Waziri watu hawa si wa kuwadharau hata kidogo, watu hawa ni wa kuwanyenyekea. Kwa nini nikasema hivyo? Mimi naona bado hatujashughulika vizuri sana na watu hawa. Sasa nitamuomba Mhe. Waziri pamoja na kwamba wana chama chao, nitakuomba Mhe. Waziri uje unambie umewafanyia nini na nini watu wenye ulemavu; kwanza vifaa vyao vya kusomea vipatikane kwa mujibu wa kila mtu na ulemavu alionao.

Naomba nikuulize umeshirikiana vipi na Wizara husika kutafutiwa wale ambao hawajapata ajira na wako wamesoma. Umeshirikiana vipi na wizara husika ya kuhakikisha hawa wanapatiwa kitega uchumi cha kuwaendeshea maisha yao.

Tatu nataka uje unambie Mhe. Waziri ni wangapi watu wenye ulemavu walioajiriwa maofisini, na wangapi ambao hawajaajiriwa, najua takwimu mnazo ni walemavu wangapi kwa Unguja na Pemba ambao tunao kwa hivi sasa na wangapi wameajiriwa na wangapi hawajaajiriwa, na wangapi wana vitega uchumi na wangapi hawana vya kuwasaidia kuendesha maisha yao?

Mhe. Naibu Spika, nilisema niyaseme hayo lakini mpaka nije nipate maelezo. Siungi mkono mpaka nije nipate maelezo mambo yangu ambayo nimeyataja hapa. Baada ya kusema hayo ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe wengi walichelewa kuingia ndani ya ukumbi na tukaelezwa kwamba leo hotuba hii tunamalizia mchana, na jioni tunafanya majumuisho na kupitisha vifungu. Kwa hivyo, wako watu wananiletea na kusema niwaweke jioni. Jioni hakuna michangio tena muda ndio huu huu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuniruhusu kuchangia hii Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika: Ujali muda**.**

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika,nitajali muda.

Kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Fatma Abdul-habib Fereji na vile vile hapo hapo nimpe pole kwa wizara yake ngumu. Niwapongeze watendaji wake vile vile wa wizara hii akiwemo Katibu Mkuu makini Dr. Omar Shajjak na Naibu wake.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuanza mchango wangu mimi nataka nimtume Mhe. Mohamed Aboud Mohamed akamshauri Mhe. Balozi ili apeleke salamu kwa Mhe. Rais, hii Wizara huyu mama anataka kusaidiwa japo Naibu Waziri. Wizara ni nyeti; imekuwa ikipoteza maisha ya watu siku zote, tumeshuhudia hapa kama Wizara ya Kilimo ina Naibu Waziri, Wizara ya Mifugo ina Naibu Waziri na ukilinganisha huwezi ukasema kipi bora. Lakini hii wizara nyeti, wananchi wanazidi kupotea, wakiwemo vijana ambao ni nguvu kazi ya kesho kutwa. Mhe. Balozi hizi salamu zipeleke kuwa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni alisema hii Wizara ipo haja ya kupatiwa Naibu Waziri. (*Makofi*)

Baada ya hapo niendelee na ukurasa wa 17 Mhe. Naibu Spika, Idara ya Watu wenye Ulemavu. Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu nimekuwa nikizungumza kuhusu tatizo la Serikali kuletwa mswada wa Sheria Barazani. Wajumbe tunatunga Sheria kupitisha lakini Kanuni za kusimamia Sheria hii hazipo, huu karibu mwaka wa nne nafikiri kanuni hizi hazijafika, Serikali iko mbioni sijui hizo mbio zitaanzia wapi na kumalizikia wapi.

Watu wenye ulemavu wanazidi kuteseka na kunyanyasika ni kitu cha kusikitisha sana. Kanuni ipo haja ya kuletwa haraka sana ili kuwasadia watu hawa. Watu hawa wamekuwa wakiumia siku hadi siku, utakuta hata wakati wa kukata barabara hawaheshimiwi, hawapati haki, kanuni haiwalindi na kwenye daladala wanateseka hawa watu kanuni haipo, bado kanuni haijaja hapa Barazani ya kuwalinda watu hawa.

Hebu tuangalie katika nchi nyengine kama Sweden, Norway viongozi wakuu wanawachukua katika msafara watu hawa wenye ulemavu, wamepewa kipaumbele wanasaidia siku hadi siku. Cha kusikitisha zaidi Mhe. Naibu Spika, Idara ya Watu wenye Ulemavu ukurasa wa 36 Idara nyeti hebu tuangalie ukurasa wa 36 pesa zilizotengwa ni milioni 366 hadi kufika Machi milioni 48 asilimia 12 kupewa. Mhe. Naibu Spika, huu ni mzaha tena mkubwa sana, kutoka milioni 196 hadi milioni 48 tunafanya nini? Kitu cha kusikitisha kabisa hichi. Mhe. Naibu Spika, hapa nataka kumwambia Mhe. Waziri nitakuwa mkaidi mpaka nipate Kiswahili ambacho nitakifahamu ili kuweza kupitisha fungu hili.

Chengine kuna hizi Jumuiya zilizotajwa Mhe. Naibu Spika, za JUWAZA, CHAVIZA, Umoja wa Wanawake. Wanachama wa Jumuiya hizi wananufaika vipi na misaada inayopatikana kwa hisani na ruzuku ya Serikali karibu milioni mia tisa sijui na ngapi zimetolewa hebu tupate maelezo, na wengine hawa watu nimerudia juzi kuna shamba kule hawana hata baskeli za kupanda katika vyama hivi. Kuna baskeli wamezifungia ndani zina malengo gani hizi si kuwasaidia walemavu, serikali sijui italisaidia vipi, suala hili ni la kukaa na mkaliangalia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije Tume ya Ukimwi Zanzibar ukurasa wa 38. Ni chombo muhimu lazima kujengwe uwezo na kuweza kunufaika wananchi kutoa elimu pamoja na kuchukua hatua za kupunguza maambukizi ya Ukimwi. Narudia tena kusema kwamba hapa lazima papatikane Naibu Waziri. Hii Wizara ni kubwa, Ukimwi leo unazidi kuendelea kukua, dawa za kulevya hazisemeki, tatizo lingekuwa sugu na zaidi suala la Ukimwi linachangiwa na nini? Hebu tutafutieni sababu Waheshimiwa kuna mambo mengine tuangalie. Nilisema mimi kabla ya siku tatu hapa nyuma; Uganda wenzetu wamefanikiwa kupiga marufuku nguo fupi, nchi ambayo inaoongozwa na Wakristo kiasi fulani.

Mhe. Waziri mimi nafikiri ipo haja ya kuangalia mazingira haya; wewe ni Waziri wa Mazingira na haya ni mazingira ya kuvaa nguo fupi, nguo za vimini zimeshafika wakati Mhe. Waziri zipigwe marufuku, vimekuwa vivutio kwa vijana wetu. Tusikae Barazani kuidhinisha mambo tusiyokuwa na uwezo nayo, kama hapa Tume ya Ukimwi inatakiwa 502 inakwenda kupewa milioni 211sawa na asilimia 42; *We are not Serious!*

Mhe. Naibu Spika, nimalizie na Idara ya Mazingira kwa kuwa ni Ofisi iliyokuwa haijafanyiwa haki iliyoko Maruhubi. Ndugu yangu Hamad Mjaja pale chumba chake utafikiri banda la kuku ndio Ofisi ya Mazingira. Ofisi ya Mazingira inatakiwa iwe mfano wa Mazingira, unaingia kwenye Mazingira yale dirisha hulijui liko wapi, mlango wa kuingilia haupo.

Ofisi ya Mazingira inakusanya pesa chungu nzima haielekei na sijui kama yule Mkurugenzi anayo gari sifikirii. Ikiwa Ofisi ya Mazingira haijajengwa kimazingira haswa, tunajihukumu vipi haya mazingira sisi wenyewe tutakuwa na mazingira kweli. Hii Ofisi mimi nitahitaji maelezo Mhe. Waziri kama kuna kiwanja kinatafutwa, lakini kama Ofisi ya Mazingira ile hatuwezi kuwa walimu ikiwa hali kama ile. Ofisi hairidhishi hata kidogo ile ya Mazingira.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, kama ulivyosema tujali muda, na mimi nimeujali sana Mhe. Naibu Spika, nitahitaji maelezo kwa Mhe. Waziri ili tuweze kumpitishia mafungu yake. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Sasa tumebaki na wachangiaji wanne naomba muda tutumie ili sote tupate kuchangia. Wa kwanza Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Mussa na tunamalizia na Mhe. Muasisi Saleh Nassor Juma.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Niabu Spika, na mimi kunipa fursa hii adhimu ya kuchangia hotuba ya Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyetujaalia tupo hapa tukiwa wazima wa afya.

Kwanza nichukue nafasi hii Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wa wizara kwa kweli kwa kufanya kazi nzuri katika utayarishaji wa hotuba hii. Lakini pia kwa sababu mimi katika kipindi kilichopita nilikuwa katika Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Nilipata fursa nzuri ya kufanya kazi pamoja na Wizara hii, na kwa kweli niliona mambo ambayo yalikuwa yanafanyika kidogo kuna ugumu wa kuyafanya hayo, na sote tunaelewa kwamba tatizo kubwa linakuwa zaidi ni kuhusiana na Bajeti ambayo wanaipata, lakini vile vile tatizo la utaalamu katika fani mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze katika suala la Walemavu. Mhe. Naibu Spika, sote tunafahamu na wengine wamechangia vizuri sana iko haja kubwa ya kutaka kufikiria suala zima la kuwahudumia walemavu katika nyanja mbali mbali ikiwemo afya, sheria na elimu pamoja na kuweka miundombinu ambayo itakidhi mahitaji ya walemavu.

Kinachosikitisha Mhe. Naibu Spika, kwamba bado suala hili hasa kuhusiana na miundombinu katika majengo yetu ya Serikali pamoja na majengo mengine yanayotoa huduma bado miundombinu kwa kweli haijawapa nafasi walemavu kwa ajili ya matumizi.

Mhe. Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu tuna vigezo katika majengo mengi ya Serikali yana upungufu, sitaki kuyataja yepi lakini wengi sisi tunayafahamu. Lakini Mhe. Naibu Spika, suala zima la elimu.

Mhe. Naibu Spika, tunafahamu kwamba elimu inahusiana na masuala ya walemavu ipo lakini haijajitosheleza. Mhe. Viwe Khamis Abdalla ameelezea vizuri, sana ukienda katika maskuli mengi hasa ya vijini kwa kweli wanafunzi wengi au watoto walemavu wengi wanakosa vifaa vya lazima vya kusomea. Sasa mimi nilikuwa namuomba hapa Mhe. Waziri katika hili kwa kweli kuna upungufu mkubwa, na asaidie ili tuhakikishe kwamba hawa kweli tunaposema tunataka kuwapa elimu, basi tuwape elimu ambayo itawapa tija wao walemavu.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kuzungumzia sana suala la elimu sio kwa walemavu tu, lakini nafikiri umeshafika wakati tunahitaji elimu sisi kama wananchi wa Zanzibar. Kuna vipindi mbali mbali ambavyo vinaendeshwa lakini bado wananchi hawajapata elimu ya kutosha na namna ya kuwahudumia walemavu. Kila mtu ana wajibu wa kumsaidia mlemavu, lakini bado elimu hiyo haijawafikia wananchi na ndio maana leo tunasema kwamba walemavu wananyanyaswa. Laiti ingelikuwa sisi sote basi tupo *conscious* kwenye masuala ya walemavu pasingetokea unyanyaswaji wa walemavu.

Mhe. Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu kumetokea watu fulani ambao wanadhalilisha watoto walemavu, hasa kwa kujua kwamba wale watoto walemavu ushahidi wao utakuwa pungufu na wao wanaweza wasije wakachukuliwa hatua hilo linatokea. Lakini pia hata katika yale maeneo ambayo wale wazee wa wale watoto walemavu wanapokwenda kushtaki, basi pia wale hawapati msaada wa kutosha. Sasa namuomba sana Mhe. Waziri, Mhe. Viwe amezungumza vizuri sana; zimeshatokea kesi watoto walemavu wamedhalilishwa, lakini watoto walemavu wanaume wamelawitiwa. Lakini sijui Wizara yake inachukua hatua gani katika masuala haya. Mhe. Waziri naomba hili uliangalie, kesi za watoto walemavu zije kwako wewe, wewe ndiye muhusika mkuu kwa watoto hawa.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwa kweli kwa kuzungumzia suala zima la mazingira. Mhe. Naibu Spika, suala la mazingira ni suala nyeti. Sasa hivi kwa upande wetu Zanzibar hata tukijua kwamba kisiwa chetu ni kidogo inahitaji kuchukuliwa umakini. Lakini nimeona hapa inajieleza kwamba kuna vipindi mbali mbali vinavyohusiana na masuala ya mazingira ambavyo vinatolewa na tunavisikia. Lakini mimi naona bado, na naomba sana, naishauri Wizara kuhusiana na suala hili la elimu ya mazingira. Elimu ya mazingira katika mitaala yetu ipo lakini haitoshelezi.

Kwa sababu elimu hii inapotolewa mara nyingi inatolewa *theoretically*. Mtoto wa mjini leo ukienda kumfundisha ukimwambia kwamba kuchimba mchanga ni kinyume cha sheria lakini asijue athari yake kwa sababu anakaa pengine maeneo ambayo hakuna uchimbaji wa mchanga, lakini kumbuka mtoto yule yule anaweza baadae akaenda kuishi katika maeneo mengine.

Ninachojaribu kusema kwamba hebu sasa hivi badala ya kusomesha tu madarasani, na nasema hivi Waziri kwa sababu wewe ndiye mwenye wataalamu wa kutosha wa masuala haya, washirikiane na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba hii elimu ya mazingira inayotolewa basi iwe elimu ambayo itakuwa inaonesha picha kamili ya matatizo ya mazingira katika maeneo yetu. Na sio tu kwamba kuna uchimbaji wa mchanga, kuna kukatwa miti, au kuna kufanyika jambo lolote ambalo litaharibu mazingira.

Mhe. Waziri nakuomba sana mkae katika mikakati yenu mhakikishe kwamba kuna ziara mbali mbali ambazo zinafanyika katika maskuli kuona kwamba watoto; hasa vijana wetu, kwa sababu ndio wao raia wa baadae waone kuna umuhimu gani wa kuyalinda mazingira yao.

Lakini Mhe. Naibu Spika, vile vile ninachotaka kusema kwamba katika elimu hizi ambazo zinatolewa je, mnafanya tathmini. Tathmini gani inafanyika ya kujua kweli elimu hizi zinaleta mafanikio. Tutizame *value for money*, isijekuwa elimu zinaletwa mradi zinarushwa lakini leo ukienda kulizungumza suala hili ukitoka ukienda kuuliza watu hawajui chochote kuhusu mazingira au elimu ambayo inatolewa lakini bado inakuwa haijawafikia wananchi.

Naomba sana Wizara yako ifanye kazi mbili; na hili naliomba katika Wizara yako katika masuala yote yakiwemo na ya walemavu. Tufanye tathmini ya kujua elimu ambayo tunaitoa inaleta manufaa gani. Kwa sababu kumekuwa na vipindi mbali mbali, kumekuwa na semina mbali mbali, tunaambiwa kwamba watu wamepewa elimu, lakini hatujui elimu ile imeleta manufaa gani katika nchi yetu. Nakuomba sana hilo lifanyiwe kazi. Tusi-*invest* pahala ambapo tunaona kwamba hapana mafanikio yoyote.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nafikiria suala la mazingira katika miji mipya. Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo katika upangaji wetu wa mambo yetu. Katika kupanga mara nyingi sana tunapanga lakini hatujitayarishi kwenye hiyo mipango. Nasema hivyo kwa sababu kwa mfano kama mji mpya ambao sasa hivi una ujenzi wa kasi mji wa Tunguu. Mhe. Waziri ukipita Tunguu unaweza kusikitika hakuna miti wala hakuna anayejali kuzungumzia suala la kupanda miti katika eneo lile. Eneo ambalo leo na kesho watu wengi watahamia. Mhe. Waziri sijui kama unafanya kazi na Wizara ya Ardhi katika masuala haya, lakini lina umuhimu mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, juzi juzi tulikuwa Dodoma, wengi tunaifahamu Dodoma namna ilivyokuwa. Dodoma ilikuwa ukipita njiani hakuna haiba, leo Dodoma wameanza kuzungumzia kuwa watakuwa na mvua nyingi sana kwa sababu ya miti. Kwa hiyo ukipanda miti uwezekano upo mkubwa wa kuwa na maji ya kutosha. Sasa sisi kwenye hilo tunazungumzia, lakini ukienda mipango ipo isipokuwa katika utendaji kwa kweli mipango inakuwa midogo. Suala la miji mipya inayozuka tuhakikishe kwamba kunatengenezwa *road map* ya kuwa na miti maalumu katika maeneo yale ili kuleta haiba ya miji yetu. Na hiyo kazi Mhe. Waziri ni kazi yenu kwa sababu mnacho kifungu cha kufanyia kazi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho mimi nataka kuzungumzia suala la madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, suala la madawa ya kulevya ni suala ambalo kila mmoja wetu anayesimama hapa analizungumzia kwa sababu ni jambo ambalo sasa hivi limekuwa kama la kawaida. Na inasikitisha kwa kweli hali ya Zanzibar tukijua hatua mbali mbali zimechukuliwa na Serikali lakini bado suala la dawa za kulevya kwa kweli halijapata ufumbuzi. Tunafahamu kwamba kuondosha kabisa haiwezekani, lakini kupunguza uwezekano huo upo. Mhe. Waziri jukumu hilo umepewa wewe.

Vile vile tunasikitika mimi nimeona katika ukurasa wa 23 nazungumzia suala zima la kesi za waliokamatwa na madawa ya kulevya kwa kuuza. Kesi hizi Mhe. Waziri naomba utwambie ni za lini. Kwa sababu kuna utaratibu

ambao unatumika kesi hizi kuziendeleza kwa muda mrefu mwisho kuuondoa ushahidi, na mwisho kuwaachia hawa watu. Na ndio maana kesi hizi zinakaa kwa muda mrefu kwa sababu hiyo. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri akija hapa atwambie ili na sisi tuweze kufanya kazi tuzikemee hizi taasisi zinazoshughulika na mambo hayo. Tuambie ukweli wa kesi hizi, kesi 21 lakini bado zinashughulikiwa. Ushahidi huo ambao unatafutwa ni ushahidi wa aina gani.

Mhe. Naibu Spika, mimi inanisikitisha vile vile kwamba bado Serikali haijatia nguvu katika masuala mazima ya kusaidia vijana wetu ambao wanataka kuacha madawa ya kulevya, lakini tunafahamu fika kwamba kuna ulazima wa Serikali kuwasaidia. Wamejikusanya wenyewe lakini bado wanategemea michango midogo midogo kutoka kwa watu binafsi au kutoka kwa wafadhili wadogo wadogo na hili haliwafikishi pahala. Mheshimiwa mmoja amesema hapa kwamba wanarudi tena na hiyo ndio kawaida. Mimi nataka kumwambia tu asione kwamba katupa pesa zake. Hiyo ni kawaida mara nyingi sana watumiaji wanapotaka kuacha wanarudi kwa sababu ya mazingira yale yale ambayo yanakuwa hayawasaidii katika kuacha tabia ile.

Sasa ningekuomba Mhe. Waziri katika hiyo *road map* ambayo inatayarishwa basi kuwepo na mikakati ya kuhakikisha kwamba Serikali inatoa fungu maalum la kusaidia vijana hawa ambao wanaacha madawa ya kulevya. Kama alivyosema Mhe. Asha wako wengine ni *very intelligent;* wana akili sana, mahodari na wana *skills* tofauti, lakini nguvu ile na vijana wale tunawaachia na mwisho wake tunawapoteza.

Mhe. Naibu Spika, namalizia kwa kumuuliza Mhe. Waziri nakumbuka kulikuwa na kituo ambacho kilikuwa kinasaidiwa kinataka kujengwa *Rehabilitation Centre* Tunguu. Kituo hichi nimekuwa nakiulizia mara nyingi sana sijui suala hilo limefikia wapi, na kama wamejitokeza wafadhili. Lakini mimi naamini kwamba pengine wafadhili bado hawajakuwa tayari. Lakini sisi kama Serikali tuna mpango gani wa kuanzisha, kwa sababu kilikuwa kimeshaanzwa na kimepangwa na eneo lipo na kila kitu, lakini tuna mpango gani wa kuhakikisha kwamba kile kituo sasa tukijenge ili vijana wetu waanze kutumia.

La mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, nataka kusema hivi kwamba Mhe. Asha alizungumza hilo kwamba wamepata barua kutoka *Sober House;* ya kuwa vijana chini ya miaka 18 wasichukuliwe. Mimi kwa uelewa wangu nimeweza kufahamu kwa nini. Tunafahamu hata kwenye majela yetu tunakatazwa watoto chini ya miaka 18 wasichukuliwe. Lakini basi Wizara yako Mhe. Waziri nakuomba hili sana kwa sababu tunao wengi, na ni bora tukianza kuwasaidia sasa wakiwa na umri mdogo kuliko kuwaachia mpaka wafikie umri wa kuanza kwenda kwenye *Sober House.* Wizara yako isaidie angalau basi iwe na *Juvenile Sober House* moja kwa watoto ambao wapo *underage,* ili iweze kukusanya vijana wetu kutoka Unguja na Pemba ambao tunaweza kuwaondosha katika mashaka hayo wakiwa na umri mdogo.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza tena Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri lakini nilikuwa naomba sana nijibiwe maswali yangu. Na ukinijibu basi nakuunga mkono kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tumepata wageni hapa wa Timu ya *Baraza la Wawakilishi Sports Club.* Wageni hawa wanatoka *Tanzania All Stars Football Club* wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Kitwana Manara, naomba asimame. Ahsante sana. Na wa pili Meneja wao Ndugu Salim Msabah, na wa mwisho Kocha Ndugu Abdalla Maulid. Karibuni sana.

TAARIFA

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, sisi wengine tumekuwa tukisikia tu majina haya kwa sababu ni wadogo kwa umri sana, na wengine tumekuwa tukiwasikia humu humu ndani ya michango ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Sasa ningeomba kidogo ungetupa wasifu wao maana tunasikia tu haya majina na mimi siwafahamu. Nitashukuru sana Mhe. Naibu Spika, kama utatusaidia kwa hilo, ni ombi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mahmoud Thabit Kombo sasa mimi nimeletewa majina nimesoma tu, kwa kweli siwafahamu kiundani sana. Sasa kama unajua hivyo wapo Ndugu Dau na Meneja wetu wa Timu kama anaweza kutoa maelezo zaidi tutampa nafasi. Kwa hiyo Meneja kama anaweza kutoa maelezo toa maelezo kwa dakika mbili tu.

Ndugu Salim Msabah: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa kutaka kujua ujio wa wageni wetu hawa na wasifu wao. Lakini niseme tu kwamba ndugu yetu Bwana Kitwana Manara ni mchezaji ambaye sote tunamfahamu, ni mchezaji mahiri, ni wa kina Mhe. Mwinyihaji Makame enzi zao hizo, kina Mhe. Suleiman Othman Nyanga, ambaye alicheza mpira pamoja na Mhe. Nyanga Bwana Kitwana Manara. Lakini alikuwa ni mchezaji maarufu sana katika kufunga magoli ya kichwa na alichezea Timu ya Taifa ya Tanzania, alichezea timu ya *Dar es Salaam Young Africans,* na alicheza mchezo ambao siku ambayo mzee wetu Mhe. Abeid Amani Karume uwanja ule wa Karume ulipobadilishwa jina na kuitwa jina la *Karume Stadium.* Yeye alikuwepo uwanjani akiwemo Mhe. Nyanga, akiwemo mzee wetu Mgeni Mwalimu.

Kwa hiyo ushahidi huo upo na picha ambazo amekuja nazo zingeonesha siku hiyo ya mchezo huo. Kwa hiyo ni mchezaji mahiri, ni mchezaji ambaye ameleta historia katika nchi yetu hii ya Tanzania. Nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Sawa tunakushukuru. Nadhani Wajumbe mmeridhika na maelezo hayo tunaendelea na michango yetu tunamalizia wachangiaji watatu.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi sina budi kuanza kumshukuru *Allah Subhanahu Wataala* na kumtakia rehma Mtume wetu Muhammad (SAW), kwa uwezo wake *Allah* kuweza kunipa uwezo asubuhi hii kusimama na mimi kuweza kutoa mchango wangu wa hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nianze ukurasa wa 8 kwenye kifungu cha 3 katika malengo ya Mradi wa Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Mhe. Naibu Spika, Wizara imejipanga katika mambo manne kuyatekeleza na wamo katika kuyatekeleza mambo hayo, lakini nataka nizungumze katika kidoto cha pili, tatu na cha nne ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu.

Mhe. Naibu Spika, kidoto cha pili kinasema "kutayarisha mkakati wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kusaidia utekelezaji wake".

La tatu, "kuimarisha muundo wa taasisi kwa ajili ya kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabia nchi".

La nne, kukuza kiwango na upatikanaji wa taarifa na uelewa juu ya athari na mabadiliko na mikakati ya kukabiliana nayo miongoni mwa jamii na taasisi za serikali.

Mhe. Naibu Spika, karne zetu hizi tulizonazo, suala la mabadiliko ya tabia ya nchi si suala geni, huko nyuma taarifa hizi zilikuwa hazipo, lakini kila ulimwengu ukikweza, kuna mambo mbali mbali yanajitokeza, tukiambiwa mazingira haya ya mabadiliko ya tabia ya nchi, nchi ni nini? Nchi ni watu. Kwa hivyo, watu ndio wanaosababisha mabadiliko haya. Hivyo, binadamu tumejisahau, wapi tunatoka, wapi tupo, wapi tunakwenda. Tumeifanya dunia kama kwamba ndio pahala pa kuishi milele.

Kufikia katika hatua hizo basi hii dunia ina yule aliyeimiliki, aliyeiumba na akaweka mazingira mbali mbali kwa ajili ya huyu mwanadamu apite katika njia. Lakini kwa kujisahau kwetu, ndio tunaona kwamba mabadiliko mbali mbali yasiyotarajiwa tunayo katika ulimwengu wetu huu wa leo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kusema hivyo, ninapenda uniruhusu kidogo ninukuu maneno matukufu ya huyu muumba wa ulimwengu. Amesema hivi, baada ya *"Audhubillahi minashaitwani rajiym, walaa talquu aydiykum ilaattahluka"* maana yake nini? Wala musijiingize kwa mikono yenu katika maangamizi na tunashuhudia bado tupo hapa hapa duniani, tuna maeneo tulikuwa tunafanya kilimo, hivi sasa hatulimi tena, tuna maeneo walikuwa wanaishi watu, hivi sasa hawaishi tena, tuna maeneo ilikuwa tunafanya kilimo cha juu, hivi sasa hamulimikii tena, jua linakuwa ni kali, maji ya chumvi yanavamia na mambo mengine mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, haya hayakuchumwa na mtu mwengine, isipokuwa ni sisi mwanadamu kutokana na mikono yetu. Kwa hivyo, tabia hizi za mabadiliko wachangiaji wakubwa ni sisi wanadamu. Ili tuweze kuyadhibiti haya Mhe. Waziri, humu katika kitabu chake ameeleza kwamba wanatoa elimu kwa jamii na wadau mbali mbali na nakubaliano nao wote waliosisitiza kitu elimu.

Mhe. Naibu Spika, kitu elimu ni muhimu mno kabisa katika mambo mbali mbali ili watu waweze kupata uelewa na ufahamu mzuri na kuweza kuona kwamba huku tunakoelekea kwa kweli hatotuletea faraja wala tija kwa kizazi hichi kilichopo na kizazi chetu kinachokuja. Kwa hivyo, mabadiliko haya ndio yanaendelea na huu ni muonja, Mwenyezi Mungu anatuonja. Kwa hivyo, tuone kwamba tumemkosa Muumba. Hivyo, kwa hali yoyote tuna haki na wajibu wa kurudi kwake ili tuweze kuondokana na suala hili kubwa ambalo nchi yetu limo katika hali mbaya.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninasema hili ni tatizo sugu, ni tatizo moja baya sana ambalo kila miaka ikiendelea, sio kama linarudi, linaongezeka. Hivyo, mabadiliko ya tabia ya nchi mimi ninasema kwamba nchi ni sisi, watu ndio watu. Kwa hivyo, ni lazima tuone kwamba ili tuweze kuishi vizuri ni kujizuia mikono yetu katika mambo mbali mbali ambayo Mwenyezi Mungu hayaridhi. Tutapata usalama na tutatokana na hili janga ambalo Mwenyezi Mungu ametuletea. Hilo ni wazo langu moja Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, jengine nazungumzia na wengi katika wizara hii tumeona sana ndugu zetu watu wenye ulemavu na mimi nichangie kidogo katika suala hili la watu wenye ulemavu. Ni kweli hakuna nchi iliyokuwa haina watu wenye ulemavu, kwa sababu kwa mawazo yangu ninahisi kwamba ulemavu unapatikana katika nyanja mbili; nyanja ya kwanza ni ya kuzaliwa, wapo wanaozaliwa wakawa tayari wamezaliwa na ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, lakini nyanja ya pili, ni kutokana na mwenendo wa mwanadamu katika harakati zake. Harakati hizi zinaweza mwanadamu kumuingiza katika masuala ya ulemavu, ijapokuwa kwamba alizaliwa hana ulemavu. Hivyo, ninahisi kwamba nyanja mbili hizi, mwanadamu yeyote aliyepo katika ulimwengu huu mpaka wa kufikia muda wake wa kufa hakupata ulemavu, amshukuru aliyemuumba sana.

Mhe. Naibu Spika, lakini tuseme kwamba lazima katika mwanadamu aliyeopo katika ulimwengu huu, nafasi ya pili ya kupata ulemavu ni baada ya kwishakuzaliwa kuwa hayupo mlemavu. Sasa hawa wenzetu ambao tayari wameshakuwa walemavu. Kwa hivyo, bado tunaiomba sana serikali iwasimamie inavyopasa watu hawa wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu huyu aliyekuwa ni mtihani kwetu sisi ambao hatuna ulemavu. Hivyo, maisha yao wanatuangalia sisi, kama sisi tunaanza kuwafanya kwamba wana baadhi tu wa ubinadamu, si binadamu kamili, hii itakuwa ni kosa. Juzi hapa Mhe. Waziri alipokuwa anajibu maswali, alitwambia kwamba idara yake hii inafanya kutoa tathmini ya Zanzibar nzima watu wenye ulemavu wa aina mbali mbali, akatwambia hili suala bado halijakamilika, lakini pia, mimi binafsi ninamuomba ni vyema suala hili likachukuliwa hatua likaweza kukamilika, likajulikana aina zote za ulemavu tulizonazo hapa Zanzibar na idadi yao ili pengine kuna wengine tunawaona si walemavu, kumbe wamo katika hesabu ya ulemavu, wanakosa haki zao mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, hivyo, ni vyema tunaiomba sana wizara hii walete hiyo idadi yao na aina zao ili pengine hawa watu ambao katika vijiji vyetu wanaonekana si walemavu, kumbe wana haki zao nyingi za kuwa wao ni walemavu zikaanza kufuatiliwa, lakini nimuombe sana Mhe. Waziri anapofanya ziara zake katika majimbo yetu, basi sisi viongozi wenzake atushirikishe ili tuone kwamba usimamizi wake unaeleweka na unaonekana.

Mhe. Naibu Spika, hivyo, baadhi yetu hatujui hizi idara zake anapokuja katika majimbo yetu, ili kuja kuwatafuta hawa watu wenye ulemavu tukaweza kushirikiana nao. Hivyo, Mhe. Waziri hili popote utakapofanya matembezi au ziara katika majimbo yetu, ninakuomba sana ushirikiane na Wawakilishi wenzangu ili tuweze kuwatoa ambao wamo katika maeneo yetu, kwa sababu ninaamini mimi baadhi ya watu wenye ulemavu hadi muda huu tulionao wamefungiwa katika majumba yao, lakini unapokuja katika maeneo yetu tukashirikiana, hawa watu basi pia tutaweza kuwafichua na kuweza kuwaorodhesha ili waweze kupata huduma kama walemavu wengine.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri katika ujumbe wenu wa mwaka 2013/2014 uliosema kwamba "Ondoa vikwazo, weka fursa ili kuwa na jamii jumuishi kwa wote". Huu ujumbe ni ujumbe mmoja mzuri sana, lakini nilikuwa namuomba Mhe. Waziri anieleze utakapokuja kusimama hapa ujumbe huu ulichukuliwa hatua kiasi gani?

Mhe. Naibu Spika, na hii jamii jumuishi iliweza kupewa taaluma kiasi gani ili kutokana na hawa watu wanaowazuia walemavu kuwaona kama sio sawa na binadamu wengine. Hasa huu ujumbe mimi ningelimuomba Mhe.Waziri sana usibabaike katika kumbukumbu zetu za vitabu, ni vyema jamii zetu zikaelimishwa ili tutoke huko tulikokuwa, tutakuwa hatuwatendei haki watu hawa.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba walemavu hawathamini, hawajaliwi, hawapati elimu, hawapati taaluma nyengine mbali mbali, kwa maana hiyo, kumdhalilisha mlemavu, wewe umejipangaje, wewe umejiona vipi umekamilika, hujui wakati gani, muda gani, saa gani Mwenyezi Mungu anaweza akakuchukulia hatua na wewe. Kwa hivyo, nakuombeni sana wananchi wa majimbo yote tusiwatendee vibaya, tusiwanyanyapae walemavu wetu. Hili ni kosa na ni kosa moja kubwa, kwa sababu wewe hujijui wakati gani utakuwa mlemavu mtarajiwa, ninakuombeni sana Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na muda wako, niingie katika suala zima la mazingira. Ni kweli tuna tatizo la mazingira, nchi yetu imeingiwa na tabia ya mabadiliko ya nchi tuliyoizungumza mwanzo, maji ya bahari yamevamia nchi, maeneo mbali mbali, tumetajiwa hapa na Waheshimiwa mbali mbali, kuna visiwa mbali mbali kule Pemba tayari maji ya bahari yameshahamia, baada ya kuwa nchi kavu hivi sasa imekuwa ni pwani.

Mhe. Naibu Spika, lakini kutokana na mazingira haya Mhe. Waziri amesema kwenye kitabu chake kwamba kuna kukuza uelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine.

Mhe. Naibu Spika, jambo lolote hatutopiga hatua kama haikupatikana elimu, kama watu hawafanyiwi elimu, hawapewi taaluma, hawaelimishwi, tutakuja kila siku tukipiga kelele hapa, nchi inakwenda, sisi tunasema hapa, lakini hapana linalokuwa.

Mhe. Naibu Spika, jambo lolote kwanza ni elimu, elimu ndio muhimu. Mwenyezi Mungu alipoumba huu ulimwengu aliviumba vitu vyote, mwanadamu alimtangulizia kama ni hazina kwake, akamuwekea miti, milima, tambarare, mabonde ili mwanadamu atakapokuja hapa akute cha kutumia kipo na huyu mwanadamu kuja kapewa elimu namna ya kuvitumia hivi vitu ili maisha yake yasiwe maisha ya hahe hohe, yawe maisha ambayo yanaweza kumuendesha katika kumudu maisha haya.

Mhe. Naibu Spika, lakini mwanadamu sisi baada ya kufika katika ulimwengu, haya mazingira tumechafua na tukisema kitu mazingira, huu ukosaji wa elimu ni suala zima la mazingira. Kwanza tuwe na mazingira sisi wenyewe, tupate elimu, tuwafundishe watoto wetu waweze kufahamu. Sasa tulipoyakosa hayo na Mwenyezi Mungu ameshatuwekea mambo mbali mbali, lakini na Mwenyezi Mungu hakutuacha tu, alitwambia, alisema vipi, naomba uniruhusu niseme Mwenyezi Mungu kasema "*walaa tufsiduu fil-ardhi ba3da islaahiha*" Wala musiiharibu ardhi baada ya kwishakutengenezwa, ardhi Mwenyezi Mungu kishaitandika na kaitengeneza, sisi wanadamu sasa tunaanza kuiharibu.

Mhe. Naibu Spika, sasa tunapoiharibu ardhi, ndio haya yanayotufika sasa mazingira yetu yanachafuka.

Mhe. Naibu Spika: Malizia.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, tatizo hili tusimuachie Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na hizi wizara chache alizozitaja katika kitabu chake, hili ni suala la nchi. Kila nchi nzima, kila wizara inahusika na suala hili la mazingira. Kwa hivyo, ili kuweza kulichukua suala hili na kuweza kutoka hapa tulipo, sasa basi naiomba sana serikali nzima tulifanyie kazi suala zima la mazingira.

Mhe. Naibu Spika, tuna miradi mbali mbali wenzetu wameanzisha, tuna miradi ya barabara, tuna mashimo hivi sasa mengi tu, wakandarasi wanaochimba vifusi hawarejeshi lile dongo walilolitoa wala madongo wanayoyatoa hawapeleki katika yale mashimbo ambayo yapo, ule pia ni jumla ya uchafuzi, lakini pia, tumejenga, tunapiga tanu, tunafanya mambo mengine, mikoko yote tumeikata, maji ya chumvi yanazidi kuja juu. Haya pia ni uchafuzi wa mazingira.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeliwaombeni sana wananchi hasa wale wananchi walio kando kando ya bahari, vizazi vyetu vinavyokuja vinahitaji kuishi, vinahitaji nyumba, kuna wale walio na uwezo wa kujenga nyumba za tofali, nyumba za mawe, lakini kuna wale walio na uwezo wa kujenga nyumba za miti. Sasa hii miti kama hatukuimarisha, kama hatukuwaanzisha vijana wetu wadogo wadogo wakaanza kuotesha ile miti ya bahari, hatma yake huko mbele

watakuja kukosa hata wale waliokuwa hawana uwezo wa kujenga majumba ya matofali, kukosa ile miti ya kujengea nyumba zao.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, muda wako umekwisha, malizia.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Hivyo, ningeliomba sana wananchi tulio katika maeneo yale hasa walimu wa vyuo vya madrassa hivi kuweza kuwashajihisha hawa vijana wao wadogo wadogo ili kuweza kupanda miti ya mikoko ili kuweza kuyadhibiti mazingira yao, kwa sababu wao ni wadau wakubwa zaidi waliopo katika maeneo yale.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Ali Hassan, jali muda.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuichangia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichangie katika nafasi hii ukurasa wa 14 kuhusu mazingira. Kwa kweli hali ya mazingira nchini kwetu yamekuwa ni ya duni sana na hasa ukitizama utupaji wa takataka ovyo unaoendelea. Hivi sasa taka zote za mji wa Unguja zinatupwa Jumbi ambalo ni Jimbo la Koani.

Mhe. Naibu Spika, ukienda katika jaa hilo hivi sasa liko katika mazingira mabaya sana hasa uchafu umezidi, ingawa zinatupwa taka ni chafu, lakini limezidi kuwa chafu sana.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia taka hizo zimekuwa ni nyingi na hazishughulikiwi kupigwa dawa kwa wakati ama kuchomwa. Hivi karibuni nilitembelea sehemu ile katika jaa la taka nilizikuta taka hizo zina harufu kali sana, nikahakikisha kwamba kwa kweli hakuna muda ambao zinapitiwa na taka hizo angalau kupigwa dawa kwa wakati, najua kwamba haziwezi kuchomwa moto kutokana na mvua nyingi, lakini angalau zingekuwa zinapitiwa kupigwa dawa ili kupunguza nzi katika jaa lile.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri akija anieleze ni mara ngapi katika kila mwezi zinatoka dawa za kinga kupewa wananchi ambao wanakaa karibu na jaa lile. Vile vile, Mhe. Waziri, anihakikishie ni mara ngapi katika mwezi mmoja linapigwa dawa jaa lile kudhibiti nzi wengi ambao wanasambaa katika mji ule jirani na shimo lile la taka, hasa ukizingatia watoto wadogo ni wengi sana na watoto wadogo huwa wanakula chochote katika michezo yao, hasa vikitungwa na nzi, basi ni hatari sana kwa watoto wetu, hasa vijana wetu wa Jimbo la Koani nataka wafanane afya zao kama alivyo yeye mwenyewe Mhe. Waziri. Wasinyonyeke kutokana na hali ya maradhi. Si hivyo, nitamchukulia hatua Mhe. Waziri, hata nikaweza kusema kama hashughulikii, naweza kutoa shilingi yangu katika kuchangia mswada wake.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikichangia ukurasa wa 17, naomba kujua tulichanga fedha nyingi sana za walemavu tulipokwenda katika hoteli ya *Zanzibar Beach Resort*. Kwa kweli kulitoka mchango mwingi sana pale ambazo zilitimia milioni 160. Naomba Mhe. Waziri akija anifahamishe fedha hizo zimetumika vipi ili tujuwe fedha zile kama zimetumika zilivyopaswa ama vipi? Kwa sababu hadi leo sijapata kujua fedha zile zimetumikaje kuhusu suala la walemavu.

Mhe. Naibu Spika, nikimalizia hapo nichangie ukurasa wa 21 kuhusu tatizo la *Sober house*. Kwa kweli tuna vijana wengi sana ambao wameathirika kwa madawa ya kulevya, lakini wakati mwingi sana kila tukitembea katika *Sober house*, huwa tunatembelea *Sober house* za hapa Mjini Unguja au Pemba au tunasema Zanzibar, lakini ni mjini.

Mhe. Naibu Spika, lakini hatuelewi kwamba watu wengi wanaoathirika na madawa haya ni kutoka katika Mkoa ya Mashamba, tunahakikisha kwamba bangi nyingi zinapandwa shamba, tuelewe wazi kwamba vijana wetu wakitaka kuhakikisha bangi yao kama ni nzuri kuja nayo mjini, basi ni lazima wanaanza kuonja wao, wakionja hizo bangi, ndio utakuta vijana wengi wanaathirika katika mikoa yetu na hivi sasa katika mikoa yetu ni jambo duni sana kuikuta *Sober house* imejengwa katika jimbo ama wilaya.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri akija aniambie kuwa ni lini katika majimbo yetu kila jimbo tutahakikisha kwamba kuna nyumba ya kulea hawa vijana walioathirika na madawa ili kuhakikisha vijana wetu wako salama. Si hivyo, inawezekana nikatoa shilingi yangu katika mswada wake ili mswada wake usipite na kuweza kutumika katika fedha za bajeti ya mwaka huu.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri atakapofika hapa anihakikishie ni lini ile nyumba ambayo inaanza kujengwa Kidimni kwa ajili ya wagonjwa ambayo imekwishawekwa msingi tu wa ukuta, ni lini utamalizika ukuta huo ili nijuwe ni mwaka gani vijana wetu watakwenda pale kulelewa kwa ajili ya kuhakikisha usalama wao.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo, machache kutokana na muda, naomba niishie hapo na naiondolea shilingi wizara hii mpaka pale atakaponihakikishia Mhe. Waziri mambo hayo ambayo nilimchangia. Hivi sasa ninaikubali kwa asilimia 5 na akinihakikishia nitaikubali kwa asilimia mia. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi nitumie fursa hii kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai.Pili, nikushukuru wewe kwa kunipatia hii nafasi ya kuweza kutoa mawazo yangu katika hii hoja iliopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuingia katika hoja, naomba moja kwa moja niwashukuru wanachama wa Chama cha Wananchi *CUF* wa Wilaya ya Chake Chake kwa kuendelea kunipa ridhaa yao kwa kunichagua kuwa Katibu wao wa Wilaya kwa Chama cha Wananchi *CUF*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ninachowaahidi wanachama wa Wilaya ya Chake Chake wa *CUF* ni kuwapatia utumishi ulio makini, mahiri, adilifu na wenye kutukuka mno. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nianze moja kwa moja katika hoja iliopo mbele yetu kwenye ukurasa wa 14, Ibara ya 33. Mhe. Waziri, hapa amezungumzia habari ya mazingira. Suala la mazingira kwa sasa sio suala la mchezo na nchi yoyote sasa hivi hasa hizi nchi zilioko katika dunia ya tatu, inatakiwa serikali zetu ziwe makini sana katika kulinda, kutunza na kuyaenzi mazingira.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kwamba kila mwaka tunaambiwa kuwa nchi yetu inatoa kipaumbele katika masuala ya mazingira, jambo ambalo sio kweli kabisa. Kwanza serikali yetu inatoa bajeti finyu mno katika Idara hii ya Mazingira na inadharau mambo ya mazingira.

Mhe. Naibu Spika, idara hii ni muhimu sana, katika kupambana na janga kubwa lililoukabili ulimwengu la mabadiliko ya tabia nchi. Kwa mnasaba huo ni kwamba suala la mazingira hivi sasa ni *International issue, w*atu wanatembela ulimwenguni, lakini wakiingia katika nchi wanakuja kuhoji mambo ya mazingira, inasikitisha sana serikali yetu hii ya *GNU*, ilivyokuwa haikutoa kipaumbele katika masuala ya mazingira katika mambo yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, kwanza tuangalia ile ofisi ya ile Idara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais eeh! inasikitisha sana, yaani kumweka Mkurugenzi katika ofisi ile akapata wazungu kuja kumtembelea katika ofisi ile, mimi yule kijana napenda nimpongeze sana jinsi alivyokuwa mstaamilivu, maana inatia haya ile ofisi, wachilia mbali kumleta mgeni kutoka nje, basi kumchukua Meya tu wa huu mji ukasema aende akakutembelee pale ofisini kwake inakuwa tatizo sana.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi naiomba sana serikali, kwanza ithamini hii Idara ya Mazingira angalau kwa kuipatia ile idara ofisi ya kisasa kabisa. Sasa wenzetu wanaingia katika mitandao kuona kwamba nchi kadhaa iliopo katika *continent* kadhaa imedhibiti mabadiliko ya tabia nchi katika misingi hii na hii. Sasa dunia tunayo katika kiganja, lakini Mkurugenzi wetu wa Mazingira hapa Zanzibar ile ofisi yake hana pakuweka vifaa vya mambo hayo ambayo anaweza kuona mambo mengi yanayopita katika ulimwengu ni tatizo, kama atapata ugeni kutoka nchi kama vile Uturuki, kwa sababu wale ni warefu, basi unaweza ukawakata kichwa kutokana na lile feni lilivyokuwa chini, inasikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, Mhe. Waziri, kama ikiwa tatizo wewe huna hela, basi omba hela ili sisi hapa tukupatie uweze kuwapatia ofisi hawa idara, ikiwa huna uwezo wa kukodi, basi tafuta ardhi, uombe hela hapa, basi wajengewe kama wanavyoomba wenzao. Hebu waangalie Wizara ya Sheria na Katiba, sasa hivi pale walipo na wao hawana mabadiliko ya tabia ya nchi wale, wana Mahakama tu na hayo mambo mengine, wamepata jengo zuri kama

lile. Je, wewe ambaye unatakiwa uwapatie watu wa mazingira ili waweze kukaa na kufanyakazi kitaalamu. Katika kijiofisi kama kile haifanyiki kazi, nawapa pole sana Idara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, halafu jinsi serikali yetu ilivyokuwa haiko makini katika ku-*recover environment degradation* ambayo waliyoifanya wao wenyewe, inasikitisha sana, kama ukienda pale uwanja wa ndege Kisauni, pana mahandaki pale makubwa sana yaliyosababishwa na serikali kwa kupitia wizara yake hii ya Miundombinu na Mawasiliano, wameharibu mazingira vibaya sana, wameharibu mazingira pahala pabaya, kwa sababu ni karibu na uwanja wa ndege na ile ni *Karume International Airport*, karibu na maeneo yale ya *landing* ya mwanzo kule Kisauni. Kwa hivyo, jirani na pale unakuta kuna mahandaki. Kwa hivyo, inapotua ndege ni tatizo, ina-*force* kubwa, unaweza kuja ku-*cause accident* ya madege pale, ikaja kuwa tatizo.

Mhe. Naibu Spika, unapoleta madege makubwa pale, halafu ukayatua katika eneo lile la uwanja wetu wa ndege, huku pembezoni kuna mashimo kama yale, ile *force* ya kutulia, inaweza kuwa *exhausted* mpaka ikafika kwenye yale mashimo, matokeo yake tukaja kupata *crack* kubwa sana pale, mimi sio mtaalamu katika masuala haya ya jiolojia, lakini najua tu mambo ya *soil chemistry*. Kwa hivyo, nadhani patakuwa ni tatizo kubwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, muangalie nyinyi wataalamu katika masuala haya, yale mahandaki yaliopo pale hayatoathiri baadaye mkasababisha *accident* madege kutokana na uharibifu wa mazingira yale, kama yatasababisha, naomba serikali iwe makini na ikayaangalie tena yale, ili wayaweke katika hali nzuri yasije yakatuharibia ule uwanja wetu wa Kimataifa ambao kwa sasa hata *Announcement board* haipo pale.

Mhe. Naibu Spika, niendelee katika suala zima la jinsi serikali yetu ilivyokuwa haiko makini. Mazingira tukiyatunza yatatuenzi, lakini mazingira tukiyaharibu yatakuwa adui yetu, serikali yetu haitunzi mazingira, hebu tuangalie pale katika kijiji changu cha Wawi jimboni kwangu, ninapiga kelele mpaka sasa kifua kinaniuma, jinsi kile Kiwanda cha Makonyo kinavyomimina moshi na kuwaathiri jamaa zangu wa mji wa chini mpaka kufikia sehemu za Magome na mpaka Mikunguni. Mimi nimepita pale leo moshi uliopo hatari. Jamani mtatuuwa.

Mhe. Naibu Spika, nilitoa wazi mimi kwamba lile bomba lipelewe juu, ili ule moshi uwe huko huko juu kwa juu, nimeonekana mpumbavu, sasa kama hamna uwezo huo, serikali kama haina uwezo huo, basi kiondoshwe kile kiwanda katika ule mji na kipelekwe Makaani huko ili moshi upotee baharini, sio kuwaathiri wale watu wa pale Wawi wanaathirika.

Mhe. Naibu Spika, juzi niliuliza nikaambiwa moshi ule hauna *carbon*, lakini baada ya *Feasibility Study*, tumeona kwamba ule moshi una *carbon* na *carbon* inapoingia katika damu inachanganyika, kwenye damu kuna *haemoglobin*, *haemoglobin* ina-*affinity with oxygen*, sasa unapoweza kuingiza pale unaweza kukuta ina-*react* na *carbondioxide*, ina-*react* na ile *haemoglobin* kukupa *carboxyhaemoglobin* ambazo ni *toxic compound*, ina-*cause powerful destruction* kwenye *body cells* na kuweza kusababisha *cancer*.

Mhe. Naibu Spika, sasa nyinyi serikali naomba mtusikilize kwamba kuna wasi wasi mkatupatia *cancer*, watu wengi wa Wawi kutokana na kile kiwanda chenu pale. Mnaona hatujaathirika hivi sasa, lakini athari inakuja kidogo kidogo, lakini moshi ule utatuathiri sisi watu wa Wawi kwa kutupatia ma-*cancer* na utawaathiri serikali baadaye kwa sababu tutakuwa hatuwezi kulima, hatuwezi kuzalisha mali ili mkapata kodi ya kuendesha nchi, msione kwamba tunasema kwa ajili ya afya yetu tu, tunasema hata kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, tukiwa wabovu sisi watu wa Wawi, nyinyi hamtapata kodi na mkiwa hamtapata kodi, basi hataweza kuendesha nchi hii, msiwe wakaidi serikali, kiondosheni kiwanda kile au lile bomba lipelekeni juu, mtatuuwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nilipoangalia katika Ibara ya 33(4) kinasema; "kukuza uelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine wa mazingira". Hebu tuelezeeni nyinyi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kama mnatoa elimu, mnatoa elimu kiasi gani kwa wakulima, hasa wakulima wa Mwambe kwao Mhe. Hija Hassan, wakulima wa Micheweni kwao Mhe. Subeit Khamis, wakulima wa Vitongoji kwangu mimi pale. Je, mnatoa elimu ipi?

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kama mnatoa elimu ya mazingira hivi, sasa wakulima wanaendelea kufanya kilimo kinaitwa *Monoculture*. Wataalamu wa kilimo waliomo humu, nafikiri Waziri wa Kilimo na Maliasili yumo humu

anajua habari ya *Monoculture* ni kulima zao la aina moja katika ardhi hiyo hiyo mwaka nenda mwaka rudi, ukilima zao la aina moja tu katika ardhi hiyo hiyo, basi unasababisha uharibifu wa mazingira kwamba panapotea mbolea pale.

Mhe. Naibu Spika, sasa mmetoa elimu kiasi gani kuwaambia wakulima kwamba walime kilimo cha aina gani kisichoathiri mazingira? Aidha, kwenye suala zima la wafugaji wetu, mmetowa elimu gani kwa wafugaji wasifanye *overgrazing*, je, mmetoa elimu gani kwa wakulima tena kwa ajili ya kuchoma moto? Mmetoa elimu gani wasichome moto na wale wa kule kwetu Micheweni kazi yao kilimo chao wao wanawasha moto wakishauwa miti ndio wanapanda? Je, mmetoa elimu ya namna hiyo kwamba wasitumie moto katika kilimo wanaharibu mazingira?

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nadhani tusaidieni katika hili, ili tuepukane na mabadiliko ya tabia nchi, pamoja na kupata matatizo ya kiafya, kwa sababu mimi nilipokwenda katika Hospitali hii ya Mnazi Mmoja, nikapita na katika mji wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mji Mkongwe, *sewage system* yote inaingia moja kwa moja kwenye bahari, hamuwezi kujua ile *Environmental pollution*, ile *Aquatic environmental pollution* inayotokea mule inawaathiri kiasi gani watu? Yale maji taka yanayotoka Hospitali ni *toxic*, wanakula samaki na sisi tunakula samaki, tunapata matatizo huko mbele.

Mhe. Naibu Spika, nadhani badala ya kuyawachia yale maji, tunaomba *for longer project* katika mambo ya mazingira, mfanye mambo ya kuyatibu ndio muyawachie baharini, musiyawachie moja kwa moja, yatatudhuru *indirect*, watakula samaki na sisi tutawala samaki tudhurike, *there is an interdependence of food between living organism* wanaita *food chain*.

Mhe. Naibu Spika, naomba musiyaingize mule, badala yake muya-*treat* kwanza, halafu ndio muyawachie kama ambavyo mlijaribu kufanya yale maji ya jimboni kwa Mhe. Omar Ali Shehe pale Chake Chake, Msingi na Mchungwani mkayafanyia *treatment*, kwa nini ya Mji Mkongwe mshindwe kuyafanyia? Sisi tunapenda samaki sana na watalii vile vile, ananikumbusha Mhe. Mahmoud pale.

Mhe. Naibu Spika, sasa nakwenda katika Idara ya Watu wenye Ulemavu, Idara hii ni muhimu sana kwa nchi, hii ndio inayoondoa tabaka baina ya watu bila ya kujali maumbile ya mtu kama ni mlemavu au ni mzima. Sasa idara ya watu wenye ulemavu ina kazi kubwa, lakini nasikitika kwamba serikali yetu haiko *serious* katika suala zima la kuondosha hii, miundombinu ilioko sio rafiki hata kidogo kwa watu wenye ulemavu, ni tatizo. Kanuni na sheria za nchi haziwapi raha walemavu.

Mhe. Naibu Spika, juzi nilitoa takwimu ndogo tu hapa, nikaliangalia Baraza zima la hapa kwetu Zanzibar, sijaona mlemavu hata mmoja na sidhani kama Katiba yetu inaelezea ukiachilia mbali nafasi za kwenye vyama kama walivyofanya baadhi ya vyama kuleta walemavu, lakini sheria haijaeleza hasa kwamba kuwepo na *special percentage* ya walemavu katika vyombo vya kutunga sheria. Hawa walemavu wana uwezo sana, juzi tuliambiwa wameshasoma sana, kuna wengine wana *PhD* na kuna wengine wana elimu mbali mbali, kwa nini tusiwape fursa na wao wakaingia kwa nafasi zao, hawawezi kupambana na watu kwenye majimbo. Msiviite viti maalum, wawekeni kwenye viti vya upendeleo vya walemavu wapewe hasa viti vya upendeleo vya walemavu katika Baraza, viti vya upendeleo vya uwaziri katika Baraza la Mawaziri, japo mmoja na yeye awemo. Hii inasikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa huko mashuleni, ukiwache zile shule za mchanganyiko sijui za nini? Watoto wenye ulemavu wanapata tabu, inasikitisha kwamba katika Wilaya nzima ya Chake Chake, ukiacha ile shule ya Michakaeni katika Jimbo la Mhe. Omar Ali Shehe, hizo za huko vijijini watoto wenye ulemavu ni tatizo, hivi juzi kulikuwa na mtoto anataka kufanya mtihani, hana *brain* na wakasema basi atasomewa, nikashangaa sana, yaani wanataka kunifanyia, mimi mitihani. Mungu bariki tena nashukuru Idara ya Elimu pale Chake Chake wakampatia zile mashine na akaweza kufanya.

Mhe. Naibu Spika, mimi naiomba serikali Mhe. Waziri muwawezesha hawa, jamani tunashindwa kuweka *brain machine* katika shule angalau chumba kimoja katika kila shule, tunashindwa hili. Mimi nadhani tujitahidi kuwasaidia hawa wenzetu watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, halafu...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe malizia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, nataka nizitumie hizi dakika tatu zilizobakia kwa kuiomba serikali ione kwamba walemavu ni watu wenye bidii. Kule Pemba kuna timu ya mpira ya walemavu. Je, serikali inajua hilo kama iko timu ya mpira ya walemavu kule Pemba. Kama serikali inajua kuwa timu ya walemavu ipo, je, imesaidia nini serikali au ndio wapo wapo tu, huko ni kuwaenzi au kuwadharau wamefanya juhudi, lakini hamziendelezi, hilo ni tatizo Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, mimi naiomba serikali hasa kwa kupitia Idara ya Michezo iende Pemba ikaangalie ile timu ya walemavu na ikiwezekana iwaendeleze, ione kwamba kuna mashindano ya walemavu Bara kule iwashirikishe na iwaingize. Timu za walemavu sasa hivi zinashiriki mpaka kwenye mashindano haya ya *Olympic*. Sisi naamini tukiwaendeleza wale wataweza, maana juzi niliwatembelea pale, kwa walivyo na moyo watafanya vizuri tu.

Mhe. Naibu Spika, mfuko aliouzungumzia Mhe. Mussa Ali, sijui ni ule au ni upi? Lakini nilikuwa nataka nijuwe matumizi ya mfuko ule, karibu shilingi milioni 200 zilizokuwepo pale zimetumika vipi? Hebu tuelezeni kidogo, mfuko ule wa watu wenye ulemavu mmeutumiaje?

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kuna taarifa kwamba haki yao ya kibajeti kule Pemba haiwafikii walengwa, hawa walemavu haiwafikii ni kwamba haki hiyo ya walemavu inakwenda moja kwa moja kwa Afisa Mdhamini, mfuko wa walemavu unakwenda katika mfuko wa Afisa Mdhamini Pemba pale, tena anaweza kuzitumia katika shughuli nyengine, huku walemavu wakiachiwa hawana jambo. Hilo ni tatizo na tunaomba ule mfuko wa walemavu uangaliwe vizuri. Sasa sijui kama naweza nika...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe nakushukuru. Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha, nina masuala mawili ya msingi sana, naomba niyaeleze. Leo asubuhi tuliahirisha kikao hapa kwa dakika tano kutokana na mahudhurio mabaya. Sasa jioni huwa zaidi, sasa kama tutachelewa leo, tutamaliza ikiwa saa 4:00 au 5:00, lakini tumalize hii bajeti yetu. Kwa hivyo, naomba mahudhurio Wajumbe waje mapema ili tuweze kufanya kazi yetu kwa mapema sana.

Waheshimiwa Wajumbe, jambo la pili, kuna Waheshimiwa Wajumbe wanatoa hoja zinajibiwa hawapo, wakija hapa wanasimama wanataka wajibiwe tena. Ukimuuliza umesikia wapi? Anasema nilikuwa garini, sasa na hilo hatulikubali. Kila Mjumbe aliyetoa hoja aje hapa asikilize majibu yake, karidhika sawa na kama hakuridhika apige buti mpaka aridhika, lakini mambo ya kusema nimesikia hoja yangu inajibiwa nikiwa ndani ya gari, sisi hatuikubali. Tuje tusikilize hoja ili tupitishe bajeti yetu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya maelezo hayo naahirisha kikao hadi saa 11:00 za jioni.

(Saa 6:59 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha
2014/2015 - Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

(*Majadiliano yanaendelea)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kutokana na michango yao na ushauri waliotoa katika kuchangia hotuba ya bajeti ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/15. Michango yote iliyotolewa hakika ni ya maana na ni muhimu katika kufanikisha mambo yanayotekelezwa na Ofisi hii.

Mhe. Naibu Spika, michango mingi iliyotolewa ilikuwa katika njia ya ushauri hivyo, naomba nichukue nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inathamini ushauri huo wote uliotolewa na inaahidi kuufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu niwatambue kwa kuwataja majina yao wale wote ambao walipata fursa ya kuchangia kwa maneno, yaani kwa kuzungumza humu ndani ya Baraza au kwa kuchangia kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, Mchangiaji wa kwanza alikuwa Mhe.Hamza Hassan Juma muwakilishi wa Kwamtipura ambae pia ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na yeye alitoa taarifa ya Kamati, maoni yake pamoja maoni ya wananchi wa jimbo lake. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk muwakilishi wa Jimbo la Kitope, Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa muwakilishi wa jimbo la Kikwajuni, Mhe. Mohammedraza Muwakilishi wa Jimbo la Uzini, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Muwakilishi wa Jimbo la Chambani, Mhe. Mohammed Haji Khalid Muwakilishi wa Jimbo la Mtambile, Mhe. Marina Joel Thomas muwakilishi wa Kuteuliwa na Mhe.Rais, Mhe. Salim Abdalla Hamad Muwakilishi wa Jimbo la Mtwambwe, Mhe. Ali Salum Ali muwakilishi wa Jimbo la Kwahani, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu muwakilishi wa Jimbo la Bububu, Mhe. Viwe Khamis Abdalla muwakilishi nafasi za wanawake, Mhe. Asha Bakari Makame muwakilishi nafasi za Wanawake, Mhe. Jaku Hashim Ayoub Muwakilishi wa Jimbo la Muyuni, Mhe. Mgeni Hassan Juma muwakilishi nafasi za wanawake, Mhe. Rufai Said Rufai Muwakilishi wa Jimbo la Tumbe, Mhe. Mussa Ali Hassan muwakilishi wa Jimbo la Koani na Mhe. Saleh Nassor Juma muwakilishi wa Jimbo la Wawi. Mhe. Naibu Spika, hao ndio waliochangia kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, waliopata nafasi ya kuchagia kwa maandishi ni Mhe. Shadya Muhammed Suleiman muwakilishi wa nafasi za wanawake, Mhe. Wanu Hafidh Ameir muwakilishi nafasi za wanawake, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa muwakilishi nafasi za wanawake, Mhe. Fatma Mbarouk Said muwakilishi wa Jimbo la Amani, Mhe. Abdi Mossi Kassim muwakilishi wa Jimbo la Matemwe, Mhe. Salma Moh'd Ali muwakilishi nafasi za wanawake, Mhe. Mahamoud Thabit Kombo muwakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki na Mhe. Kazija Khamis Kona muwakilishi wa nafasi maalum wanawake.

Mhe. Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza sana Mhe. Salehe Nassor kwa kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi Wilaya ya Chake Chake, namuomba *Allah* amuwezeshe kutekeleza vyema majukumu yake kama inavyostahiki.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa ufafanuzi pamoja na majibu ya baadhi ya masuali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kupitia idara moja moja na naomba hapa niwatanabahishe Waheshimiwa Wajumbe kwamba nimejitahidi sana kuziweka hoja katika idara. Kwa hivyo, pengine Mheshimiwa hatotajwa jina lake, lakini hoja yake itakuwa imezungumzwa, hii ni kwa sababu ya kubana matumizi ya wakati ambao wenyewe ni mdogo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia naomba kutoa ufafanuzi juu ya hoja za vifungu zilizotolewa na Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa na Mhe. Ali Salum, kwa mwaka wa fedha 2014/15 makisio ya mishahara kwa ajili ya Ofisi kuu Pemba ni jumla ya Shs. 210,000,000/= hii inajumuisha mishahara na waajiriwa wa kudumu wa serikali posho maalum kwa wafanyakazi na asilimia kumi ya mchango wa *ZSSF* kwa wafanyakazi, mgawanyiko huo unapatikana kupitia kasma kama zinavyoonekana katika kitabu chetu kasma namba 211101, 211110 na kasma 212101 alichokuwa anakizungumza Mhe. Hamza kifungu namba 211100 chenye jumla ya Shs. 207,260,000/=, sio mishahara peke yake ndani yake kuna vifungu vya mambo mengine ikiwemo posho za vikao, likizo, posho la kushika wadhifa na mambo mengine ambayo siyo sehemu ya mishahara.

Mhe, Naibu Spika, naomba niwafahamishe Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba tunavyoandika ndani ya kitabu chetu na jinsi majinia au kodi zilizotolewa ndani ya kitabu hiki ambacho kinaandika makisio kidogo, kuna utafauti na nafikiri serikali ipo kujipanga katika kuirekebisha hali hiyo ili iweze kuandama sambamba, ndio maana wakati mwengine Wajumbe wanapata kubabaika katika kufahamu, kuhusiana na hoja ya vifungu kwa ajili ya Tume ya Taifa ya kuraatibu na udhibiti wa dawa za kulevya vinaonekana, Mhe. Hamza alisema vinaonekana na tarakimu 00, hii ni kwa sababu sasa Tume haipo tena katika fungu la Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ambalo linasimamiwa na Katibu Mkuu.

Mhe, Naibu Spika, kuanzia mwaka huu wa fedha Tume ya kuratibu na udhibiti wa madawa ya kulevya itakuwa na fungu lake ambalo ni namba 51 na kwa mwaka huu linapatikana katika kitabu namba 2 ukurasa namba 371.

Mhe. Spika, kabla ya kuendelea kutoa ufafanuzi wa vifungu kama ambavyo imeulizwa na Mhe. Mahommoud Mussa, ningependa kutoa ufafanuzi wa jumla kama ufuatao: Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais huwa ina utaratibu wa kuweka vipaumbele kwa ajili ya mwaka husika na hivyo hufanywa na kila Wizara na Taasisi ya

Serikali, maeneo hayo huwa yanapangiwa bajeti, vipaumbele hivi huweza kubadilika mwaka hadi mwaka hali hiyo ndiyo inayopelekea kupanda kushuka au kutokuwepo kabisa kwa bajeti katika baadhi ya mafungu yanayoonekana ndani ya kitabu chetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nitoe ufafanuzi kwa kila kifungu kama ilivyoulizwa, fungu dogo 0401 kasma 263166 huduma ya utafiti, moja kati ya kazi za msingi za Idara ya Mipango Sera na Utafiti, ni suala la utafiti kazi ambayo inapelekea kufanya maamuzi ya kitaalamu, naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe kwamba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais katika mwaka wa fedha 2012/13, iliandaa mpango mkuu wa utafiti ambao unaelekeza maeneo mbali mbali ya utafiti katika Sekta za Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Idara hii ni miongoni mwa vipaumbele vyake ni kujenga uwezo wa watendaji wa kufanya utafiti kama inavyoonekana katika ukurasa wa 20 wa kitabu changu kifungu kidogo cha kwanza na cha pili.

Mhe. Naibu Spika, kupitia kasma hii, idara imepanga kufanya mafunzo juu ya mbinu za utafiti Unguja na Pemba kwa watendaji 20 kutoka idara na Tume ndani ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rasi pamoja na kufanya utafiti katika maeneo ya mazingira watu wenye ulemavu na Tume ya kuratibu na kudhibiti madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika, fungu dogo 0501 kwenye kasma 220107 ununuzi wa kanda za kurekodia na santuri, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mjumbe kwamba kasma hii inahusisha vifaa mbali mbali kwa ajili ya habari na mawasiliano, kupitia kasma hii Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imepanga kununua *video recorder*, *capture card used, portable digital audio tape recorder*, *DVD* na *CD*, waya *extraction* kebo na *mic table stand* kwa lengo la kuimarisha kitengo cha habari na mawasiliano ili kuhakikisha kwamba jamii inapata taarifa sahihi zinazohusiana na Sekta za Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kupatikana kwa vifaa hivyo, kutakiwezesha kitengo cha habari na mawasiliano cha Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupunguza utegemezi katika kufanya majukumu yake, ndio maana likaonekana fungu hilo, safari hii linakuwa na bajeti hiyo.

Mhe. Naibu Spika, fungu dogo 0501 kwenye kasma 220201, kasma hii imeongezeka kwa vile kutakuwa na mkutano mmoja mkubwa wa wafanyakazi wote pamoja na mafunzo ya ndani ya wafanyakazi juu ya *organization culture,* shughuli hizo hazikuwepo mwaka jana, pamoja na hayo viburudishaji vinategemewa kutolewa katika mikutano na vikao mbali mbali ikiwemo mkutano na Mheshimiwa Waziri na waandishi wa habari juu ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi, mikutano ya bodi za zabuni matarajio ni zaidi ya vikao vinne, Kamati ya uongozi, Kamati tendaji za Ofisi matarajio jumla vikao 48. Vile vile, wageni wa Mheshimiwa wanatarajiwa kupatiwa viburudishaji.

Mhe. Naibu Spika, fungu dogo 0901 kwenye kasma mbili 211116, ongezeko kwa kasma husika limetokana na kuongezeka kwa shughuli lengwa linalohusisha kasma hii, yanayotarajiwa kutekelezwa kupitia kasma hii ni haya yafuatayo: Serikali kupitia serikali ya Netherlands inategemea kuendesha mafunzo ya aina tofauti juu ya tathmini ya athari za kimazingira, mafunzo hayo yatanufaisha jumla ya washiriki sabini kutoka taasisi tofauti za serikali, serikali ya Netherlands itagharimia sehemu ya mafunzo hayo na fedha nyengine zitatoka kwenye kifungu hiki ukiwa ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kufanikisha mafunzo hayo. Warsha ya uhamasishaji juu ya mapitio ya sheria ya mazingira lengo ni kuwafikia wadau 30 wakiwemo Wajumbe wa Kamati ya kusimamia shughuli za viongozi, kuendesha uperesheni 96 za marufuku ya mifuko *plastic* na uperesheni 96 za kudhibiti uchukuaji holela wa mali asili zisizorejesheka.

Mhe. Naibu Spika, fungu dogo 2101 kwenye kasma 220201 limeonesha kukua kwa sababu Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia idara hii inatarajia kulingana na miaka iliyopita kasma husika inatarajiwa kuja kuhusika kuja kutumika kutekeleza shughuli zifuatazo: Uanzishwaji wa mkakati wa mawasiliano kwa watu wenye ulemavu, matarajio ni kufikia wadau 90, Warsha kwa wadau juu ya mkakati wa mawasiliano kwa watu wenye ulemavu, vikao mbali mbali vya idara vya kuendesha kazi kulingana na sheria, mafunzo kwa Jumuiya za watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, fungu dogo 2101 kwenye kasma 220509 limeonekana kuongezeka kulingana na miaka iliyopita, hii ni kutokana na gharama za mshauri juu ya mkakati wa mawasiliano kwa watu wenye ulemavu na gharama za uwezeshaji ambao watatumika katika kutoa mafunzo yatakayoendeshwa.

Mhe. Naibu Spika, fungu dogo 2101kwenye kasma 220514 limeonekana kukua sana ukilinganisha na miaka iliyopita, kasma hiyo imelenga kukamilisha ufikiwaji wa sera kwa walengwa kupitia mafunzo na utayarishaji wa sera husika kuliangana na mahitaji ukijumuisha hati nundu.

Mhe. Naibu Spika, fungu dogo 2102 kwenye kasma 220105, kifungu kinaonekana kukua ukilinganisha na miaka iliyopita kwa sababu pamoja na shughuli nyengine katika kipindi cha utekelezaji cha mwaka 2014/15, Ofisi ya faragha inatarajia kuandaa na kuchapisha nakala 1000 za jarida maalum juu ya shughuli za Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kipindi cha miaka minne shughuli hii haikuwepo mwaka uliopita.

Mhe. Naibu Spika, kifungu 211208 ni kwa ajili ya huduma za malipo ya walinzi fedha hii sh. 5,400,000/= zilizoainishwa ni kwa ajili ya ulinzi wa mkataba kwa Idara ya Mazingira Pemba ambayo kwa sasa idara hiyo ina mlinzi mmoja tu na ni mgonjwa hali ambayo inamuongezea mzigo wa ziada, ukizingatia hadi muda huu hatujafanikiwa kuajiri mlinzi mwengine wa kudumu.

Mhe. Naibu Spika, kifungu 311203 kimsingi hiki ni kifungu cha ununuzi wa vipando fedha zilizowekwa hapa ni 351,000/= zimepangwa kununulia baskeli mbili kwa ajili ya wahudumu.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu suala la Mhe. Mahmoud kuhusiana na fedha za mradi wa jimbo la Kilimani katika Jimbo lake la Kikwajuni, naomba nianze kwa kutoa Historia fupi kuhusiana na fedha za mabadiliko ya tabia nchi kupitia mfuko wa dunia wa mazingira, yaani *GEF the Global Environment facility*, kwa kawaida Serikali ya Jamhuri ya Muungano ndiyo inayoratibu utaratibu ni kwamba Ofisi ya Makamo wa Kwanza inapopata taarifa ya uwepo wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, basi hutakiwa kuwasilisha vipaumbele vya maeneo yanayopaswa kuzingatiwa kwa matumizi ya fedha husika, kilichojitokeza kuhusiana na fedha hizi ni kwamba Ofisi ya Makamo wa Rais Jamhuri ya Muungano ilichukua hatua ya kuchagua eneo la Kilimani bila ya kuishirikisha Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ambapo hii ni kinyume na utaratibu baada ya kuombwa na Mbunge wa Kikwajuni, Mheshimiwa Masauni ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge inayohusika na mazingira.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliheshimu uamuzi huo na kuliingiza eneo la Kikwajuni kuwa miongoni mwa maeneo yatakayofaidika na fedha za mradi huo, maeneo mengine ya mradi huo ni Tumbe, Mashariki na Magharibi, Ukele na Kisiwa Panza kwa eneo la Pemba na maeneo mengine ni bwawani Unguja.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Tanzania Bara, mradi huu unahusisha maeneo ya Pangani mjini, Bagamoyo, vijiji vya Kao kwa Mduma, Kidindu, Kwamsanja, Saadani na Makorogwe na Rufiji Nyamisati Gelta. Hatua ambayo imefikiwa hivi sasa kwa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imepokea barua pepe siku ya Jumatatu tarehe 19/5/2014 inayoeleza kuwa mradi utafanyiwa ukaguzi wa kuangalia hali halisi ilivyo na kwamba Kampuni ya *ICO Solution* ya Afrika ya Kusini ndio iliyoteuliwa na *SMT* kufanya kazi hiyo kwa maeneo yote ya mradi, kazi hiyo imeanza tarehe 21/5/2014 kwa maeneo ya Tanzania Bara na kwa hapa Zanzibar wataalamu hao wanatarajiwa kufika tarehe 31/5/2014 na watakuwa hapa hadi tarehe 6/06/2014.

Mhe. Naibu Spika, tumeiona *Hansard* ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Samiya Suluhu Hassan inayosema kwamba kuna fungu kubwa la fedha zilizotolewa kwa ajili kujenga ukuta eneo la Kikwajuni, lakini fedha hizo hazikutumika na badala yake zikabadilishwa matumizi na kutumika hasa katika kisiwa cha Pemba. Maelezo hayo Mheshimiwa Mjumbe wa Baraza hili tukufu na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili mimi kama Waziri ninayehusika na suala la mazingira Zanzibar, nasema sio sahihi hata kidogo na kwa kweli amelipotosha Bunge.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais hadi leo haijapokea hata shilingi moja kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano za mfuko wa *GIF* na wala hakuna mradi wowote wa kisiwa cha Pemba uliotekelezwa kwa fedha zinazotajwa hapa fedha za mazingira, kiutaratibu fedha yoyote inayoingia katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Wizara ya fedha, lazima iwe na taarifa nayo, iwe imepitia Wizara ya Fedha moja kwa moja, iwe imepitia idara au taasisi yoyote ya serikali, iwe imepitia Ofisi au Wizara taarifa hiyo, lazima itakuwepo Wizara ya fedha, namuomba Mheshimiwa Mjumbe mimi nimeiona *Hansard* na yeye ameiona na mimi nilimuarifu Mhe. Makamo wa Pili suala hili atusaidie.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu yeye ndie anaeratibu shughuli hizi za Muungano, atutafutia basi kwa maandishi usahihi wa fedha hii kuletwa hapa kwetu, pengine imeingia kwenye mkono wa mtu, imeondoka, lakini shughuli za kiserikali haziendi kwa maneno zinakwanda kwa maandishi na ushahidi wa maandishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, hili nimefatilia kadiri nilipofika na nafikiri Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anaendelea kulifatilia suala hili, ukweli tulionao sisi ni huu tuliouweleza hapa.

Mhe. Naibu Spika, ndio wakati mwengine ukaona sisi Wajumbe wa Baraza hili tukufu tulipokwenda kule katika mambo ya Katiba tukawa tunasema tuwe na utaratibu utakaoeleweka ambao kila mmoja atapewa chake katika Jamhuri hii ya Muungano wa Tanzania na itakuwa hakuna utatanishi tena. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa haya ndio masuala ambayo sisi wengine tuliona sababu zetu moja ni hizo kwamba zinapoingia kwa mtu mmoja, halafu mmoja agawe, matatizo ndio kama haya, tunagombanishwa, tunafitinishwa, kwa maneno ambayo si ya kweli hata mimi ningekuwa Mhe. Mahmoud tena amenivumilia sana, mimi nafikiri Mhe. Mahmoud Mussa wa Jimbo wa Kikwajuni, sio Mahmoud Thabit Kombo, mimi amenivumilia sana, mimi nafikiri ningekuwa ndio Mbunge au Mwakilishi wa Jimbo hilo na Waziri kule naambiwa maneno mengine na hapa naambiwa maneno mengine, mimi nafikiri nimeshamkaba Waziri anipe taarifa sahihi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini nashukuru sana ndugu zangu wote wawili hawa wamekuwa wavumilivu ingewaja wakati mwengine nao uvumilivu umewashinda na naelewa kwa nini kwa sababu hawana usahihi, lakini naomba kwa niaba ya serikali nieleze hilo hapa hatuna pesa ya *GF* iliyotoka Ofisi ya Makamu wa Rais SMT, kuja kwenye Serikali ya Mapinduzi hadi hivi ninavyoeleza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya ufafanuzi huo, naomba nielezee kuhusu sasa mafanikio ya safari kuna Wajumbe walihoji juu ya safari na kwa kuanzia, naomba nitoe ufafanuzi kwamba safari hizi za nje kulitokea utatanishi kidogo.

Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa mmoja alisema nataka kujua juu ya safari za nje za Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais ni kwa kweli kwa mwaka huu hakuwa na safari za nje za kazi ila safari hizo zilikuwa ni za watendaji na naomba nieleze kama ifuatavyo: Ofisi ya Mkamu wa Kwanza wa Rais inashughulikia masuala ya Mtambuka ambayo Kitaifa yana mikataba, kutokana na utaratibu wa kila mwaka kunakuwa na mikutano maalum ya kujadili utekelezaji wa mikataba hiyo pamoja na kuweka muelekeo.

Mhe. Naibu Spika, Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Mataifa wanapaswa kuhudhuria ushiriki wa Zanzibar katika vikao hivi ikiwa ni nchi moja inayounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapata fursa ya kuzungumzia jitihada zinazofanywa Zanzibar katika suala la mapambano juu ya dawa za kulevya, masuala ya watu wenye ulemavu, masuala ya UKIMWI na masuala ya Mazingira.Aidha ushiriki wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais unatoa nafasi ya kuwa karibu na mashirika ya Kimataifa na watekelezaji wengine kuwashughuli zinazofanana na Ofisi yetu. Vile vile, hii kutoa fursa ya kujenge uwezo na kujifunza kwa wetendaji wa Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais, lakini vile vile, kuweza kupatiwa misaada katika wakati fulani.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba nieleze mafanikio kwa ufupi yaliopatikana kupitia safari hizo saba za nje zilifanywa na wetendaji wa Ofisi wa Makamu wa Kwanza wa Rais, Safari ya Marekani, ujumbe wetu ulishiriki katika mkutano wa Kimataifa uliojadili haki na fursa za watu wenye ulemavu katika utekelezaji kabla na kupanga utekelezaji baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza ya maendeleo ya *MELENIUM,* yaani (*Cost Team*), safari ya Portland ujumbe wetu ulishiriki katika mkutano wa kumi na tisa (19) wa mabadiliko ya tabia nchi ushiriki wetu uliufanya Zanzibar kuwa ni sehemu ya maamuzi ya mkutano huo ambao moja kati ya maamuzi muhimu ni kuanzisha kwa mfumo maalum wa kuzisaidia nchi zitakazo athiriwa na mabadiliko ya tabia nchi ikiwemo nchi za visiwa.

Mhe. Naibu Spika, safari nyengine Mhe. Naibu ni safari ya Mauritius, Zanzibar ni sehemu ya mradi wa visiwa unaoitwa *Island Project* vilivyopo Magharibi mwa bahari ya Hindi, yaani *West Indian Ocean.* Hivyo, tunafaidika kwa ushiriki wetu katika mikutano na mafunzo mbali mbali yanayotolewa kupitia mradi huu, hadi sasa watumishi kumi na tano (15) kutoka taasisi mbali mbali wamehudhuria mafunzo ya aina tofauti nje ya nchi na wengine kutoka taasisi mbali mbali, yaani *SUZA*, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu, Idara ya Maafa, Tume ya Mipango, Wizara ya Fedha, Idara ya Uvuvi, *CODECOZ*, Idara ya Zima moto na uwokozi wote hao wamepatiwa mafunzo ya ndani, aidha Zanzibar ni Mjumbe wa Kamati ya Uongozi wa mradi wa *WOCC.*

Mhe. Naibu Spika, safari Seychelles ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilishiriki katika Ujumbe wa serikali uliokwenda Seychelles kujifunza hatua za kimaendeleo zilifikiwa hasa ukitilia maanani maumbile ya visiwa vyetu

na Seychelles, Safari ya Afrika ya Kusini Ujumbe ulishiriki Mkutano Mkuu wa Kimataifa kuhusu maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI kupitia Mkutano huo washiriki kutoka Zanzibar waliwasilisha mada inayohusu kuyafikia makundi maalum, safari ya Malawi Mkutano wa Mawaziri wa *SADEC* wa Afya na masuala ya UKIMWI kuhusu utekeleza wa Mkutano wa Kimataifa wa UKIMWI uliofanyika Afrika ya Kusini.

Mhe. Naibu Spika, safari ya Austria kwa mara ya mwanzo Zanzibar ilialikwa rasmi Mkutano wa Kimataifa unaosimamia uhalifu wa dawa za kulevya, Shirika la Kimataifa linalosimamia uhalifu wa dawa za kulevya *UNODC* waliweza kugharamia sehemu ya Ujumbe wetu pamoja na ushiriki kwa mara ya kwanza. Pia, Ujumbe wetu ulipata fursa ya kipekee kuwasilisha *road map* ikiwa na gharama zake za utekelezaji wa sheria yetu ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya,

Mhe. Naibu Spika, aidha, ujumbe ulipata fursa maalum ya kuwasilisha mada juu ya uzoefu wa Zanzibar wa kupambana na dawa za kulevya, vile vile, ushiriki wetu umeifanya Zanzibar kuwa karibu na shiriki hili la *UNODC* katika kuwajengea uwezo wataalamu wetu na wadau mbali mbali, hivi leo yameanza mafunzo ya siku nne ya *METHEDONE* kwa wataalamu wetu katika Hoteli yetu ya *Grand Palace*, mafunzo haya yatakuwa ni endelevu kwa wadau mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu hayo, sasa naomba kutowa ufafunuzi pamoja na majibu ya masuali yalioulizwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kupitia *sector* ya mazingira, Waheshimiwa waliochangia katika *sector* hii ni wengi akiwemo Mhe. Hamza, Mhe. Asha Bakari, Mhe. Mgeni, Mhe. Jaku, Mhe. Viwe, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Mhe. Mahmoud Mohammed, Mhe. Mohammed Mbwana, Mhe. Salim Abdulla, Mhe. Mwanaidi Kassim, Mhe. Shadya, Mhe. Saleh Nassor na wengine wengi, wengi wao walitoa ushauri juu ya namna ya kusimamia *sector* hii, tunapokea ushauri huo na tutaufanyia kazi, Mhe. Rufai nakushukuru sana kwa kutumia mda wako kuturudisha katika maandiko Matakatifu ili binaadamu turudi katika mazingatio hayo na tuweze kuyasimamia vizuri mazingira yetu.

Mhe. Naibu Spika, walitaka ufafanuzi juu ya mambo mbali mbali yanayohusiana na *sector* ya mazingira na naanza kutoa ufafanuzi huo, Waheshimiwa, mbali mbali walitaka Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais kuwa na mashirikiano na taasisi nyengine katika suala zima la kutunza mazingira, napenda kuwahakikishia kwamba hilo linafanyika hivi sasa, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum iko katika hatua za kutayarisha mkakati wa Zanzibar wa usimamizi wa taka, mkakati huo unatoa maelekezo juu ya namna bora ya kusimamia taka Rasimu ya awali ya mkakati huo umeshatayarishwa kwa kuwashirikisha wadau wote muhimu na inasubiri kupelekwa kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni zaidi, dira ya mkakati huo ni kuwa na Zanzibar safi kutokana na usimamizi bora wa taka.

Mhe. Naibu Spika, aidha, kuhusu taka za Hospitali katika kisiwa cha Chumbe Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na taasisi nyengine ilifanya tathmini juu ya namna bora ya udhibiti wa taka za Hospitali na ripoti inayoelezewa hatua zinazofaa kuchukuliwa imewasilishwa serikali.

Mhe. Naibu Spika, suala la utupaji taka katika eneo la Jumbi, napenda kumuarifu Mhe. Mussa Mwakilishi wa Jimbo la wananchi la Koani kwamba hivi sasa eneo la Jumbi halitumiki tena kwa matumizi ya kutupwa taka. Hata hivyo, upigaji dawa katika sehemu za majaa kutoka dawa za kinga haimo katika majukumu ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumuarifu Mhe. Mohammed Mbwana kwamba suala la udhibiti na uharibifu wa misitu linaratibiwa zaidi na Wizara ya Kilimo na Maliasili na ni imani yangu kwamba wakati ukifika Wizara hii itatoa maelezo ya kina juu ya hatua zinazochukuliwa kudhibiti uharibifu huo pamoja na kuwawezesha wananchi namna ya kukabiliana na mahitaji ya nishati ya kupikia, lakini kupitia mradi wamabadiliko ya tabia nchi, Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka imefanya tafiti mbili za kukusanya taarifa za msingi za uharifu wa misitu, sambamba na kuangalia mbinu mbadala za nishati ya kupikia kwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile tafiti zilionyesha kuwa taasisi zetu kama vile Dakhalia, Vikosi vya JKU, Mafunzo, KVZ, Zimamoto na KMKM vinatumia kuni nyingi kwa kupikia na kupelekea uharibifu mkubwa wa misitu yetu, kupitia mradi husika mafunzo ya kutengeneza majiko sanifu kwa Askari wa vikosi yamefanyika chini ya uwozeshwaji wa mkufunzi kutoka *TATEDO* Tanzania Bara, mpango uliopo ni wa kujenga majiko ya mfano kwa

kuanzia katika chuo cha mafunzo Kilimani. Vile vile, mpango kazi wa kupunguza uharibu wa misitu umetayarishwa.

Mhe. Naibu Spika, suala la mifuko ya *plastic,* nalo lilichangiwa sana napenda niwatowe wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe kwamba mifuko hii huwaangamizwa kwenye sehemu iliyowazi mbali kabisa na makaazi ya wananchi wanaofanya kazi hii, huvaa vifaa vyote vinavyostahili kwa kujikinga, aidha, kwa upande wa kilo zilizokamatwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, hili liliulizwa na Mheshimiwa wa kutoka Mtambwe Mhe. Salim, kutoka Unguja kumekamatwa *kilogram* moja (1) kutoka Pemba mia tisa na sabiini na saba (977).

Waheshimiwa Wajumbe, kazi ya udhibiti wa mifuko ya *plastic* ni ngumu na inahitaji mashirikiano ya kila mmoja wetu, si rahisi katika kipindi cha muda mfupi ambapo Ofisi imeanza Operesheni kuweza kumaliza kazi hiyo, Operesheni hizo zinakwenda hatua kwa hatua na sisi tunaamini kuwa hatua hizo zinaridhisha na ndio maana Zanzibar kwa sasa inapigiwa mfano katika suala hilo. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeshafanya kazi kubwa, naombeni na nyinyi Waheshimiwa Wajumbe mtuunge mkono pale Mhe. Mjumbe anapoigundua mifuko ya *plastic*, atupe taarifa asiendelee na safari zake, atupigie simu, awapigie watendaji wangu ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, haisaidii hata kidogo kwa Mhe. Mjumbe wa Baraza lako hili tukufu ambae ndiye mtungaji sheria kuona sheria ikivunjwa, aidha, kwa kuona magari ya mchanga yanapita wakati sio au mifuko ya *platic* inatumika na yeye akinyamazia kimya akasubiri bajeti kuja kutwambie hapa, kwa kweli mnakuwa hamjatusaidia sana, sisi wote tunatakiwa kushirikiana katika masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, suala la udhibiti wa mchanga, nalo limeanza na linaendelea vizuri, lakini ni gumu na ndio maana hata askari wanaosimamia hili mara kadhaa huwa wanajeruhiwa na wananchi hawa waovu na wahalifu. Hivyo, kila mmoja wetu awe askari wa jambo hili na sisi tusiyafumbue macho tunapoyaona tuyatolee ripoti.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na hoja ya mabadiliko ya tabia nchi ambayo imechangiwa sana na Wajumbe wengi, naomba nikubaliane na wachangiaji wote kwamba hili ni suala zito na ambalo linahitaji ushirikiano na ushiriki wa kila mmoja wetu, hasa kwa kuzingatia kwamba maeneo ya visiwa, ndio yaliyo hatarishi kwa jambo hili, Ofisi yetu imeshaandaa mkakati wa mabadiliko ya tabia nchi, mkakati huu umeelekeza maeneo ya vipaumbele yanayofao kuzingatiwa ikiwa ni pamoja na maeneo ya ukanda wa pwani, ambapo mmong'onyoko wa fukwe ndio umejitokeza zaidi, kwa kujua kwamba gharama za kuzuia athari hizo pamoja na za sekta nyengine ni kubwa, Ofisi yetu peke yake haiwezi kudhibiti athari hizo ila kwa mashirikiano ya jamii, taasisi mbali mbali pamoja na Washirika wa Maendeleo, tunaweza kupiga hatua.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na Ofisi ya Idara ya Mazingira, napenda kukubaliana na hoja nyingi za Waheshimiwa, lakini naamini kwamba serikali imelisikia hili na italifanyia kazi, lakini hata hivyo, Ofisi yetu nayo iko katika hatua za kujaribu kutafuta watu wa kuweza kutusaidia katika masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa ningie masuala ni mengi na nitaomba Wajumbe wengine wanivumilie kwa sababu nikiyajibu yote kwa saa moja, haitawezekana, naomba niingie katika Idara ya Watu wenye Ulemavu, nashukuru sana kwa michango na ushauri na nakubaliana na Wajumbe wote kwamba sisi hapa wote ni walemavu watarajiwa, huwa kila siku nalisema hilo na ukweli huo haufichiki.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nitoe maelezo kuhusu juhudi za serikali za kusimamia haki za Watu wenye Ulemavu, idara hii ilipokabidhiwa kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilikuwa tayari inasheria namba (9) ya mwaka 2006. Hata hivyo, hakukuwa na sera ambayo ni kitu muhimu katika kuweka muongozo ambao wadau wote hupaswa kuitekeleza ili kutoa huduma, haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu, hayo yote yaliyoelezwa na Waheshimiwa Wajumbe mengi yao yamesababishwa na kutokuwepo kwa sera hiyo, kama nilivyotoa taarifa kupitia kitabu changu, hivi sasa Ofisi yetu imekamilisha Rasimu ya awali kwa kutambua mapungufu mengi yaliyopo katika kufikia haki na fursa, kazi ya uandaaji wa sera ilifanyika baada ya kufanya utafiti na kubaini mapungufu hayao.

Mhe. Naibu Spika, lengo ni kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata haki na fursa stahiki pamoja na kufanyia kazi, changamoto mbali mbali zinazowakabili ndugu zetu hao.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na kuwasaidia watu wenye ulemavu walioko Pemba ni kwamba ruzuku inayotolewa kwa sasa huwa zinapitia katika Jumuiya mbali mbali za watu wenye ulemavu katika tathmini tuloifanya kuhusiana na ruzuku hiyo, tumegundua kwamba baadhi ya Jumuiya hazifikishi fedha hizo kisiwani Pemba, Ofisi yetu imeshawasiliana na Jumuiya husika na imeandaa muongozo kwa mwaka huu wa fedha, shughuli nyengine zinazofanywa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kama vile za kutoa visaidizi hugusa pande zote mbili za visiwa vyetu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ali Salum, alitaka kujua mahusiano yaliyopo kati ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Wizara ya Afya katika suala la kupatikana kwa viungo bandia kwa watu wenye ulemavu, Ofisi yetu ina mashirikiano ya karibu na Wizara ya Afya kupitia shughuli zake ilizojipangia ikiwemo uwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya katika Baraza la Taifa la watu wenye ulemavu ili kuweza kutoa michango yake na kusimamia maamuzi ya Baraza kwa upande wa *sector* ya Afya ikiwemo upatikanaji wa viungo bandia kwa watu wenye Ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, alitaka kujua, je, Ofisi yetu imejipangaje kuwasaidia watu kwa mwaka huu, naomba kumjibu Mhe. Makungu kama ifuatavyo: Katika mwaka huu 2014 -2015, Ofisi kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu imejipangia kutekeleza yafuatayo; kuwapatia ruzuku, kwa vikundi vya ujasiriamali na Jumuiya za Watu wenye ulemavu, kuwapatia visaidizi mafunzo ya Uongozi na masuala ya fedha, mafunzo ya makuzi ya awali ya maendeleo ya mtoto mwenye ulemavu na kushirikisha katika shughuli nyengine ikiwemo kuanzia mpango wa mawasiliano na mpango mkakati wa sera ya Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na suala la kesi Mhe. Ibrahim Makungu na Mhe. Viwe, Mhe. Bi Mgeni walitaka kujua kesi za udhalilishaji kwa watu wenye ulemavu wanasaidiwa vipi?

Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri kwamba tatizo la ubakwaji ni kubwa na bado hatuna maamuzi sahihi yanayotokana kwa wale waliofanya matendo hayo. Hivyo, naomba tushirikiane na taasisi zote ikiwemo Mahakama, Polisi, Wazazi na Jamii kwa ujumla ili kuwasaidiwa watoto wetu wenye Ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi yetu kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu inafanya ufuatiliaji wa karibu juu ya masuala haya ikiwemo kuishauri Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka juu ya kuzifanyia upya vipimo vya *DNA*, aidha, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pale inapotokea kushindwa kwa kesi kwa sababu zisizoridhishwa kukatia rufa kesi hiyo na kusikilizwa katika Mahakama nyengine ya juu kama ya kesi ya tarehe 30/04/2014 iliyohukumiwa katika Mahakama ya Mwera, Ofisi ya Makamu wa Kwanza pia kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu inashirikiana na kitengo cha hifadhi ya mtoto kilichopo chini ya Ustawi wa jamii katika ufatiliaji wa kesi za udhalilishaji kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Asha Bakari Makame, alitaka kujua Ofisi yetu inashirikiana vipi na Ofisi ya Rais kazi na Utumishi wa Umma ili kupata ajira kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Spika, suala la ajira kwa watu wenye ulemavu ni changamoto kubwa, lakini kupitia Baraza la watu wenye ulemavu, nimefanya ziara mbili na kuonana na Katibu wa Tume ya Utumishi Serikali pamoja na ziara moja kwa Wizara husika kwa ajili ya kuzungumzia changamoto hiyo, pamoja na hayo, watu wenye ulemavu wanatakiwa waombe ajira pale zinapotangazwa na kuelezea aina ya ulemavu walionao ili Tume iweze kutambua kwamba muombaji ni mtu mwenye ulemavu na kuweza kupatiwa kipaumbele kama sheria yetu ya Umma inavyoeleza.

Mhe. Naibu Spika, watu wenye ulemavu ambao wameajiriwa katika *sector* binafsi na za serikali na wangapi wana vitega uchumi wangapi hawana napenda kueleza kwamba kutokana na takwimu tulizonazo ni kwamba waloajiriwa katika taasisi na sekta mbali mbali ni elfu moja na nane Unguja na Upande wa Pemba ni mia saba na arubaini. Hata hivyo, idara inaendele kukusanya taarifa hizi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku, nae alitaka kujua kwa nini fedha za idara ya watu wenye ulemavu zimepungua katika kifungu cha ununuzi wa visaidizi kutoka mia mbili na ishirini mwaka jana mpaka kufikia milioni thamanini kwa mwaka huu hii ni kutokana na ufinyu wenyewe wa bajeti.

Mhe. Naibu Spika, pia, kulikuwa na suala lilohoji juu ya fedha za mfuko wa watu wenye ulemavu hadi sasa fedha zilizokusanywa ni milioni mia moja tisiini na tano laki nne na thamanini na tatu, lakini bado kuna ahadi ambazo hadi leo hazijatekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, sasa nigusie sekta nzima ya dawa za kulevya, Waheshimiwa wamechangia katika sekta hii karibu wote waliozungumza humu ndani kwa kuwa ni suala nyeti, michango mingi imehusu *Sober house* na biashara haramu ya dawa za kulevya na mradi wa kituo cha tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya.

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya jukumu lake kubwa ni kuratibu vita dhidi ya dawa za kulevya, ikiwemo kupunguza usambazaji kwa njia ya kuelimisha jamii, kupunguza usafirishaji na kuwaunganisha wana jamii na wasimamizi wa sheria pamoja na kubaini mapungufu yanayojitokeza katika maeneo yao mbali mbali. Kinga na Tiba na marekebisho kwa watumiaji wa dawa za kulevya katika kuratibu Tume pia huwa inawaunganisha wana jamii na wasimamizi wa sheria kwa lengo la kuibua mbinu za kuzuia na kupambana pamoja na kubaini mapungufu ya upepelezi na kuyafanyia kazi. Kuimarisha mahusiano ya kimataifa kwa lengo la kupata taarifa za wanaojihusisha na biashara kwa lengo la kuwachukulia hatua za kisheria na kuwahamasisha wana jamii kwa kukubali kutoa ushahidi unaohusiana na uhalifu wa dawa za kulevya.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuwafahamisha wajumbe kwamba *Sober Houses* zimeanzishwa kwa juhudi za watu binafsi, ofisi yetu inawashukuru sana wananchi waliochukua hatua hiyo. Hadi sasa kuna jumla ya *Sober Houses* 136 ziko Pemba na 7 ziko Unguja. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais hadi sasa inatoa ruzuku kwa Soba House 11 kwa kuzipatia shilingi 1,500,000 kwa kila moja. Pia Ofisi yetu kwa kushirikiana na vitengo vya Wizara ya Afya hufanya uchunguzi wa siha kwa vijana wa *Sober House* na kuwapatia huduma zinazostahiki. Kuhusiana na hoja ya kuzuia vijana wa chini ya miaka 18 na wenye watoto wachanga, hili lilichangiwa na Mhe. Bi Asha Bakari Makame na Bi Mgeni Hassan Juma, hili ni katika kuhakikisha kwamba *Soba Houses* zinazoanzishwa zinakidhi vigezo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe taarifa kwamba suala hilo lililoelezwa hapo ni kweli na kwamba hatua hiyo imefanywa kwa makusudi, kwa sababu ya kumlinda mtoto. Katika sheria zetu chini ya miaka 18 ni mtoto na Idara wakati huo ikiwa Idara sasa ni Tume imeandaa muongozo wa jinsi ya *Soba Houses* hizi kuweza kusajiliwa na kuweza kufanya kazi. Kwa kweli kwenye *Sober House* hii inayozungumzwa *Sober House* ya wanawake, kulipatikana kwamba kuna watoto chini ya miaka 18 hawa sio waathirika wa dawa za kulevya. Ni watoto ambao wazazi wao ndio waathirika wa dawa za kulevya nao wanakaa kwenye nyumba hizo na wapo bado. Na mwengine alikuwa na mtoto wake mchanga na yeye yumo humo humo.

Mhe. Naibu Spika, hili limefanywa kwa makusudi, kwanza kwamba watoto wale nyumba hizi zinaitwa nyumba za kurekebisha tabia kwamba wale waliomo tabia zao zina mtihani na zimo kwenye kurekebishwa. Mhe. Naibu Spika, wakiachiwa watoto ambao wao sio waathirika wakawa watoto hao wanaathirika kiakili, wanaathirika kisaikolojia na hata afya zao zinakuwa katika matatizo. Ndani ya *Sober Houses* hizi wengi hawa ni waathirika wa maradhi mbali na watoto ni rahisi sana kuweza kupokea maradhi. Lakini lugha zinazotumika ndani ya *Sober Houses* hizi, hazikuzi mtoto wala haziwi na malezi mazuri kwa mtoto. Kwa hivyo hilo limefanywa kwa makusudi kabisa katika kuona kwamba mtoto wetu huyu analindwa ili akue bila ya kufanyiwa matatizo yoyote.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala kidogo la Mhe. Ali Salum kuhusu nyumba ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Naibu naomba nianze kwa kutoa maelezo ya msingi kwamba, baada ya uundwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa viongozi wetu wa kitaifa walistahiki kupatiwa stahiki zao yakiwemo makazi yanayostahiki na kwa bahati nzuri kwa upande wa Makamo wa Pili ilikuwa rahisi, kwa vile kama Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali aliweza kurithi yale yote yaliyokuwa yametengwa kwa ajii ya Waziri Kiongozi. Kwa upande wa Mhe. Makamu wa Kwanza ililazimika kumtafutia nyumba stahiki kwa Unguja, Pemba, Dar es Salaam. Na kwa kuanzia ililazimika kuwekwa Bosnia, nyumba hiyo aliishi kwa kitambo na zikajitokeza dosari mbali mbali zikiwemo, nyumba haikuwa na faragha ya kuishi kiongozi wa kitaifa kama ni makaazi ya kudumu ya walinzi na matokeo yake walinzi waliishi pia ndani ya nyumba na kuwa kama hoteli.

Ghasia zilizojitokeza wakati wa *weekend* kuanzia Ijumaa jioni hazikuwa zikitoa fursa kwa kiongozi kupata mapumziko na ukosefu wa maji nao umekuwa ukilazimisha kununuliwa maji kwa ajili ya matumizi nyumbani, lakini pia nyumba haikuwa katika hadhi ya kukaliwa na kiongozi. Tuliwasilisha kadhia hii serikalini na serikali ilifanyia maamuzi yafuatayo:-

Kutafuta nyumba ya serikali inayoweza kufanyiwa marekebisho na kuweza kumuweka Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, ikishindikana hatua ya pili basi ilikuwa atafutiwe nyumba ya binafsi, serikali iweze kukodi na kumuweka Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais. Juhudi ya kutafuta nyumba ya serikali zilifanywa chini ya Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Ni nyumba moja tu ilionekana inaweza kuwa na hadhi ya kuwa na makaazi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini nyumba yenyewe ilikuwa mbovu mno na ilihitaji gharama kubwa na isingekuwa rahisi serikali kulipa gharama hizo kwa mkupuo mmoja.

Kwa hivyo serikali iliamua kukodi nyumba kwa ajili ya makaazi ya Mheshimiwa na nyumba 7 binafsi zilipatikana na kuweza kukaguliwa na kitengo cha ulinzi wa viongozi PSU na kwa bahati nyumba ya Mbweni ndio ilionekana kufikia kigezo.

Aidha kwa upande wa Pemba, awali viongozi wote wawili Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais walipangiwa wawe wanafikia nyumba ya kulala wageni ya Wizara ya Fedha ambayo baadae ilionekana ni tatizo kwa viongozi wetu wawili kuwapangia wakiwa wanachangia chumba kimoja.

Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais akawa anaomba kufikia nyumba ya Mhe. Spika, ambayo Baraza hili hili lilitoa muongozo kumtafutia Mhe. Makamu wa Kwanza Rais nyumba, kwa vile zaidi ya mara mbili alilazimika kukatisha ziara yake Pemba kumpisha Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kutumia nyumba hiyo. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliweza kumpatia nyumba ya binafsi ya kukodi.

Kwa upande wa Bara juhudi kubwa tulitumia kumtafutia nyumba ya serikali Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ili kumpatia makaazi ya kudumu. Ofisi ya Katibu Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi ilimtafutia nyumba haikupatikana. Meneja wa Shirika la nyumba la taifa na kuonana na Katibu Mkuu Wizara ya ujenzi ambapo kwa pamoja na kuonana nao na kuiandikia rasmi. Hata hivyo hadi leo pamoja na kufuatilia hatujafanikiwa.

Mhe. Makamu wa Kwanza Rais anaendelea kufikia Hoteli katika safari zake za Dar es Salaam. Hivyo fursa iliyobakia kumtafutia nyumba binafsi na hili lipo katika bajeti yetu ya mwaka 2014 ambapo Mhe. Ali Salum aliuliza fedha hizi ni za nini? Nyumba ya Unguja kodi ni dola 2000 kwa mwezi na ya Pemba ni dola 1000 kwa mwezi. Mhe. Naibu Spika, yaliyochangiwa kwa kweli ni mengi mno na tunaweza kuchukua hata masaa 2 kuweza kuyajibu haya.

Mimi ninaomba nimalizie kwa kutoa maelezo kidogo kuhusiana na Tume ya Ukimwi. Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii kutamka kwamba waheshimiwa wengi nao wameligusia suala hili na mimi naomba nijibu kama ifuatavyo:-

Mhe. Mohammed Mbwana alitaka kujua je matumizi ya *condom*, yanasaidia vipi katika kupunguza maambukizi ya ukimwi na kama matumizi hayo hayaongezi vitendo vya uasharati. Mhe. Naibu Spika, kuna mikakati ambayo imeshauriwa kitaalam kutumika duniani kote katika kukabiliana na maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi. Mikakati hiyo ni kwanza:-

Kujizuia tusifanye kabisa ngono yaani hilo tendo la nje ya ndoa, kuwa muaminifu kwa kuwa na mtu mmoja peke yake. Yaani mume awe muaminifu kwa mkewe na kinyume chake hii inajulikana kama *zero grazing* na kama mtu hawezi mawili yaliyotajwa juu na kama ni lazima afanye ngono na mtu asiemuamini basi anashauriwa atumie condom. Mambo matatu hayo yanaweza kumuepusha mtu asipate maambukizi kwa kupitia njia ya kujamiiana hakuna mtu anayelazimishwa uamuzi bado unabaki kwa mtu mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya pili ni ya Mhe. Mohammed Mbwana ni kwamba suala la uasharati haliambatani na kuwepo au kutokuwepo kwa *condom*. Ni uamuzi wa mtu binafsi kwani hata vitabu vitakatifu vya dini zetu vinakataza tendo la uasharati lakini bado lipo.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya Mhe. Salum Abdalla ni kutaka kujua kwa nini *condom* za kiume zinasambazwa kwa wingi zaidi ikilinganishwa na zile za kike. Mhe. Naibu Spika, napenda kuwajibu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu hoja hiyo kama ifuatavyo:-

Condom za kiume zimetengenezwa na kuanza kutumika kwa shughuli nyengine hata kabla ya ukimwi. Shughuli hizo ni kwa ajili ya uzazi wa mpango na kuzuia magonjwa yatokanayo na kujamiiana. Kwa hivyo matumizi yake

yamezoeleka zaidi katika jamii, *condom* za kike zimebuniwa hivi karibuni baada ya kuona njia gani inaweza kuongeza ufanisi katika kuzuia maambukizi ya virusi vinavyosababishwa ukimwi kwa upande wa wanawake.

Jengine ni kwamba katika uzalishaji wa *condom*, viwanda vinavyozalisha condom huzalisha condom za kiume zaidi kuliko za kike. Aidha elimu ya utumiaji wa *condom* za kike bado iko chini. Juhudi za kutoa elimu kwa watumiaji zinaendelezwa. Naye Mhe. Salum Abdalla alitaka kujua haya makundi maalum ni yepi, makundi haya ni makundi ambayo yapo kwenye hatari ya kuambukizwa ama virusi vya ukimwi kutokana na tabia hatarishi wanazofanya au wanazofanyiwa.

Makundi yenyewe ni wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao, wanawake wanaouza miili yao, jina jengine wanaitwa dada poa na wanaotumia dawa za kulevya hasa kwa njia ya sindano.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Khalid alizungumza kuwa mchango wa Serikali ya Mapinduzi wa asilimia 34 ni mdogo sana kwa hivyo aliitaka serikali kuiongezea Tume Fedha ili iweze kutekeleza mipango inayojipangia hasa kwa vile fedha za wafadhili zinapungua siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Marina nae alitata kufahamu kuwa kuna utaratibu unaotumika wa kuwapima wanafunzi wa shuleni na vile vile kutaka kujua matokeo ya upimaji huo. Napenda kumjulisha Mhe. Marina kuwa muongozo wa upimaji wa hiari wa virusi vya ukimwi unakataza upimaji wa virusi vya ukimwi chini ya umri wa miaka 18 isipokuwa kuwe na ulazima wa kupima kutokana na mahitaji ya kiafya au ya kisheria.

Kwa wanafunzi wenye umri wa miaka 18 wanapima kwa utaratibu wa hiari lakini takwimu zao zinajumuishwa kwenye takwimu za kawaida. Mhe. Jaku alitaka kujua kwa nini kumbi za starehe zisipigwe marufuku wakati zinachangia katika ongezeko la maambukizi ya ukimwi. Mhe. Naibu Spika, ninakubaliana na ushauri wa Mhe. Jaku lakini napenda kumjulisha kwamba suala hili linahusisha taasisi nyingi na linahitaji kufanyiwa kazi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nasema nina majibu mengi sana na isingekuwa rahisi kuyataja hapa yote naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu na kwa wale ambao watakuwa bado wana masuala wataendelea kuniuliza wakati tunapitisha vifungu kama yapo lakini nimejitahidi kuyazungumzia mengi sana.

Kwa sasa Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kuikubali hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumzi vya ofisi yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO – 2014/205

FUNGU 06 – OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Kifungu 0901 Idara ya Mazingira	10,500,000
Jumla ya Fungu	10,500,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba	399,575

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante Mhe. Naibu Spika, mimi niliuliza na naomba niulize kwa ufafanuzi tu sio kuzuia kifungu bali ningeomba Mhe. Waziri kama ataweza kutupa ufafanuzi kwenye kifungu (a) na (b) hii 211200 mishahara isiyokuwa ya fedha taslim, nilikuwa ninauliza tu hii kodi ya nyumba pamoja na ununuzi wa sare kwa nini ilikaa kwenye *wages and salary in kind? Usually wages and salary in kind* vifungu hivi huwa havikai katika eneo hilo nilikuwa nauliza ambacho ni cha milioni sita na laki nne.

La pili, hapo hapo kwenye fungu hilo hilo kuna ukurasa wa 45 nadhani niko kwenye fungu hilo hilo bado, kifungu 311200 ununuzi wa Honda, Vespa, Ciao ama pikipiki nimeona hapa bei yake ni 351,000. Sasa mimi labda sikumsikia vizuri alipotoa ufafanuzi huo na maana baskeli siku hizi ndio bei zake hizo. Lakini hapa kama ni baskeli pameandikwa *motorcycle*. Kwa hivyo labda na hapo tupate ufafanuzi kidogo tu. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu hoja mbili za Mhe. Mahmoud Thabit Kombo. Mhe. Naibu Spika, haya ni mazoea ambayo tumeyarithi kama nilivyokuwa natoa maelezo pale, kwamba Wizara ya Fedha ina *code* zao nawao ndio wanaoelekeza watendaji wetu ukitaka kuweka kifungu hiki ukiweke wapi. Kwa hivyo kunaonekana kama kuna utatanishi kati ya tunavyofahamu sisi wajumbe na hizi *code* zilizomo huu. Maana yake kuna kifungu kimoja nilikielezea bado kinataja santuri wakati santuri haziko tena on *circulation.* Kwa hivyo hiyo ni aina ya taarifa hizo na ninafikiri Waziri wa Fedha amelichukua hilo kwa ajili ya kulifanyia kazi.

Na lile la 311203 nilitoa taarifa pale kwa hicho kinahusiana na manunuzi ya baskeli mbili kwa ajili ya wafanyakazi.

Mhe. Mahamoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nampongeza kwa majibu yake mazuri kwa kusema kwamba ni mazoea na mimi kweli nakubaliana nae ni mazoea maana yamekuwa yakitajwa kama hivi kwa miaka mingi iliyopita. Ahsante sana.

Kifungu 03

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kuchangia niliulizia suala la malipo ya huduma ya ulinzi *(security service fees*) hivyo Mhe. Waziri wakati anajibu maswali yake ameniambia kwamba ni malipo ya ulinzi Pemba kama sikosei. Lakini mimi bado sijatosheka kwa sababu hii ni Taasisi ya Serikali na alipoeleza hii ni ulinzi kwa vile vikundi vya hawa walinzi wetu ambao wamejisajili.

Tatizo jengine aliloniambia yeye Mhe. Waziri ni kwamba pana mlinzi mmoja hivyo kuna upungufu, hivyo napata tabu kuelewa Mhe. Mwenyekiti pahala panapotokezea mapungufu ya mtu kustaafu taratibu za kisheria inatakiwa mtu aajiriwe mwengine ili ku-*cover* ile nafasi. Sasa kama kumekuwa na utamaduni sasa hivi ikiwa kuna mtu amestaafu mimi nafikiri Mhe. Waziri atanieleza kwa sababu bado sijatosheka na majibu yake.

Jengine nihoji sababu za msingi maana yake tuna vikosi vya ulinzi vya SMZ tukaache kulinda ofisi za Serikali kwa vikosi vyetu ambavyo nina imani kwamba gharama labda itakuwa nafuu zaidi kuliko hiyo gharama iliyowekwa ili tukaacha ile tukachukue vikosi vya uraiani, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nirudie yale yale niliyoyaeleza kwa sababu sina jibu jengine na hilo ndiyo jibu sahihi. Kikawaida ofisi inatakiwa kuwa angalau na walinzi wawili ukumbuke wote kwamba kuna siku za *holiday* ambazo kuanzia asubuhi mpaka usiku siku nyingine inakuwa hakuna kazi wala *activities* yoyote ndani ya maofisi yetu. Ofisi hizo zinahitajiwa ziwe katika hali ya usalama.

Sasa nimesema inapotokea hali ya dharura mlinzi mmoja aidha amestaafu au amekuwa mgonjwa, aidha na kwa ghafla uajiri si jambo la ghafla ni lazima uliombe katika *nominal roll* yako na wapatikane ili uweze kupewa. Serikali haiwezi ku-*risk* kuacha majengo na mali za Serikali zikiwa katika hatari kwa kuweka mlinzi mmoja kwanza huo hautakuwa ni ubinadamu, mlinzi mmoja huyo akitokewa na dharura yoyote pakaweza kuibiwa kosa litakuwa ni letu sisi ofisi. Kwa hiyo, sisi tumechukua hatua hii kwa ajili ya dharura pale tutakapopata mlinzi wetu wa kuajiriwa wa kudumu suala hili linasita na huu ni utaratibu upo ndani ya Serikali yetu na unaruhusiwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, bado mimi napata kigugumizi sana kwa sababu nchi hii inaongozwa kwa mujibu wa sheria Mhe. Mwenyekiti na ili mtu astaafu kuna *notice* ile ambayo anapewa *before* kwamba mwezi fulani

unatakiwa kustaafu. Sasa nachanganyikiwa kwamba inafikia pahala mtu anastaafu halafu maombi yanakuwa hayajaja wakati kuna muda ambao mtu wa kustaafu unakuwa unaeleweka kabla. Sasa unasubiri mpaka mtu anastaafu halafu unachukua pesa za walipa kodi unaajiri taasisi ambazo binafsi.

Halafu jengine nikamuuliza kwa sababu sijajua gharama za vikosi vyote vikoje, kwa sababu tunapotumia vikosi maana yake pesa ile bado ina-*rotate* katika Serikali, kama tumeamua labda kwa uoni wake labda ndiyo tunasaidia ajira za watu binafsi, atanisaidia Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, anayosema Mhe. Ali nadhani tumeyafahamu sote, lakini ni hivi nataka na yeye afahamu kwamba muda wa kustaafu mtumishi hauna maana kwamba unakwenda sambamba na muda wa ajira, mtumishi anaweza akastaafu lakini ile nafasi kujazwa ikawa bado muda wake haujafika kujaza ile nafasi.
Lakini vile vile kuna wastaafu wengine wanastaafu kwa maradhi huwezi ukajua kwamba huyu mtu ameshafikia miaka 60, anaweza kustaafu mtu kwa ugonjwa tu. Kwa hivyo, lazima akubali kwamba maelezo ambayo ameyatoa Mhe. Waziri kwamba tunazo taratibu za kuijaza ile nafasi kwa muda ili mpaka pale ambapo mtumishi yule atakapoweza kupatikana, basi ile nafasi anachukua yule mtumishi na yule aliyeajiriwa kwa muda anaondoka.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, tatizo langu unajua nashindwa kuelezwa kwa sababu mimi nasoma kitabu Mhe. Mwenyekiti, sasa kama yatatokezea kama ya Mhe. Hija Hassan Hija ya juzi kuondoka kwa nongwa hapa kwa kunipa majibu yaliyokuwa hayana msingi, nafikiri itafikia pahala…

Kinachonishangaza Mhe. Mwenyekiti, kwamba huu uajiri sijui una muda gani kwa sababu tangu bajeti ya mwaka jana, mwaka mzima mwaka jana kama wameshindwa kuomba uajiri na mwaka huu tunaingia mwaka wa pili. Sasa kwa kumaliza sitaki matatizo naye, hivyo aniambie tu Mhe. Waziri miaka miwili hii ameshindwa kuomba ajira ya mlinzi aniambie tu baada ya miaka mingapi anategemea kuomba hiyo ajira ya mlinzi ili tuondokane na suala hili la kuajiri *security fund?*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sisi tupo kwenye mchakato wa kuajiri na maombi haya yamepelekwa wakati wowote tutakapoletewa huyo mlinzi wa kudumu hili suala la walinzi hawa binafsi litasita.

Mhe. Ali Salum Haji: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti, nina subiri pengine.

Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba	369,575,000
Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera	

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa yakuweza kuuliza swali moja tu kwa hapa sasa hivi.

Mhe. Waziri alipokuwa akijibu masuala alijitahidi sana kutuelezea namna ya suala zima la zile fedha ambazo zimetoka kwa ajili ya mradi wa Kikwajuni. Maelekezo yake nimeyasikia lakini mimi bado naendelea kuchanganyikiwa hususan baada yakwisha kuipata *hansard* ambayo ni hii kutoka katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na nina hakika Waziri anapokuja kuleta hoja au kuzungumza kitu katika Bunge au iwe ndani ya Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa kanuni zetu kwa mfano ndani ya Baraza la Wawakilishi, kwa kutumia kifungu cha 59 (3), waziri hawezi kuja kuzungumza kitu ambacho hakina yakini. Kwa msingi huo basi, naomba unipe fursa nisome *hansard* ambayo inaelekeza na kutoa jawabu ya suala langu baadae nipewe jawabu la kuweza kuniridhisha kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni. Naomba kusoma *hansard* hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: *Hansard* ya Baraza gani?

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa: Ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Mwenyekiti: Ndiyo unayotumia wewe sasa hivi?

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa: Ndiyo ninayotumia mimi sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti: Haya soma.

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa: Ahsante imetoka kwa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano.

"Mhe. Mwenyekiti, amesema kile kifungu cha Nam. 270800 ambacho ni fedha za ruzuku za *MEMC* tulizozungumzia, fedha za *GEF* ninataka nihakikishiwe Mhe. Mnyaa kwamba pesa hizi hazitumiki upande mmoja, katika hotuba yangu tulisema kwamba fedha hizi zinaombwa kwa ajili ya miradi midogo midogo, sasa hivi ofisini kwetu kuna miradi mitatu kutoka Zanzibar. Mradi kutoka Kaskazini maeneo ya Matemwe, na mradi wa Pwani Mchangani, kuna mradi kutoka Pemba na kuna mradi kutoka Kusini Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, ufundi wa fedha hizi ni namna ya kuombwa, ukiomba na mradi ukatimiza vigezo, fedha hizi zinakwenda. Mimi nataka niseme kwamba kwa mwaka 2013 kuna fungu kubwa la fedha lilikwenda kwa ajili ya mradi wa kujenga ukuta eneo la Kikwajuni Mjini Unguja. Fedha zile hazikutumika baada ya kufika Zanzibar, fedha zile zilibadilishiwa matumizi na zikatumika katika miradi mengine hasa katika Kisiwa cha Pemba. Kwa hivyo basi, fedha hizi zitatumika pande zote".

Alikuwa anajibiwa huyo Mjumbe ambaye alikuwa akiuliza suala katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa kwa vile naona hapa hili Bunge ni chombo kikubwa na sisi hatuna haja ya kupoteza muda kwa kulumbana, ninachokuomba Mhe. Mwenyekiti tutumie kanuni ya 120 ili tuunde Kamati Teule ambayo itakwenda kupata uthibitisho wa suala hili. Je, hizi fedha zilikuja Zanzibar au hazikuja au kuna nini baina yake hapa kati kati. Naomba muongozo wako Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani kabla hajatoa uamuzi bado Mawaziri wapo na utapewa maelezo na utakinai.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru ndugu yangu Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa kwa nia yake njema na dhamira nzuri yakutetea wananchi wa Kikwajuni na wa Zanzibar kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyotueleza kwa *hansard* hiyo naomba Mhe. Mahamoud atuachie jambo hili katika Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais kwa kuwa ni suala ambalo linahusu mambo ya Muungano na wizara yetu hii inasimamia mambo ya Muungano kwa upande wa Zanzibar. Hivyo tulifanyie kazi tukiwa na ushahidi ambao ametupa tuwasiliane na waziri muhusika, tupate maelezo ya kina ili baadae tuje na jibu sahihi. Si vyema kwa jambo kama hili ambalo wahusika wapo na wizara husika zipo kuunda Kamati Teule, ni jambo ambalo bado lingefanyiwa kazi kwa taratibu za kiserikali kwa kuwasiliana na wenzetu tukapata majibu yaliyo sahihi ili tupate majibu muafaka ambayo yatasaidia katika kuendeleza shughuli mbali mbali zikiwemo hizi za kudhibiti mazingira katika nchi yetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi naheshimu sana maelezo ya swahibu wangu hapa Mhe. Muhammed Aboud Muhammed lakini suala hili la mazingira ndani ya eneo la Jimbo la Kikwajuni ni suala la muda mrefu. Tukiangalia hii *hansard* toka mwaka 2013, hili suala linazungumzwa kwamba lilikuwa tayari mustakabal wake umekwisha kufikia, na kipindi ni kirefu tumekuwa tukileta na kuleta ikiwa mimi mwenyewe pamoja na watu wengine ambao nilikuwa nawaomba kuliulizia suala hili hadi tumefikia leo hapa, na bado suala hili halijapata ufumbuzi ambao unastahiki.

Mhe. Mwenyekiti, bado naendelea kusisitiza maombi yangu yakutumia kanuni kifungu Nam. 120 kuundwa Kamati Teule ili tuweze kupata ithibati ya suala hili, badala ya kuendelea kusubiri wakati hali ya mazingira ndani ya Jimbo la Kikwajuni inazidi kuharibika na maisha ya watu sasa hivi yanazidi kuwa mabaya. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, na mimi bado namuomba Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa kwamba wakati wa kuunda Kamati Teule bado haujawasili, na utakapowasili basi sisi kama Serikali tutakuwa hatuna kipingamizi. Lakini tunayo nafasi yakuwahoji wenzetu kiutaratibu fedha yote inayotoka Jamhuri ya Muungano lazima iingie Hazina ya Zanzibar, tunayo nafasi yakutaka kujua tarehe gani zimetumwa, tunayo nafasi yakutaka kujua zimeingia kwenye *account* gani. Sasa haya yote bado sisi hatujayapatia majibu yake, mimi nadhani Mheshimiwa atustahamilie kwanza kwani Dar es Salaam siyo mbali tutapata nafasi hiyo tutauliza wenzetu. Na kama

wao wana *quiry* au wana hoja kusema kwamba pesa hizo zimepelekwa Pemba na sisi tunayo nafasi kuwauliza ndugu zetu wa Pemba, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kazipeleka kwa kutumia *account* gani, kama hizo pesa zimekwenda.

Sasa haya yote hatujayafanyia kazi bado, hivyo mimi namuomba Mhe. Mahamoud shemeji yetu huyu awe mstahamilivu tumalize hii kazi, sisi Serikali tukishindwa kumpa majibu ndiyo hapo tena anaweza akasema kwamba sasa wakati wa kuunda Kamati Teule basi na sisi kama Serikali tutasema iundwe, kama itashindikana Kamati ya Sekta kufuatilia tutasema Kamati Teule iundwe. Mimi namuomba atupe nafasi hiyo sisi Wizara ya Fedha tulishirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tutafanya kazi hiyo na tutampa jibu katika kipindi kijacho.

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana sana na hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha hapa swahibu wangu na shemeji yangu, ndugu yangu Omar Yussuf Mzee, lakini tatizo ambalo mimi nalipata kinachoonekana hapa Mhe. Mwenyekiti hii pesa iko hewani hatujui kwamba iko ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au iko ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi hoja yangu nataka kuelezwa hii fedha hasa iko wapi na ndiyo maana nikaleta hoja ya kuunda Kamati Teule ili Kamati hii sasa iende ikafanye uchunguzi itaweza kufahamu hii fedha ilitoka ndani ya Jamhuri ikaja Zanzibar au imekuwa imepata matatizo gani hapa njiani. Kwa sababu kutoka Tanzania Bara mpaka kuja Unguja pana bahari hapa na ina kina kirefu, ndiyo maana nikataka kupata ufafanuzi wa suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, bado hoja yangu iko pale pale naomba nipate ufafanuzi wake.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Mahamoud anavyosema mwenyewe na sisi tunataka tupate huo uhakika fedha hii kama imeletwa kutoka Tanzania Bara, imeingia wizara gani, imeingia katika *account* gani na hapo ilipoingia kama imeingia imetumika kinyume na utaratibu tuweze kujua na haya tutampa maelezo Mhe. Mahamoud hilo ambalo analolitaka yeye ndiyo tunamwambia kwamba sisi Serikali bado hatujashindwa atupe muda tulitafute. Na nataka nimwambie tu na kama kweli zimeingia ndani ya Serikali hii halafu zikatumika kinyume cha utaratibu basi hao ambao waliofanya hivyo itabidi sasa chini ya Makamu wa Pili wa Rais iwachukulie hatua, hatuna njia nyingine itabidi wachukuliane hatua tu. Kwa hivyo, atupe nafasi kwanza tufanye hiyo kazi na kama nilivyoeleza tutashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais sote tuzitafute hizi pesa tujue zimeingia tarehe gani na katika account gani, halafu tutampa maelezo.

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwa kumuheshimu na kumpenda sana shemeji yangu naomba sasa aniambie muda gani atatumia kuhakikisha suala hili litakuwa limemalizika.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru shemeji yetu Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa kwa msingi huo nataka nimuhakikishie kabla ya kumalizika Baraza hili la bajeti basi tutampa majibu yaliyo sahihi na tutaleta taarifa hii rasmi ya Serikali hapa Barazani.

Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuheshimu kiti chako naomba tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti

Mhe. Mahamoud Thabit Kombo: Tupo katika kifungu 0401 ambayo ni Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ninaelewa Idara hii kazi zake kwa upana kidogo. Katika kifungu hicho hicho Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 263100 ukurasa wa 47, kuna hii sehemu ya ruzuku ambayo ni huduma za utafiti *(research service)* hapa pana milioni 76,645,000 katika mchango wangu niliuliza kidogo naomba mchanganuo wa *research* hizi, naamini kwamba kwa kuwa Idara hii inafanya *research* maeneo *very sensitive* kama vile mazingira, madawa ya kulevya, walemavu kidogo huko kwa hiyo ningeomba mchanganuo wa *research* hizi za kugharimu milioni 76 kwa hizo sehemu ambazo husika zitafanyiwa hizo *research.*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli pana fungu hapo kama alivyoeleza Mhe. Mahamoud Thabit Kombo na hilo ni fedha za ruzuku kwa ajili ya tafiti. Wakati nafanya majumuisho nilitaja kwa kuwa sasa nina makaratasi mengi itabidi nianze kuyatafuta tena kidogo ni kazi, kwa sababu hizo ni tafiti zinazohusiana na shughuli zinazofanywa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, zikiwemo tafiti zinazohusiana na Idara ya Watu wenye Ulemavu, zinazohusiana na shughuli za mazingira na suala zima la dawa za kulevya, lakini vile vile shughuli za UKIMWI.

Shughuli zote ambazo zinaratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ndio tafiti zinazoshughulikiwa fedha zake, ndio hizo zinazoonekana hapa katika Idara ya Sera, Mipango na Utafiti.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, nimeuliza swali *very simple question,* yaani hizi fedha shilingi 76,000,000 kwa hizo sehemu tatu zimegawika vipi, sikupata jibu hilo. Lakini kama ataniahidi kunipatia kwa maandishi basi nitashukuru, nitatizama wakati huo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Sawa Mhe. Mwenyekiti, hizi fedha zote zinaonekana mchanganuo wake katika *MTEF* na zipo na tutampatia kwa maandishi.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	146,065,000
Kifungu 0501 Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1,610,184,000
Kifungu 0901	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze rafiki yangu Mhe. Saleh Nassor Juma kwa kipindi cha tatu mfululizo kuwa Katibu wa Wilaya Chama cha Wananchi *CUF*, na hii inapelekea wakati wowote kuwa Mwenyekiti kwa dalili hizi. *(Makofi)*

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, kifungu 0901 Kasma 263100, nilihoji ofisi ya rafiki yangu Hamad Mjaja, Mazingira. Ofisi ile hairidhishi na kama kweli mazingira ndio kioo chenyewe kile basi tuna wakati mgumu. Nilikuwa nataka kujua lini *list* ile itafanyiwa marekebisho.

Hoja yangu ya pili hapa hapa bila ya kupoteza muda, kama hiyo ni Ofisi ya Mazingira, imeshirikishwa vipi kuondoa Kituo cha Daladala Darajani na hivi sasa tunashuhudia *parking*. Ni hayo tu Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, wakati najibu nilieleza kwamba tunakubali kuwa jengo la Idara ya Mazingira liko katika hali mbaya halitoshi, lina kila ila mbaya ya kuwa Ofisi ya Mazingira. Lakini kutokana na ufinyu wa maofisi ya serikali ndio wamejibana bana pale. Suala hilo linajulikana serikalini na jitihada za kutafutwa ofisi ambazo zitakuwa na hadhi zinaendelea ndani ya serikali, lakini ofisi zote haziwezi kujengwa kwa wakati mmoja.

Sisi wenyewe Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais tunaendelea na jitihada za kuona kwamba tunaweza kupata jengo hata yale wanayohama watu wengine, ambalo litakuwa katika hali nzuri. Lakini vile vile serikali inao mpango wake labda Waziri wa Fedha kama atapenda kutaja kuweza kuhakikisha kwamba ofisi zote za serikali zinapatiwa majengo, lakini mpango huo uko kwa awamu na bila shaka Idara ya Mazingira nayo imo katika utaratibu wa kupatiwa ofisi ambayo itakuwa inaridhisha. Hata sisi mtu ukiwa mrefu kidogo ukienda kwenye hiyo ofisi inabidi uende kwa kuinama, wafanyakazi hapatoshi, vifaa pa kuweka hatuna, lakini kwa sasa ndipo tulipokuwanapo hatuna pengine, tunajitahidi kutafuta njia ya kuweza kupata pahali pazuri.

Suala la Kituo cha Mabasi kilichopo karibu na Skuli ya Kisiwandui, hili tumezungumza na waziri mhusika kwa kuona jinsi gani kituo kile ambacho kipo kwa muda kwa sababu si cha kudumu kitaweza kuwasaidia watoto wenye ulemavu, kupanga mpango kuona kwamba watoto wenye ulemavu wanaosoma katika skuli ile ambayo inatoa elimu ya mjumuisho, wanasaidiwa ili wasipate athari na purukushani kubwa iliyoko pale kwa kushirikiana pia na vyombo vyetu vya ulinzi, yaani Jeshi la Polisi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nafikiri hoja yangu ya mwanzo nilikuwa nataka kumshauri kama itawezekana. Mimi naona Hoteli ya Bwawani bado haijajaa na nafasi ipo, sijui anafikiria vipi kuwapeleka kule kutokana na hali hiyo.

Hoja ya pili nafikiri Mhe. Waziri hakuisikia au hakuifahamu, naomba niizungumze kidogo kidogo ili ipate kueleweka. Nasema ofisi yake imeshirikishwa vipi kuondosha Kituo cha Daladala Darajani wakati yeye yumo katika mazingira, ndio mazingira yale na leo tumeshuhudia pale pale *parking* zimeanza kurudi.

Mhe. Mwenyekiti: Umemuelewa? Hoja ya kwanza anakushauri kwamba Bwawani nafasi ziko je, mnatizamaje kwenda kuhamia kule?

Halafu la pili, katika kuhamishwa kama mtu wa mazingira ulishirikishwa kuhamishwa kituo Darajani kuja pale Kisiwandui?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nimepokea ushauri wake lakini nimuarifu tu kwamba ile Hoteli ya Bwawani haiko chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwa hivyo, sisi wenyewe hatuwezi kuamua tu kujiondosha kule tuliko Idara yangu ikenda kwenye Hoteli ya Bwawani. Hayo anayosema ni sahihi kwamba iko tupu na labda iko pia tunaweza kuipata bila ya kuilipia, hayo ni mambo ambayo itabidi tuyatafiti, labda tuuchukue huo ushauri kwa ajili ya kufanyia kazi na tafiti zinazohusika.

Hili la pili, kwa kweli katika masuala ambayo moja kwa moja yanahusiana na taasisi yenyewe moja peke yake, mengine kufanyia maamuzi Ofisi yetu inakuwa haiyaingilii maamuzi hayo. Kwa hiyo, suala zima la kuhamisha Kituo cha Daladala hili ni suala linalohusika na Manispaa na ofisi yangu haijashiriki katika suala hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naona Magharibi inaingia tusipoteze muda tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Salum Haji hoja tatu zimetolewa pale, moja kamaliza yule, sasa ngoja nyengine mbele uwahi. Tunaendelea.

Kifungu 0901 Idara ya Mazingira 113,284,000
Kifungu 2101 Idara ya Watu wenye Ulemavu

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tuelewane, mtu mmoja akitoa hoja mbili mwenzake anamalizia moja. Kwa hivyo, kila mtu atoe moja na wenzake wapate.

Mhe. Ali Salum Haji: Nakushukuru, mueleze Mhe. Jaku Hashim Ayoub asing'ang'anie hoja akatuzuia na sisi. Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilitaja kifungu 263129, Huduma za Walemavu na nilizungumzia namna ya bajeti ya mwaka jana ambayo ilitengewa shilingi 258,020,000, lakini mwaka huu ikatengewa shilingi 115,625,000. Nilitaka kujua sababu za msingi za kuwapunguzia bajeti ndugu zetu walemavu katika suala hili.

Pia wakati nachangia katika kitabu hoja ya pili naichukua kabisa Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia suala zima la ushirikiano wa Taasisi ya Makamu wa Kwanza na Wizara ya Afya katika suala zima la viungo vya walemavu, walemavu wa viungo, viungo bandia. Mhe. Waziri wakati akifanya majumuisho hapa amesema kwamba wanashirikiana vizuri. Tatizo langu Mhe. Waziri anijibu, unajua kushirikiana kimaneno na kisera si tatizo, lakini tatizo linaloonekana ni kwamba vile viungo vinauzwa na tunaowauzia ni walemavu. Sasa kinachonipa tabu kwamba mimi nilifikiri labda Ofisi ya Makamu wa Kwanza itatenga fedha kama alivyotenga mapesa ya kodi ya nyumba kuwasaidia walemavu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu vile viungo vinauzwa sasa leo mtu hana mguu unamuwekea gharama ya kwenda kununua kiungo, sijui kama hili suala linaingia akilini, leo mtu hana mkono utamuwekea gharama ya kwenda kununua kiungo, hivi kweli tunawatendea haki walemavu Mhe. Mwenyekiti? Sasa nataka kujua labda wizara yake haoni kwamba kuna haja ya kutenga fungu kwa wale watu ambao wana ulemavu wa mikono.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza hili kwa unyonge kabisa, kwa sababu ndani ya mwaka mmoja nina vijana wawili ambao wamepoteza viungo vya mikono ikiwemo ajali ya pili ya vijana ambao walikuwa wanakwenda Makunduchi. Kijana wangu wa pili amepoteza mkono, kijana anahitaji kiungo labda Mhe. Waziri anambie ninachotaka kukijua ni namna gani wizara imejipanga katika mashirikiano ya kutenga fungu kwa upande wa walemavu kuwasaidia hawa walemavu wa viungo. Nashukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu hoja mbili zilizoelezwa na Mhe. Ali Salum Haji kama ifuatavyo:

Kwanza kifungu 263129 aliuliza kwa nini fungu hili limepungua kutoka shilingi 258,000,000 kwenda shilingi 115,000,000. Mhe. Mwenyekiti, bajeti inapangwa kutokana na kile ulichonacho. Kwa hivyo, ukiwa na kidogo na matumizi yako yanakuwa kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, matatizo ya ndugu zetu wenye ulemavu ni mengi na makubwa, mimi nilifikiri Mhe. Ali Salum Haji na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa sasa angalau waone jitihada kiasi gani serikali imeifanya. Kabla ya Idara ya Watu wenye Ulemavu kuwepo kwenye Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kulikuwa hakuna ruzuku yoyote hata ya shilingi moja ya kusaidia watu wenye ulemavu, chini ya ofisi yetu kumeanzishwa utaratibu huu wa kuweza kuwanunulia vifaa. Sasa kama ninavyoeleza watu wenye ulemavu wana matatizo ya vifaa vya elimu, watu wenye ulemavu anavyoeleza yeye pia na mimi nakubali wana matatizo pengine ya kupatiwa viungo bandia, watu wenye ulemavu hususan watoto hata watu wazima wanahitaji vifaa vya kuweza kutembelea na ulemavu uko wa aina tofauti. Watu wenye ulemavu wa kuona wanahitaji mabuku ya kusomea yenye *braille*. Kwa hiyo, mtatizo ni mengi lakini uwezo wa serikali ni mdogo.

Mimi kama kutaka ningetaka wapewe fungu kubwa sana hata kuwawezesha wale wajasiriamali watu wenye ulemavu tuweze kuwawezesha vile vile. Kwa sababu wanakuwa katika vikwazo katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku, lakini uwezo wa serikali yetu ni mdogo. Kwa hiyo, ndio maana kule kunakotengenezwa vifaa na hili suala lingefahamika zaidi kutoka Wizara ya Afya, wanatakiwa kuchangia katika kutengeneza vifaa hivyo. Uwezo ukiwa mzuri bila shaka fungu hili la huduma kwa watu wenye ulemavu likiweza kukua basi ni dhahiri kwamba tunaweza kutoa huduma hiyo. Lakini kwa sasa ni vigumu na hatuwezi kuitoa huduma hiyo bure kutoka Idara yetu ya Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, mimi hii hoja ya mwanzo nitaiachilia lakini hii ya pili ya viungo bado nitaing'ang'ania. Pamoja na majibu mazuri ya dada yangu hapa, unajua ameeleza vizuri tatizo ni fedha na akajaribu kuitupia baadhi ya mzigo sekta husika kwamba Wizara ya Afya ina haja ya kupunguza bei; akitaka hivyo itabidi mpaka mwisho tutafute sekta inayotengeneza vigurudumu huko Uingereza. Yeye ndiye mwenye wadau, hawa ni wadau wake walemavu na tunawaona jinsi wanavyoteseka Mhe. Mwenyekiti.

Mimi nilifikiria labda Mhe. Waziri atanisaidia moja tu, kusema labda kupitia ule Mfuko wa Walemavu uliokusanywa basi labda atatenga fungu dogo la kuwasaidia wale walemavu wa viungo sio kubwa, angalau kupunguza ile gharama. Kwa sababu gharama ni kubwa na watu wanashindwa kupata viungo bandia, na kama tutafanya mahesabu watu ambao wana ulemavu katika nchi yetu ni hatari, kama kuna watu 100 basi ambao wana viungo bandia ni watatu. Hii ni hatari na ni hatari kwa nchi yetu kwa sababu hawa watu tunawakosesha haki za msingi Mhe. Mwenyekiti. Anieleze angalau katika ule Mfuko wa Walemavu atatenga kiasi gani kupeleka Wizara ya Afya ili kuwasaidia watu wenye ulemavu wa viungo. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, unashauri ule Mfuko kidogo atenge fedha.

Mhe. Ali Salum Haji: Anieleze kupitia pesa za Mfuko wa Walemavu watatenga kiasi gani kupeleka Wizara ya Afya kuwasaidia walemavu wake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nipokee ushauri wa Mheshimiwa katika yale matatizo mengi ya watu wenye ulemavu ambao Mfuko huu unalengwa kusaidia basi moja nalo liwe hilo.

Mhe. Ali Salum Haji: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hapa nilizungumzia suala zima la Skuli ya Kisiwandui na watu ambao wanasoma skuli ile kwamba ni walemavu ambao Mwenyezi Mungu amewajaalia maumbile maalum. Na nikataka vile vile nielekezwe hapa na Mhe. Waziri atakapokuja ni sababu zipi zinazoendelea kuona kwamba eneo lile bado daladala ziendelee kuwepo pale na kuweza kuleta matatizo na bughudha kwa wanafunzi ambao wanasoma pale. Tulisema kwamba, wanafunzi wale ndio wanaopaswa kuangaliwa hasa namna gani ya kuweza kulindwa kutokana na afya zao. Sasa naomba Mhe. Waziri atusaidie kwa sababu alipotoa ufafanuzi hakunijibu suala hili, naomba maelekezo yake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa maelezo yalitolewa hapa sasa hivi, lakini kama unataka nyongeza Mhe. Waziri ongeza kidogo. Mimi nilikuwepo nimesikia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, najua Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa leo alikuwa na suala lake la Kilimani limemkaa kichwani ndio liko mbele. Kwa hiyo, alikuwa hasikii kitu chengine.

Mheshimiwa nilieleza kwamba utaratibu ule wa pale ni wa muda tu na kwa ajili ya kukabiliana na hali iliyopo sasa ofisi yetu inashauriana vile vile na Manispaa pamoja na Jeshi la Polisi, kuhakikisha kwamba kunakuwepo na hali ya utulivu na kuweza kuwasaidia hususan watoto wetu wale wenye ulemavu mpaka kituo kile kitakapoondoka. Lakini lini kitaondoka hili ni suala linaweza kujibiwa na mwenzangu ambaye yupo hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini pia nataka nimuombe Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni kuhusu kituo. Kwanza nataka niseme waendesha daladala wanao-*park* kituo kile hawakuruhusiwa kisheria, kile si kituo cha ku-*park* ni kituo cha kushusha na kupakia abiria tena hakipo katika usawa wa Skuli ya Kisiwandui, kipo katika usawa wa *block No. 7*, wanashusha wanapakia. Kwa hiyo, wale wanaokaa pale wanafanya ubishi na wanavunja sheria. Sisi kama serikali tutaendelea kuzihimiza taasisi zinazohusika hasa Jeshi la Polisi kusimamia lile ili ile vurumai iweze kuondoka pale, lakini si kituo ambacho kimewekwa pale kisheria. Ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nimefarajika na Mhe. Waziri toka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, lakini zaidi tutazidi kulizungumza suala hili litakapokuja katika bajeti ya wizara husika. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 2101 Idara ya Watu wenye Ulemavu 278,442,000
Kifungu 2101 Idara ya Faragha

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa nina hoja mbili, hoja moja wakati Mhe. Waziri anafanya majumuisho sikupata kusikia jawabu langu. Kwa sababu leo niko makini sana kwa kweli na sio kwake kwa wote watakaokuja baadae asiwe na wasi wasi.

Hoja moja sikupata jibu Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa katika ukurasa wa 61, fungu 272100 kifungu kidogo 272108 *Support Social Economic Activity* hili ni fungu la kusaidia shughuli za kiuchumi za kijamii. Mhe. Mwenyekiti, nilitaka anisaidie kunipa mchanganuo kwa sababu hata kwenye kiambatanisho mengi ameyapembua kwenye kiambatanisho katika masula ya mafunzo na *Activity* na mambo ya Kimazingira na nini. Lakini hakupata ufafanuzi wa yale maeneo ya hizi pesa zilizotumika na nilimtaka anitajie Shehia kwamba labda Shehia gani ambazo zilinufaika na huu mfuko na huko kwenye kitabu imeelezea na huu mfuko na kwenye kitabu imeelezea masuala ya Msikiti, Madrasa pamoja na idadi ya watu wahusika. Sasa hili sikulipata jibu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, hili fungu dogo la 211201 Matengenezo ya Nyumba , alijaribu kutoa maelezo mengi Mhe. Mwenyekiti, mimi bado nina masikitiko makubwa sana katika hichi kifungu na nna masikitiko makubwa kwa sababu hata Mhe. Waziri katika majibu yake kwa kweli hayakunifurahisha hata kidogo. Wakati anajibu suala la kuhamisha makazi ya Mhe. Makamu wetu wa Kwanza wa Rais kutoka katika maeneo ya Bosnia kuja huku Mbweni ameeleza kwamba Mzee wetu pale siku za *Week end* anapata tabu ya kulala kwa sababu ya zogo, akaeleza tatizo la maji Mhe. Mwenyekiti.

Cha kushanganza Mhe. Mwenyekiti, kwamba sijui huyu mzee wetu ana utukufu gani kwa sababu historia ya Bosnia mimi nina kumbukumbu ya viongozi wakuu watatu wameshakaa pale. Sasa kama hawa wana maumbile na yeye atanisaidia katika majibu yake. Mhe. Dr Omar Ali Juma ameishi pale, Dr. Mohd Gharib Bilali ameishi pale, Mhe. Rais wetu ambaye tunae sasa hivi Dr Ali Mohd Shein ameishi pale.

Mimi nilifikiria kwamba angenijibu vya kutosha kwamba labda angenijibu kwamba ameondoka kwa dharura kwamba kuna matengenezo yatafanywa ili baadae arudi ningejiridhisha Mhe. Mwenyekiti. Lakini kwa hoja kwamba za *Week end* kwa sababu hata hapo alipo Mhe. Mwenyekiti, hayuko katika pahala ambapo pana faragha yuko kati kati ya majumba ya watu amezungukwa na majumba ya watu Mhe. Mwenyekiti. Watu wakiamua kupiga rusha roho

sijui atalala vipi? Mimi nilimwambia kabisa kwamba viongozi wetu wanahitaji wakae katika *VIP Area*. Sasa majibu alionipa Mhe. Mwenyekiti, mimi sijaridhika nayo.

Lakini pia katika hizi fedha ambazo zimetengwa za Ujenzi wa Nyumba ambazo amelalamikia ikiwa leo mtu anaweza kwenda kumuweka hoteli nashangaa kwamba asiweze kukaa pale Mhe. Mwenyekiti, hili suala la fedha pia anisaidie kwa sababu huu ujenzi umetafautika nini? kwa sababu pesa ambazo zimetengwa kwa ujenzi milioni tisini na nane, lakini mwaka huu zimekuja milioni kumi na nne kuna *Different* ya karibuni milioni kumi na nane anisaidie maelezo ya kutosha ili nimpitishie.

Mhe. Mwenyekiti, kama sikupata majibu ya kutosha mimi sitoridhika labda Wajumbe wenzangu wataridhika na hili kwamba mwenzetu ana utukufu mkubwa sana tafauti na viongozi wenzake waliopita atanisaidia Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hoja tatu zote umetoa peke yako hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo sio mapya yale yale niliyoyaleza tu. Lakini nimfahamishe vizuri ndugu yangu hapa. Anavyoeleza mimi nashindwa kumfahamu mara anaonekana ana imani sana na huyu kiongozi na kwamba awekwe kwenye sehemu nzuri kama viongozi wengine mara anahoji ana utukufu gani sasa nashindwa kuelewa. Lakini nitajibu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza hilo ni agizo la Serikali Kuu kwamba nyumba ya Bosnia ya muda mrefu haijawahi kufanyiwa ukarabati wowote na haistahiki kukaa kiongozi sio agizo la Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais huyo ni kiongozi wa nchi na naomba nimuarifu pia anaonekana kuelewa kwamba ile nyumba imekaliwa na fulani na fulani. Nimfahamishe tu kwamba hawakuwa wanafanya makazi ya kudumu pale, walikuwa na makaazi yao mengine ya kudumu. Kwa hivyo, hayo hayakuwa makaazi ya kudumu.

Sasa nimeeleza sababu nyingi moja wapo tu ikiwa ya ghasia za *Week end.* Sasa nashindwa mimi kumfahamu Mhe. Ali Salim kama ana jengine aseme. Lakini kwa maelezo niliyoyatoa na si mara ya kwanza, Bajeti iliyopita limeulizwa hili na nimelieleza kwa kina kwamba nyumba ya Bosnia haifai kukaa kiongozi na ni uamuzi wa Serikali Kuu si uamuzi wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais mimi sina maamuzi hayo.

Kwa hiyo, Serikali imeamua kumuweka kiongozi wake kwenye makaazi anayostahiki. Sasa kuanza kuhoji utukufu wa kiongozi mimi najua, viongozi wetu watatu hapa tunawaheshimu na wana hadhi ya Viongozi Wakuu. Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Kwanza na Mhe. Makamu wa Pili hizo ndio hadhi ninazozijua mimi, utukufu ninaoujua ni wa *allah* na kama utakatifu wa mwenyewe *Sub-hana wataala*. Lakini hawa ni viongozi ambao wanastahiki kukaa kwenye makazi yenye hadhi yao. Hicho ndicho ninachokijua na huo ndio uamuzi wa Serikali uliofanyika. Sasa nashindwa kumuelewa.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja ya pili, shughuli za Kijamii fedha hizo ugawaji wake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, suala hili lipo kwenye mafungu ya viongozi Wakuu wa Serikali. Lipo kwa Mhe. Rais, lipo kwa Mhe. Makamu wa Pili na lipo kwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ni fedha zao ambazo wanakuwa nazo zinatengwa kwa ajili ya shughuli zao kama viongozi. Kwa hiyo, uchanganuo wa hili lote chuo gani, skuli gani wala hakuna maelekezo yanayosema kwamba katika fedha hizi uhakikishe asilimia fulani imekwenda Mkoa fulani au imekwenda chuo fulani, au imekwenda kanisa fulani au skuli fulani ni yeye mwenyewe. Viongozi hawa watatu kwa kadri wanavyokwenda wakifanya shughuli zao ahadi wanazoweka ndipo wanakotoa.

Kwa hiyo, mimi sikuona sababu ya kuuleta mchanganuo hapa. Lakini Mhe. Ali Salim kama anataka mchanganuo upo ni mrefu mno tutaweza kumletea kwa maandishi aone jinsi gani fedha hizo zilivyotumika.

Mhe. Ali Salim Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namshukuru mama angu. Suala la kusema pesa za Serikali ndio hoja niliyoitaka mchanganuo hii pesa ya Serikali Mhe. Mwenyekiti, na pesa ya Serikali inavyotumika lazima ieleweke na ndio maana mimi nikataka nitajiwe Shehia. Sasa hili nitakubaliana nao kwamba nataka anieletee Mhe. Waziri na ndio utararibu lazima tujue wapi zinakwenda na wapi zinatumika vipi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hoja hii imemaliza, kulikuwa na hoja ya *difference* haikuijibu ya pesa ya fungu 211201 hiyo hakujibu kabisa. Tofauti ya mwaka jana na mwaka huu. Lakini bado narudi kwenye nyumba Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninapouliza nauliza kutokana na majibu yake, yeye Mhe. Waziri ndiye alinambia kwamba pale *Week end* alikuwa anapata tabu hata hawa waliokaa kama walikuwa hawana makaazi ya kudumu lakini miongoni mwa siku waliokuwa wakikaa *Week end* ilikuwa inaingiliana ni yeye mwenyewe alinijibu. Kwamba pale alikuwa anapata tabu siku ya *Week end* ghasia nyingi. Sasa aliponieleza hili ndio nikasema kwamba iweje yeye ghasia zimuudhi na wengine zisiwauzi akahisi labda kwamba mimi nina jambo fulani, hakuna jambo Mhe. Mwenyekiti.

Lakini bado nakuja hapa Mhe. Mwenyekiti, kwamba hata hilo eneo na ndio maana kasema kwamba nampenda, yote yapo kwa nini nisimpende na kiongozi. Mhe. Mwenyekiti, bado nadadisi kwamba hapo alipo usalama pia sio mzuri, lazima tujue.

Halafu hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, nielezwe sababu ya msingi kwamba anachoelezea kwamba ile nyumba imekuwa na matatizo ya uchakavu najua uchakavu maana yake ni kwenda na kurudi. Mhe. Mwenyekiti, nielezwe sababu za msingi bado sijapewa sababu za msingi Mhe. Mwenyekiti, za kuondoka Bosnia kwenda kukaa vichochoroni.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Salim Haji kaa upewe sababu za msingi.

Kwanza unaambiwa kuwa Serikali ndio iliyoamua hivyo kwa hiyo Serikali ipo itazungumza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo ya ziada kuhusu suala la Mhe. Ali Salim Haji.

Kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa maelezo yake ya kina na mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, ni uamuzi wa Serikali kama alivyosema Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwamba nyumba ya Bosnia iko katika hali mbaya na inahitaji kufanyiwa matengenezo makubwa, na sababu nyengine za mahala penyewe zilivyojitokeza Serikali iliamua Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais atafutiwe pahala pengine na kwa sababu Serikali haina nyumba za kutosha kwa viongozi wetu ukweli ni huu. Tuna matatizo makubwa ya nyumba kwa viongozi wetu na tunafanya jitihada ili tuweze kujenga nyumba mpya zitakazokidhi na zenye sifa za viongozi wetu hawa wakuu.

Kwa hiyo, kwanza tuombe radhi sana mahala ambapo hata sasa anapokaa Mhe. Makamu wa Kwaza wa Rais asingepaswa kuwepo hapo angepaswa kuwepo pahala mazuri zaidi ya alipo. Lakini kutokana na hali halisi ya uwezo wetu Mhe. Makamu wa Rais ameridhia kukaa hapo anapokaa na tunamshukuru kwa imani hiyo.

Kwa hiyo, niwaombe Wajumbe wezangu tukubaliane na maelezo ya Mhe. Waziri kwamba sasa hivi tatizo letu ni ukosefu wa nyumba kwa viongozi wetu wakuu. Mara Serikali itakapopata uwezo tutajitahidi na tumo mbioni kujenga nyumba zitakazokidhi na stahiki kwa ajili ya viongozi wetu wakuu hapa Unguja Pemba na sehemu nyengine wanazokaa ikiwemo Dar - es Salam.

Kwa hiyo, naomba sana Mheshimwia aridhie hili na ajue kwamba uamuzi wa Serikali na pale Bosnia nia yetu Serikali itaendelea kuwa ni *Rest House* itatumika kwa viongozi wanaokuja kwa muda wakitoka Dar-es Salaam wakitoka sehemu nyengine hata viongozi wa nchi nyengine wanapokuja nchini kwa sasa hatuna mahala pa kuwaweka ndio maana inatubidi tuwaweke kwenye Mahoteli.

Kwa hiyo naomba turidhie maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri wa Nchi na hiyo kauli ya Serikali na tumuombe sana Mheshimiwa akubaliane nasi kutokana na hali halisi ya uwezo wetu wa kiuchumi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Salim Haji Serikali imetoa kauli.

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Serikali imetoa kauli na nimesikia. Lakini ninapozungumza Makamu wa Kwanza wa Rais simzungumzi kwa huyu aliekuwepo hichi ni cheo ambacho kiko kikatiba. Nataka nieleweke leo yuko huyu kesho yuko mwengine. Serikali kauli iliyotoa Mhe. Mwenyekiti, kwamba huyu ameridhika kukaa pale. Lakini tuna miezi michache tu au mwaka mmoja tutafanya uchaguzi inawezekana atakekuja asiridhike na kukaa pale.

Mhe. Mwenyekiti, pale pahala bado si mazingira mazuri ya kumuweka kiongozi mkuu. Sasa Serikali inatakiwa ijipange sijui katika hili Mhe. Mwenyekiti, Serikali inatuahidi labda muda gani basi anaweza kufanya huo utekelezaji kwa sababu nina hofu tusije kupata Makamu wa Rais mwengine kipindi kinachokuja akawa hajaridhika tukawa tunahangaika kumtafutia makaazi. Atwambie basi katika hii mipango amepanga muda gani ambao Serikali itatekeleza ujenzi wa viongozi wetu ili kukaa katika makaazi yanayostahiki.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nia njema ya Serikali ya kuwajengea nyumba viongozi wetu wakuu ipo, tumesikia ushauri wa Mhe. Ali Salim ushauri mzuri mara tutakapopata fedha tutafanya hivyo kama Pemba tayari tumeshapata viwanja na Mfuko Mkuu wa Serikali utaliona hili na sisi tunajitahidi kuhakikisha kwamba nyumba za viongozi wetu zinajengwa ili wake katika makaazi stahiki.

Ni kweli anaweza kuja Makamu wa Kwanza mwengine na akasema pale pasifae ataamua atakapoona inafaa na Serikali ina wajibu wa kumtafutia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Salim Haji: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 2102	- Idara ya Faragha	411,150,000
Jumla ya fungu		2,928,700,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 12 - TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Kifungu 0201 - Utawala Unguja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilikuja mapema kama ulivyoagiza hapa saa 10:30 niko hapa na Mhe. Fatma Fereji alinijibu hoja hii uhakika nilimsikia. Kwa wazo nitalichukuwa na nitalifanyia kazi.

Kuhusu maadili na mporomoko wa mavazi na nguo zetu. akanambia suala hili atalichukuwa na atalifanyika kazi sina tatizo nalo na wala sina nia ya kuzua kifungu. Uzoefu unavyoniambia katika Baraza hili anaweza akachukua lile, lakini likakaa kwenye *door* atwambie huu Mswada lini utakuja?

Mhe. Mwenyekiti: Mswada gani?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa nguo fupi au nguo za uchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim Ayoub ananiuliza mengine ambayo moja kwa moja hayapo kwangu.

Mimi nilisema tutachukuwa sehemu yetu sisi katika suala zima la kuona kwamba maadili ya watu wetu yanakuwa mazuri kwa kukaa na Wizara ya Hahari, Utamaduni, Wizara ya Katiba na Sheria na wote wanaohusika tulizungumze kwa pamoja na ionekane nini kiweze kufanyika. Lakini pia Wizara ya Wanawake na Watoto, Vijana vile vile tunahitaji kulizungumza.

Kwa hiyo, siko katika nafasi ya kumwambia lini nitaleta mswada huo kwa sababu hauko moja kwa moja katika ofisi yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, umemfahamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nimemfahamu Mhe. Mwenyekiti, lakini Serikali yote ndio ipo hapa na wanatusikia na nafikiri Kiongozi Mkuu mmoja kati yao anaweza kuinuka kwa niaba ili wananchi wapate kusikia chombo chao lini kinafanya haki.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub hili suala la Wizara mbali mbali. Ikija Wizara ya Utamaduni utazungumza ndio wahusika zaidi. Tumefahamiaka kwa hivyo, tunaendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0201- Utawala Unguja	608,537,400
Kifungu 0301- Ofisi Kuu Pemba	202,462,600
Jumla ya fungu	811,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU- 51 TUME YA TAIFA YA KURATIBU NA KUZUIA MADAWA YA KULEVYA

Kifungu 5101 Utawala Unguja

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa na mimi kuongea mawili matatu katika kifungu hichi.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilitaka nipate majibu na nilizungumzia suala la kupunguza hapa shilingi juu ya suala zima la matumizi ya choo ambacho kimejengwa *Airport.* Na Mhe. Waziri alipokuja hapa hakunijibu suala hili. Naomba kupata maelezo juu ya suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa alitaka kujua kwa nini choo kile hakitumiki. Naomba kidogo niwarudishe Wajumbe nyuma kwamba suala la ujenzi wa choo kile ni la muda mrefu sana na lilikuwa ni fedha za wahisani tulizosaidiwa na *UNDP* baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuomba kufanyiwa hivyo. Lakini kwa kweli wakati kinajengwa choo kile ilikuwa hakujafanyiwa tafakuri ya kina, kitu gani hasa kinahitaji kiwepo kwa ukamilifu wake. Unajua masuala ya mbinu za kupambana na dawa za kulevya ni masuala kidogo mageni mageni na yanabadilika kadri siku zinavyokwenda. Tukajikuta kwamba choo kile kimewekwa pale na baada ya kukamilishwa miundombinu ya kuweza kutumia choo tunaambiwa na vyombo vya ulinzi na usalama kwamba choo kile hakiwezi kutumika kwa sababu kwanza eneo liliopo si la stara, yaani kile kilifanywa kuingizwa ingizwa tu pale *Airport* iliopo kwa sababu eneo halikuwepo la kutosha. Lakini vile vile kunahitajika kuwekwe *x-ray machine* katika eneo lile lile pale pale mtuhumiwa anapokamatwa kabla ya kupelekwa chooni.

Sasa ukosefu wa miundombinu hiyo imekifanya choo kile kiwe hakiwezi kutumika. Na Serikali imeona basi kwa kuwa sasa tumeingia katika ujenzi wa jengo jipya la Uwanja wa Ndege, tufanye utaratibu sasa wa kuweza kupata sehemu katika jengo jipya. Na kwa kweli tunafanya hivyo kwa mawasiliano na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ili huduma hiyo ya choo iwepo ikiwa kamilifu. Kwa sababu sasa inajulikana kwa ukamilifu kitu gani kinatakiwa kuwepo pale. Kwa hivyo hiyo ndio sababu kwa nini choo kile hakijatumika pamoja na kwamba fedha zilizoletwa na nyengine zetu sisi kimewekwa maji yapo na kila kitu, lakini watu wa vyombo vya ulinzi na usalama wanasema kwamba hakijakamilika kwa matumizi yake.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo napata mashaka. Na kwa kuwa Serikali inawajibika kwa pamoja sijui ni utaratibu gani unaotumika na kuona kwamba baadhi ya miradi yetu mingi sana baada ya utafiti, na kwamba suala hili linaweza kumalizika katika utaratibu fulani. Baadae tunakuja kutumia tena iwe kodi za wananchi au ni mchango wa wahisani kurudia tena kufanya marekebisho kwa suala ambalo tayari watafiti wamekuja wakachungua na kuona kwamba jambo lile linawezekana kwa gharama ya kiasi kadhaa. Na baadae kitu kile kikawa hakifai tukatafuta gharama nyengine. Je, Mhe. Waziri hawa watafiti ambao walikuwa wanafanya kazi hizi, kazi hizi wanapozifanya huwa hawazifanyi kwa uhakika au wanafanya kwa makusudi ili fedha za wananchi walipa kodi ziweze kupotea.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa najibu swali langu nilisema kwamba suala zima la mapambano dhidi ya dawa za kulevya na utaalam wake wa mapambano haya ni mambo kidogo mageni hasa kwa nchi maskini kama zetu. Kwa hiyo awali Jeshi la Polisi wao walizungumza huko na Mkurugenzi wa Mashtaka kwamba tunahitaji kuwa na choo kwa ajili ya kuweka watu wetu hawa wanaoingia na dawa watakaokamatwa, *whether* wetu au wanatoka sehemu nyengine waweze kukitumia choo hicho. Kwa hiyo walipoomba gharama walijua ni choo, lakini sasa kadri siku zinavyoendelea na utaalam na mbinu za mapambano zinavyoendelea wanasema hapana choo hakiwezi kuwa mbali na *x-ray machine* ikawa mbali. Yote haya yanahitajika sehemu ya kutosha yaani iwe nafasi ya kutosha na huduma zote zile ziwe pamoja.

Nimhakikishie Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa kwamba hiki choo kipo kimewekwa vizuri pale lakini bado wenzetu hao hao wa Jeshi la Polisi wanakwenda *training* kila siku na wanatembelea nchi za wenzetu kuona wenzao wanafanya vipi. Wamekisema kwamba kina mapungufu na kwa sasa hakiwezi kutumika. Kwa hiyo utaratibu unafanywa ili tuweze kupata nafasi katika eneo jipya kwa sababu pale tulipo katika *Airport* ile hakuna eneo. Sijui kama amewahi kwenda kutembelea Mheshimiwa au siku moja niweze kumchukua akakione hapo kilipo. Hakuna ujanja wa aina yoyote kuweza kuweka huduma hizo nyengine zinazotakiwa. Kwa hiyo kwa kweli katika mazingira yale choo kile hakiwezi kutumika pale.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka Mhe. Waziri anisaidie. Kwa sababu fedha zile ndio tayari zimekwisha kwenda na tatizo linaonekana litaendelea kuwepo. Ni njia gani mbadala tutakayotumia baada ya kukosekana kwa hii ambayo tulikuwa tunaitarajia.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hata kabla ya choo hiki hakijakuwepo njia mbadala inayotumika ni watuhumiwa hawa kupelekwa hospitali, wanapigwa *x-ray* na yanatumika mabeseni katika kuwaweka sehemu ya stara ili waweze kutoa hicho walichonacho. Hiyo ndio njia mbadala na kwa sasa inaendelea kutumika njia hiyo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa ya kiti chako tuendelee.

Kifungu 5101	Utawala Unguja	304,000,000
Kifungu 5102	Ofisi Kuu Pemba	60,000,000
Jumla ya Fungu		364,000,000

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 06	Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais	
Kifungu 0401	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	2,200,000,000
Jumla ya Fungu		2,200,000,000

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 12	Tume ya Ukimwi	
Kifungu 0201	Utawala Unguja	1,331,410,000
Jumla ya Fungu		1,331,410,000

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)
(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya ofisi yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja ya kwamba Baraza lako liyakubali mabadiliko hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa tuiamue. Wale wanaokubali Hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/15 wanyooshe mkono. Waliokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe tunawashukuru kwa kazi kubwa tuliyofanya na kuweza kupitisha Hotuba ya Mhe. Waziri. Sasa kwa kuwa muda haujamalizika na kazi yetu tumemaliza nimuombe Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atoe hoja ili tuweze kuahirisha.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa shughuli zilizopangwa kwa ajili ya siku ya leo zote zimemalizika. Na kwa kuwa muda wa kawaida haujafikiwa wa kumaliza shughuli zetu. Na kwa kuwa shughuli zimekwisha. Kwa hiyo naomba Baraza lako uliridhie kuahirisha mpaka kesho saa 3:00 asubuhi. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaosema tuahirishe mpaka kesho. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe nishukuru tena kwa ushirikiano wenu mzuri mliotupa na hivi sasa tunaahirisha kikao chetu mpaka kesho Jumanne tarehe 27/05/2014 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:12 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 27/05/2014 saa 3:00 asubuhi)